# Nipashe

Ijumaa Machi 13, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580178

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Uchunguzi sakata la Lugola, Andengenye wafanyiwa kazi

UKURASA 3




UKURASA 13

# JPM amlipia faini Msigwa



**CHADEMA** pia wamlipia, Mnyika, Mwalimu nao mambo shwari, Mdee alonga baada ya kutoka gerezani...*Endelea ukurasa wa 2*



Wabunge wa Chadema, Esther Matiko (Tarime Mjini) na Halima Mdee (Kawe), wakipongezwa na wanachama, katika Makao Makuu ya chama hicho, Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kulipiwa faini na kuachiwa huru kutoka katika Gereza la Segerea. **PICHA: MIRAJI MSALA**



## BAA LA CORONA

SHIRIKA la Ndege (ATCL) limetangaza kusitisha mpango wake wa kuanza safari za Dar es Salaam - Guangzhou, China kutokana na mlipuko wa virusi vya Corona.

## MAMA NA MWANAWE WAUAWA KINYAMA

UKURASA 3

# DPP amkaba koo Lema

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** KAGERE KUVUNJA REKODI YA 'KIATU' MSIMU ULIOPITA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# JPM alimpia faini Msigwa

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli ametoa Sh. milioni 38 kati ya 40 zilizohitajika kumnusuru Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa, kutumikia kifungo cha miezi mitano gerezani baada ya kukutwa na hatia ya makosa manne ya uchochezi.

Jumanne wiki hii, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, iliwahukumu vigogo saba wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na mwanachama mpya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Vincent Mashinji, kulipa faini ya jumla ya Sh. milioni 350,000 au kwenda jela kutumikia kifungo cha miezi mitano kila mmoja.

Juzi, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kilimlipia faini Dk. Mashinji na Chadema ikawalipia faini wabunge watatu; Halima Mdee, Esther Bulaya na Esther Matiko.

Akizungumza na waandishi wa habari nje ya viunga vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jana, Kaka mkubwa wa Mch. Msigwa, Benet Msigwa, alisema wameshakamilisha taratibu zote za kulipa faini na mahakama imetoa kibali cha kwenda kumtoa gerezani ndugu yao.

"Ndugu tumetembeza harambee ya mchango, tumejichangachanga tukapata Sh. milioni mbili, tukaona tumwombe msaada Mheshimiwa Rais kwa sababu mjomba wetu (mpwa) amemuoa binti wa Mheshimiwa Rais.

"Tangu hukumu imetolewa, ndugu tumekuwa kwenye kampeni kubwa ya kutafuta fedha kwa kesi iliyokuwa ikimkabili Mch. Msigwa ndipo tumefanikiwa kupata mchango wa Mheshimiwa Rais," alisema na kumshukuru Rais Magufuli kwa ukarimu wake.

**CHADEMA NAO WALIMPIA**

Wakati familia ya Mch. Msigwa ikichangiwa na Rais Magufuli kumnusuru mbunge huyo kutumikia kifungo gerezani, Mkurugenzi wa Itikadi na Uenezi wa Chadema, John Mrema, alisema jana jioni kuwa chama hicho kilishafanya malipo kwa ajili ya Mch. Msigwa, John Mnyika na Salum Mwalimu na kinachosubiriwa ni taratibu za kufuata ili watolewe gerezani.

Mrema alionyesha stakabadhi ya malipo yaliyofanywa jana kupitia Benki ya CRDB kwa ajili ya kuwanusuru vigogo hao watatu wa Chadema.

"Katika Sh. milioni 234 zilizopatikana kupitia michango ya wanachama na wananchi, bado tunauhitaji wa Sh. milioni 90, simu zote zilijaa, tunawaomba mwendelee kutuma kwa kuwa namba zimefunguka, tunaamini tutapata fedha na kuwatoa viongozi wengine waliobakia," Hezekiah Wenje, mbunge wa zamani wa Chadema alisema jana.

**MACHOZI YA MDEE**

Muda mfupi baada ya kutoka gerezani, Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha), Mdee, aliwaambia waandishi wa habari kuwa wanafikiri hukumu dhidi yao iliandaliwa ili kuwakandamiza.

"Kihitosria, makosa yenye adhabu haijawahi kutokea kwa makosa hayo kutozwa Sh. milioni 10, na kama (washtakiwa) wakikosa fedha hizo wangekwenda jela miezi mitano kwa kila kosa. Lengo lilikuwa ni kutufunga na hadi sasa Mwenyekiti wa Chadema, Mbowe, wamemfilisi mali zake zote. "Walikuwa wanajua sisi si maskini. Mimi Halima Mdee ukienda kwenye akaunti yangu ukikuta milioni moja ni afadhali... wanajua wamefunga akaunti zote, hii adhabu haikuwa bahati mbaya kwa kuwa walijua hatuna hata mia," alalalamika.

Mdee ambaye kitaaluma ni mwanasheria, aliendelea kusema: "Watanzania hamjui mlivyotusitiri... (akalia). Mimi ni kamanda, lakini napata hisia nilikuwa najua tulivyonyong'onyezwa na watu wamekata tamaa, lakini mmetuchangia.

"Tunawashukuru sana kwa kutuchangia, huu ni upendo na bado pesa zinaingia, tunawaomba muendelee kutuchangia na fedha zenu zitaonyesha sauti, mmefanya kazi kubwa, mnakaribia kumaliza, kesho (leo) tumalize tuwatoe kina Mbowe na wenzake," alisema huku akifuta machozi.



Kaimu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, James Kaji, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu Umoja wa Mataifa (UN), kuipongeza Tanzania kwa jitihada za udhibiti na mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# DPP amkaba koo Lema

**Waandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, amemtaka Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema (Chadema), ajitokeze na kueleza lini alikwenda kutoa taarifa kituo chochote cha polisi kuhusu matukio ya watu 14 kuuawa.

Februari 29 mwaka huu, Lema akiwa katika mazishi ya Katibu Mkuu wa Chadema Jimbo la Manyoni Mashariki, Alex Joas, alitaja orodha ya watu 14 waliouawa kwa kuchinjwa na kuchomwa moto wilayani humo.

Hata hivyo, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mganga alimtaka Lema ajitokeze na aeleze lini alitoa taarifa polisi kuhusu matukio hayo ya watu kuuawa na kama jeshi hilo halikuchukua hatua.

"Ajitokeze na aeleze lini alitoa taarifa za hawa watu kuchinjwa na anawafahamu na kwamba polisi wameshindwa kuchukua hatua za kuwakamata waliochinja.

"Tunapochukua hatua, naomba mnielewe, hatuwezi kuendelea kuwa na taifa la watu wenye uzushi, wenye kueneza taarifa zenye taharuki na chuki na kusababisha watu wakae kwa mihemko kwamba hakuna amani.

"Kwa hili ninasema nitachukua hatua, hatuwezi kuendelea na uvunjifu na upotoshaji wa hali ya namna hii halafu watu wanatoka mnaanza kusema wanasiasa wa vyama vya siasa wanaonewa, wakati watu wanafanya upuuzi wa namna hii.

"Haiwezekani, tusijifiche kwenye siasa, uwe CCM, uwe chama chochote kile kwa ajili ya kuvuruga amani ya nchi au kuleta mtafaruku na kuwafanya watu waishi kwa hofu," alionya.

Alipoulizwa hatua ambazo atazichukua dhidi ya Lema, Mganga alisema anazifahamu na pia zinafahamika kwa ofisi yake.

"Mtaziona wakati nitakapozichukua, ninajua kuna hatua nitazichukua, ni lini na ni zipi, mtaziona na mtajulishwa kwa sababu ni hatua ambazo hazifanyiki kwenye kificho labda nitamshtaki au sitamshtaki, nitaangalia.

"Watanzania mnayo haki ya kutoa maoni au mawazo, lakini tusitumie haki hizo kwa maslahi yetu binafsi tuwe wanasiasa au raia wa kawaida.

"Ibara 28 ya Katiba inasema kila raia ana wajibu wa kulinda, kuhifadhi na kudumisha uhuru, mamlaka na umoja wa taifa," alisema.

Mganga alisema lengo la mbunge Lema ni kuwatisha Watanzania wasiishi kwa amani.

**WAHUJUMU UCHUMI**

Mganga pia alisema mpaka sasa, watu 357 waliokuwa na tuhuma mbalimbali ikiwamo uhujumu uchumi waliomwandikia barua ya kuomba kukiri makosa, wameachiwa huru na serikali imepokea Sh. bilioni 13.5.

Hata hivyo, DPP Mganga aliwataka watuhumiwa walioingia mkataba na ofisi yake na mahakama kutoa amri, wazingatie bila kukiuka makubaliano hayo.

"Wasiotimiza na kufuata masharti tuliyokubaliana na ofisi yangu, sitawaacha wakikiuka mikataba hiyo, amri ya mahakama lazima itekelezwe la sivyo tutawachukulia hatua," alionya.

***Imeandaliwa na Romana Mallya na Hellen Mwango***

# ATCL kusitisha safari za China

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKA la Ndege Tanzania (ATCL) limetangaza kusitisha safari za kuelekea katika Jiji la Guangzhou China kutokana na kuwapo na ugonjwa wa virusi vya corona.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Ladislaus Matindi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mkutano wa tano wa Bazara la Wafanyakazi la shirika hilo, kueleza kuwa safari za ndege kuelekea China katika Jiji la Guangzhou zilizopaswa kuanza Aprili mwaka huu hazitakuwapo kutokana na tishio la ugonjwa huo.

"Hatuwezi kwenda sehemu yenye hatari ya kuambukizwa ugonjwa huo, tulipanga kuanza safari Aprili lakini kutokana na mlipuko wa ugonjwa huo nchini humo hatutakwenda tena, tutakwenda pindi hali itakapotengemaa," alisema Matindi.

Matindi alisema ATCL inakabiliwa na changamoto lukuki ikiwamo baadhi ya viwanja vya ndege kutokuwa na taa hali inayosababisha kushindwa kufanya safari nyakati za usiku, baadhi ya viwanja vya ndege kutokuwa na vyumba vya kuhifadhia mizigo hususani inayohitaji ubaridi kama mboga na matunda.

Naye Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, akifungua mkutano huo alisema, ugonjwa wa corona umeleta athari kubwa katika sekta ya anga duniani na kwamba kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (AITA), zilizotolewa hivi karibuni mapato yatokanayo na sekta ya anga duniani yanatarajia kuporomoka kwa asilimia 19.

"Mashirika ya ndege duniani yanatarajia kupata hasara ya Dola za Marekani bilioni 113 kutokana na kutokea kwa ugonjwa huu, mara nyingi ugonjwa wa mlipuko unapotokea sekta ya anga ndiyo ya kwanza kuathirika," alisema Nditiye.

Mhandisi Nditiye alisema licha ya ATCL kusitisha safari kuelekea China, lakini Tanzania haina mpango wa kuzuia ndege za mataifa mengine kuingia nchini kutokana na kuwapo kwa ugonjwa wa virusi vya corona, bali itaboresha upimaji wa abiria wa kigeni wanaoingia katika viwanja vya ndege nchini.

"Vilevile ndege za Shirika la ATCL hazitakwenda kwenye nchi zilizoathirika na ugonjwa wa virusi vya corona, hatuwezi kwenda katika nchi zilizoathirika, na ugonjwa huu endapo ukiendelea kushika kasi katika nchi nyingi duniani tutasitisha safari za nje ya nchi," alisema Mhandisi Nditiye.

Alisema mojawapo ya athari zinazotarajia kutokea nchini kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona ni pamoja na kukosa abiria kwa ATCL pamoja na kupungua kwa baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi.

Nditiye alitoa agizo kwa mamlaka husika kuhakikisha zinaimarisha ulinzi sehemu za mipakani ikiwamo katika viwanja vya ndege ili kuudhibiti ugonjwa wa virusi vya corona kuingia nchini.

## HABARI KITAIFA



Paroko wa Parokia ya Nyololo Jimbo la Iringa, Padre Maraino Passmonte, akizindua kitabu kipya cha 'Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Maendeleo' mjini Iringa jana, kilichoandikwa na waandishi wanne kwa ushirikiano ambao ni Profesa Gaudens Mpangala, Padre Pius Mgeni, Steven Kilasi na Claudis Sabuni. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Mama, mtoto wauawa kinyama, miili yatupwa nyumba ya mjomba

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

MKAZI wa mtaa wa Vuta, Kijiji cha Kizwite, Manispaa ya Sumbawanga, Violet Mafunda (21), ameuawa kwa kuchinjwa na mtoto wake mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu kunyongwa kisha maiti zao kutupwa nje ya nyumba ya mjomba wake na watu wasiojulikana.

Akizungumzia tukio hilo, mjumbe wa serikali ya mtaa wa Vuta, Milton Bonifas, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Machi 11 na watu wasiojulikana walidaiwa kufanya mauaji hayo.

Alisema walipata taarifa kutoka kwa majirani kuwa kuna mwanamke kauawa kwa kuchinjwa akiwa na mtoto wake mgongoni ambaye inadhaniwa kuwa naye alinyongwa katika tukio hilo.

Alisema yeye na mwenyekiti wa mtaa walifika eneo la tukio na kukuta miili hiyo, wa mwanamke ukiwa umechinjwa na kuvuliwa sketi na nguo za ndani, huku akiwa amebeba mtoto mgongoni ambaye naye akiwa amekufa na kulazwa kwenye mfereji wa maji machafu.

Walisema walipoikagua miili hiyo walibaini ni wa Vaileth na kisha kutoa taarifa polisi ambao walifika na kuichukua kwa uchunguzi.

Naye Kefas Lemizio anayeishi jirani na ilipookotwa miili hiyo, alisema walipoamka asubuhi waligongewa mlango na jirani yao na kuambiwa kuwa nyuma ya nyumba yake kuna maiti ya mpwa wake ikiwa imetupwa na watu wasiojulikana.

Monica Kaizya mkazi wa mtaa huo alisema, tukio hilo limewapa simanzi wanawake wa eneo hilo kwa kuwa kitendo kilichofanyika ni ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kuviomba vyombo vya usalama kufanya uchunguzi kuwakamata watuhumiwa na sheria ifuate mkondo wake ili kukomesha vitendo hivyo.

Pia pembeni ya maiti hao walikuta kukiwa na nyanya na vitunguu, nyanyachungu na mboga za majani alizokuwa akiuza mwanamke huyo.

Mwandishi wa habari hizi alipomtafuta kwa njia ya simu Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Justin Masejo, kuzungumzia tukio hilo alijibu kwa ujumbe mfupi wa maandishi kuwa yupo kwenye kikao katika ofisi ya mkuu wa mkoa na hawezi kutoka kwa wakati huo.

# Sakata la Lugola, Andengenye lafanyiwa kazi

**Na Hellen Mwango**

MKURUGENZI wa Mashtaka Nchini (DPP), Biswalo Mganga, amesema bado ofisi yake na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), wanalifanyia kazi sakata la tuhuma za aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola na aliyekuwa Kamishna wa Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye.

Alisema taasisi hizo mbili zina utaratibu wa kufanyakazi na kwamba hakuna jambo la kificho, kila kitu kitakapokuwa tayari umma utafahamishwa kupitia vyombo vya habari.

Akizungumza na waandishi habari ofisini kwake jijini Dar es Salaam, alisema kuna utaratibu wa utendaji wa kazi zao hivyo suala hilo likiiva litawekwa hadharani.

"Kwa sasa sina majibu siwezi kusema jalada la Kangi na Andengenye kama limefika ofisini kwangu au la, sina utaratibu wa kutoa taarifa nusu nusu, muda ukifika nitawaita niwaeleze kinachoendelea," alisema DPP.

Lugola alivuliwa madaraka baada ya Rais John Magufuli kuonyesha kusikitishwa na utendaji wa viongozi wa Wizara ya Mambo ya Ndani hasa utiaji saini wa mkataba wa mradi wa thamani ya Euro milioni 408.

Aliamua kutengua uteuzi wa Lugola wa Uwaziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na nafasi yake kuchukuliwa na George Simbachawene.

Awali, Lugola aliteuliwa kushika wadhifa huo kutoka kwa aliyekuwa akishikilia wizara hiyo, Mwigulu Nchemba, ukiwa ni mchakato wa mabadiliko ya baraza la mawaziri yaliyofanywa na Rais Magufuli, akieleza pamoja na mambo mengine kutoridhishwa na namna ambavyo suala la ajali za mara kwa mara linavyoshughulikiwa, watu kutowajibika kutokana na matukio hayo.






TANGAZO

# WIZARA YA MAJI

## WIKI YA MAJI KITAIFA MWAKA 2020

Tarehe 22 Machi ya kila mwaka ni siku ya Maji Duniani. Maadhimisho haya yanatokana na Azimio Na. 47/193 la Umoja wa Mataifa (UN) kuwa kila ifikapo Machi, 22 ya kila mwaka nchi wanachama ziadhimishe siku ya maji Duniani kwa pamoja.

Maadhimisho haya yanafanyika katika kutambua umuhimu na thamani ya maji katika maisha ya binadamu na uchumi wa Dunia kwa ujumla
Lengo kuu la maadhimisho na matukio ya Wiki ya Maji hapa nchini ni kuungana na Mataifa mengine katika kutathmini utekelezaji, mafanikio, na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa miradi ya maji na kuainisha mikakati ya kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira na kusimamia utunzaji wa rasilimali za maji nchini.

Kaulimbiu ya maadhimisho haya kwa mwaka huu ni "Maji na Mabadiliko ya Tabia Nchi; Uhakika wa Maji Salama kwa Wote". Kitaifa maadhimisho yatafanyika mkoani Dar es Salaam katika ukumbi wa hoteli ya APC, Mbweni kuanzia tarehe 17-22 Machi.

Wiki ya Maji itatumika pia kufanya tathmini ya mafanikio ya sekta ya maji katika kipindi cha miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano (2015-2020), sambamba na hilo yatafanyika maonyesho na ubunifu wa huduma na bidhaa zinazohusiana na sekta ya maji.

Maadhimisho yatajumuisha matukio makuu manne kama ifuatavyo,

1. Tarehe 16 Machi; Uzinduzi wa miradi mbali mbali ya maji iliyokamilika;

   Matukio yatakayofanyika katika Hoteli ya APC Mbweni

2. Tarehe 17-18 Machi; utafanyika Mkutano wa Kisayansi wa Watalaam wa Sekta ya Maji (Scientific Water Conference) ambapo utafanyika uzinduzi wa;
   2.1. Kitabu cha hydrolojia (Hydrological year book)
   2.2. Atlasi ya Rasilimali za Maji (Water Resources Atlas);

   Mgeni Rasmi: Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan

3. Tarehe 19-20 Machi: Siku ya EWURA ambapo ripoti ya Utendaji wa Mamlaka za Maji ya mwaka 2018-2019 itazinduliwa na kujadiliwa

   **Mgeni Rasmi:**
   **Waziri Mkuu wa**
   **Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
   **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**

4. Tarehe 21 Machi; utafanyika Mkutano Mkuu wa Wadau wa Sekta ya Maji (Joint Water Sector Review) ukiambatana na;

   4.1. Mapitio ya taarifa ya hali ya sekta ya maji kwa muda miaka mitano (Water Sector Status Report : 2015-2020)

**Katibu Mkuu**
**WIZARA YA MAJI**

# HUDUMA YA MAJI INAIMARIKA

Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 kipaumbele katika matumizi ya maji kimewekwa katika upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, ikifuatiwa na mazingira na hatimaye matumizi ya maji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii. Wizara ya Maji ina jukumu la kusimamia moja kwa moja huduma ya maji majumbani pamoja na matumizi mengine.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo anasema kutokana na mahitaji yanayoongezeka kutokana na idadi ya watu ni muhimu kuwa na Grid, mtandao mkubwa wa maji.

"Ni muhimu kabisa tuwe na grid ya maji, kama ulivyo umeme, kutoa maji katika eneo moja hadi jingine" Prof. Kitila anasema na kuongeza mabadiliko yanayofanyika katika sekta ya maji yameenda sambamba na wataalam wa sekta hiyo kuonyesha uwezo na morali ya kazi.

Prof. Kitila anaongeza kuwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) imeanzishwa ili kutatua changamoto za miradi ya maji vijijini, hivyo inawajibika kusimamia utekelezaji wa miradi na utoaji wa huduma ya maji vijijini. RUWASA inafanya kazi kwa kaulimbiu "Maji Bombani".

Juhudi zinazochukuliwa na Serikali zimeimarisha sekta ya maji ambapo Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi mwezi Desemba 2019, jumla ya miradi ya maji 1,423 vijijini na mijini imeendelea kutekelezwa, ikiwemo miradi 1,268 ya vijijini na miradi 155 ya mijini. Jumla ya miradi 792 imekamilika ambapo miradi 710 ni ya vijijini na 82 ni ya mijini. Miradi 631 inaendelea kutekelezwa, ikiwemo miradi 558 ya vijijini na miradi 73 ya mijini.



*Waziri wa Maji Mhe. Profesa Makame Mbarawa akiangalia ubora wa kizimba na bomba zilizotumika katika kizimba cha kupunguza msukumo wa maji (BTP) katika eneo la mashamba la Simba. BTP moja ya kazi yake ni kuzuia mabomba kupasuka. Mradi wa maji wa Longido bomba kuu limelazwa kwa umbali wa kilomita 94. Thamani ya mradi ni kiasi cha Shilingi bilioni 15.7.*

Matokeo ya hatua hizi yanaonekana na kujidhihirisha kwa tafiti mbalimbali zinazofanyika kuhusiana na huduma za maji. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Bajeti Katika Kaya (Household Budget Survey) ya mwaka 2019 iliyotolewa na Shirika la Taifa la Takwimu (National Bureau of Statistics-NBS), hadi kufikia mwezi Juni 2019, asilimia 64.8 ya wananchi vijijini tayari walikua wanapata huduma ya maji kutoka vyanzo vya maji vilivyo safi na salama. Taarifa hiyo inawiana kwa karibu na takwimu zilizopatikana kupitia utafiti uliofanywa na Wizara.

Aidha, kwa mujibu wa takwimu za upatikanaji wa huduma ya maji zinazokusanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kila mwezi kupitia mtandao wa MajIs, asimilia 84 ya wananchi waishio makao makuu ya mikoa na asilimia 60 ya wananchi waishio katika makao makuu ya wilaya na miji midogo wanapata maji safi na salama kupitia mamlaka za maji.

Kazi inafanyika ili kufikia malengo yaliyowekwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kuwafikisha Watanzania huduma ya maji kwa asilimia 85 vijijini na asilimia 90 katika miji midogo/makao makuu ya Wilaya; na asilimia 95 katika makao makuu ya Mikoa.
Miradi inayotekelezwa itafikisha huduma ya maji ya kutosha kwa wananchi kwa sababu Tanzania ina rasimali za maji za kutosha. Taftishi zilizofanywa na Wizara mwaka 2019 zimeonesha kuwa rasilimali za maji zilizopo na zinazofaa kwa matumizi mbalimbali ni wastani wa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka. Kiwango hiki kinagawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni maji juu ya ardhi (mita za ujazo bilioni 105) na maji chini ya ardhi (mita za ujazo bilioni 21) kwa mwaka.

Kiasi hicho cha maji kikilinganishwa na idadi ya watu milioni 54 (takwimu ya mwaka 2018) inaonesha kuwa kiasi cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa mita za ujazo 2,300. Kiasi hiki ni juu ya wastani wa mita za ujazo 1,700 ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa. Chini ya kiwango hicho, nchi huhesabika kuwa na uhaba wa maji (water stress).

Hadi mwaka 2019, mahitaji ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali nchini kama vile majumbani, umwagiliaji, viwanda na mazingira yalikua wastani wa mita za ujazo bilioni 40 kwa mwaka, sawa na asilimia 31.7 ya rasilimali zote za maji zilizopo nchini.

Wizara ya Maji inawajibu wa kusimamia rasilimali za maji ambapo kupitia Bodi za Maji za Mabonde huhakikisha rasilimali hiyo inahifadhiwa, inalindwa, inatunzwa na kuendelezwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Aidha, Bodi za Maji za Mabonde huhakikisha rasilimali za maji zilizopo nchini zinagawiwa katika uwiano ulio sawa kwa matumizi mbalimbali.

215667502

HABARI KITAIFA

# Serikali yafuta rasmi leseni TanzaniteOne

**Na Mwandishi Wetu**

Wizara ya Madini imesema hakuna majadiliano yoyote yanayoendelea kati ya serikali na Kampuni ya TanzaniteOne na badala yake leseni ya Kitalu C iliyokuwa inamilikiwa na kampuni hiyo kwa ubia na Shirika la Madini la Taifa (Stamico) imefutwa.

Kwa mujibu wa sheria, wizara imesema tayari eneo hilo limerudishwa serikalini na hakuna mwekezaji mpya.

Waziri wa Madini, Doto Biteko, na Katibu Mkuu wake, Prof. Simon Msanjila, walisema juzi kwa nyakati tofauti wakati wa kikao kazi kati ya wizara na kamati ya eneo lililodhibitiwa la Mirerani, kilichofanyika jijini Dodoma.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Mkurugenzi wa Leseni Tume ya Madini, Mhandisi Yahaya Samamba, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mhandisi Joseph Nyamhanga, Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zephania Chaula ambaye ni Mwenyekiti wa eneo lililodhibitiwa la Mirerani na Uongozi wa Tume ya Madini.

Biteko alisema hatua ya kufuta leseni hiyo ilitokana na maelekezo yaliyotolewa na Bunge na Serikali baada ya Kamati Maalum iliyoundwa kuchunguza biashara ya Madini ya Tanzanite kubaini kuwa leseni hiyo ilitolewa kinyume cha sheria.

Waziri Biteko aliongeza kuwa kwa sasa serikali inaangalia namna bora ya kuligawa eneo hilo kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu ili kuhakikisha madini ya tanzanite yanakuwa na manufaa zaidi kwa taifa na kuchochea ustawi na maendeleo ya nchi kupitia madini hayo. Aliongeza kuwa serikali iliwashirikisha wadau kupata maoni ya namna ya kuligawa eneo husika.

"Serikali nzima inaangalia eneo la Mirerani, eneo hilo linahitaji mazingira rafiki ili wachimbaji wafanye shughuli zao kwa amani na usalama na serikali ipate mapato yanayostahili. Wajibu wetu wizara ni kuhakikisha ukuta wa Mirerani unapandisha mapato ya serikali," alisisitiza.

Aliongeza kuwa ndoto yake akiwa Waziri wa Madini ni kuona biashara ya tanzanite inafanyika ndani ya ukuta katika Kituo cha Pamoja cha Biashara ya Madini ya Tanzanite kilichojengwa na serikali na kuongeza kuwa serikali haizuii madini hayo kuuzwa katika masoko mengine.

Biteko alitaka mamlaka zinazohusika na usimamizi wa eneo hilo kuhakikisha zinatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa bila kuvuruga taratibu na kuongeza kuwa: "Tume ya Madini iliundwa maalum kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali madini."

Katika hatua nyingine, Waziri Biteko alizitaka ofisi za madini nchini kuhakikisha zinatoa ushirikiano kwa taasisi nyingine za serikali katika masuala yanayohusu sekta ya madini ili kuweka mazingira rahisi ya utekelezaji wa majukumu katika sekta, zikiwamo kamati za ulinzi na usalama katika maeneo husika.

Naye Dk. Mwinyi aliishauri wizara kutoa taarifa kwa wizara hiyo endapo itakuwa na mahitaji maalum ya ulinzi katika eneo hilo na kutumia fursa hiyo kukipongeza kikosi maalum kinachofanya kazi eneo hilo kwamba, kinatekeleza wajibu wake ipasavyo.

"Nafurahi kusikia kwamba jeshi Mirerani linatekeleza majukumu yake kikamilifu na hakuna mwingiliano. Endapo mtakuwa na mahitaji maalum mtatutaarifu sisi," alisema.

# Makandage apewa wiki kuwasilisha maombi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imetoa siku saba kwa mshtakiwa Joseph Makandage, kuwasilisha maombi nje ya muda kwamba hati ya mashtaka ya kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili na wenzake wawili ina upungufu kisheria.

Makandage aliwasilisha maombi hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, wakati kesi hiyo ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upande wa Jamhuri baada ya kupitia maombi ya mfanyabiashara James Rugemalira, unaomba mahakama kuyatupilia mbali kwa sababu haina mamlaka ya kutoa maamuzi yake.

Pia alidai kuwa maombi hayo yamewasilishwa wakati si muafaka.

Katika maombi yake, Makandage anadai kuwa hati ya mashtaka dhidi yao ina upungufu wa kisheria na kuiomba mahakama kuitupilia mbali iwaachie huru au itoe amri nyingine yoyote ambayo inaona inafaa.

Hakimu alisema mahakama yake inatoa siku saba kwa Makandage kuwasilisha maombi yake na kesi hiyo itatajwa Machi 26, mwaka huu.

Mapema mahakamani hapo, Rugemalira aliwasilisha hoja za awali, kuomba kuondolewa katika kesi ya uhujumu uchumi na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP).

Alidai mahakamani kuwa aliandika barua kwa Kamishna wa TRA kupitia mjumbe wa Takukuru aliyetembelea gerezani akielezea jinsi Benki ya Standard Chartered Hong Kong, inavyokwepa kodi, huku akieleza kuwa wanaostahili kujumuishwa kwenye kesi ni benki hiyo na si yeye.

Pia, alidai aliandika notisi kwa taasisi tisa ikiwamo Usalama wa Taifa (TISS) akitaka DPP awasilishe hati ya kuachiwa kwake na asipofanya hivyo atawasilisha hoja ya kuiomba mahakama imwondoe katika kesi hiyo.

Mbali na Rugemalira, wenzake ni Harbinder Sethi na Makandege.

Katika kesi ya msingi, Makandage anakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kusababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000 pia yapo ya utakatishaji wa fedha.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Bravo Msajili Vyama vya Siasa kwa ufafanuzi huu

**JUZI** Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Mohammed Ali Ahmed, aliwatoa wasiwasi wadau wa siasa nchini na umma kwa ujumla, kwa kuvihakikishia vyama vya siasa kuwa hakuna kitakachofutwa kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Naibu Msajili huyo alifafanua kwamba sheria ya vyama vya siasa haimpi mamlaka Msajili wa Vyama vya Siasa kufuta chama chochote kabla ya miezi 12 (yaani mwaka mmoja) kabla ya uchaguzi, na kama ingekuwa ni kufuta jambo hilo lingefanyika miezi 12 kabla ya Oktoba mwaka huu.

Ufafanuzi huu unakuja siku chache baada ya Ofisi ya Msajili kutangaza kuanza kufanya uhakiki wa vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu ambavyo ni 19.

Mambo yatakavyoangaliwa ni kama chama kina ofisi, mahesabu yake yako vizuri, kimesajiliwa na kadi za wanachama ziwe na picha zao.

Ofisi hiyo ilifafanua zaidi kuwa uhakiki huo unalenga kuwekana sawa na kama kutakuwa na kasoro, watapewa muda wa kujirekebisha, na kwamba jambo hilo halikuwa na lengo la kufuta chama na kwamba kama kutakuwa na kasoro, kutakuwa na muda wa kuzirekebisha kasoro hizo.

Aidha, alisema lengo ni kuhakikisha vyama vyote vya vinatulia na kukaa kwenye mstari kwa kuwa wakati wa Uchaguzi Mkuu watakuja waangalizi kutoka nje ambao watapita kwenye vyama.

Hizi zimekuwa habari njema kwa umma, wadau na vyama vya siasa, ambavyo baada ya kusikia habari hizo vilihisi kuwa lengo kuu la kufanya uhakiki ni kuvifuta na kuzua taharuki ikiwa imebaki miezi takribani saba kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu.

Baadhi ya wafuasi wa vyama vya siasa na wadau walikuwa wanalalamika na kudai kuwa kuna nia ya kufuta vyama katika kipindi hiki ambavyo vyote vipo kwenye maandalizi ya kuelekea uchaguzi huo, ingawa hakukuwapo mamlaka ya serikali iliyokuwa imethibitisha taarifa hizo.

Kwa ujumla kitendo cha msajili kujitokeza hadharani na kutuliza hali ya wasiwasi iliyoanza kujitokeza kwenye vyama na wadau, ni cha kupongeza kwa kuwa sasa hali ya utulivu inakwenda kurejea miongoni mwao.

Ufafanuzi kama huu unahitajika pale linapotokea jambo linalogusa maslahi ya wengi kwenye jamii, ili kuondoa wasiwasi au namna yoyote ya kuwafanya watu wasitulie kutokana na kuwapo kwa taarifa potofu.

Vyama vingi kwa sasa akili ziko kwenye kujiimarisha kuelekea uchaguzi mkuu, hivyo vinapokumbana na vikwazo ambavyo ni tishio kwao wasiwasi unapandisha joto lao na kushindwa kufanya vyema kwenye shughuli zao za kisiasa.

Hatua ya Msajili kulitolea suala hilo ufafanuzi ina tija kwa sababu inarejesha imani ya vyama vya siasa, wadau na umma kwa ujumla kwa taasisi hiyo, ambayo ndiyo mlezi na msimamizi wa vyama vya siasa.

Pia inaweka mazingira ya kuvijengea imani vyama, wadau na umma kuelekea uchaguzi mkuu kwamba hakuna mamlaka yoyote ya serikali yenye nia mbaya ya kuvifuta bila kufuata taratibu za kisheria.


Sisi tunaona kuwa vyama vinapaswa kutoa ushirikiano kwa kujiweka sawa na uhakiki huo kwa kuwa umeeleza bayana mambo yatakayoangaliwa kwenye suala hilo, kwa kuwa lengo ni zuri la kuhakikisha kuwa vyama vya siasa vinazingatia sheria ya Vyama vya Siasa Namba 5 ya mwaka 1992.

Ihakiki hio ni muhimu kwa kuwa kwa kipindi kirefu tumeshuhudia baadhi ya vyama vikishindwa kuzingatia sheria hiyo hususan kutokuwa na ofisi zinazoeleweka nchi nzima, wanachama na kutokufanya shughuli za kisiasa hadi wakati wa uchaguzi.

Ndio maana baadhi ya vyama vya siasa vimekuwa vikiitwa 'vyama vya uchaguzi'.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






**Muungwana Lazima Nilonge**

# Suala la taulo za mabinti, tuzame kujua ya shuleni

Na Yasmine Protace

MTOTO wa kike anakumbana na changamoto ambazo zinaanzia nyumbani au shule. Ni hali inayochangia hata kushindwa kusoma vizuri au kutohudhuria vipindi darasani.

Ni changamoto inayoweza kumkuta mtoto wa kike, anatumikishwa kazi nyingo pasipo kuwa na fursa ya kupumzika, hali inayochangia asiweze kujisomea kwa usahihi, sababu kuu ni kukosa muda sahihi wa kufanya hayo muhimu katika talauma, ndani ya muda muafaka.

Iko bayana, kuwapo changamoto nyingine inayohusiana na hilo, ni binti anapokuwa kwenye hedhi, anaweza akawa amepatiwa taulo la kujisitiri, lakini shule anayosoma haina maji au inakosa chumba maalumu cha kumhudumia.

Ni hali inayoyosababisha mtoto kushindwa kuhudhuria masomo, kutokana na kukosa chumba au maji na anapokuwa katika siku hedhi, analazimika kubaki nyumbani, ili aweze kujihudumia vizuri na anaporejea hali ya kawaida, anarudi shuleni kuendelea na masomo kama kawaida.

Imo katika kinachosababisha watoto wasihudhurie masomo, kwa kukosa maji au kutokuwapo vyumba vya kujisitiri katika shule zao.

Katika kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani, asasi ya TGNP Mtandao iliandaa maadhimisho kwa kushirikiana na vituo 14 vya Taarifa na Maarifa vilivyopo katika Wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam.

Hapo, baadhi ya wanafunzi walishiriki katika maadhimisho na walitumia nafasi husika kutoa yao ya moyoni.

Walisema kwa nyakati tofauti kuwa, wanakumbana na changamoto ya kushindwa kuhudhuria masomo kutokana na shule zao kutokuwa na miundombinu ya maji.

Anasema, mmoja wa wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Mabibo jijini Dar es Salaam, kuwa shule yao haina maji ya uhakika na watoto wa kike wanapoingia katika hedhi, wanakosa maji, ni sababu inayomfanya ashindwe kuhudhuria masomo.

Niseme kuwa ni jambo jema mabinti hao wanapewa taulo, lakini kuna sura ya pili, bado tatizo lipo katika suala la upatikanaji maji. Kwa kweli, ni changamoto!

Ushauri wake ni kwamba, kinachotakiwa sasa kuangaliwa ni umuhimu wa shule zikawa na maji ya kutosha, ili wasichana hao wanapokuwa katika hedhi, iwepo huduma kwao ya kiafya na utetezi wa nafsi binafsi

**Anasema, mmoja wa wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Mabibo jijini Dar es Salaam, kuwa shule yao haina maji ya uhakika na watoto wa kike wanapoingia katika hedhi, wanakosa maji, ni sababu inayomfanya ashindwe kuhudhuria masomo.**

Husna Said, ni mwanafunzi wa chuo kimoja akipata mafunzo ya ufundi umeme, jijini Dar es Salaam, anasema katika kumtambua mwanamke masomoni, pia wakumbukwe wasichana walio nje ya shule.

Anasema kuwa, wapo wasichana wanaoishia darasa la saba na kushindwa kuendelea na masomo, lakini wanapokumbana na changamoto, matatizo yao wanabaki njia panda, nani wa kumwambia?

Kwa mujibu wa Husna, haki mara nyingi inapigiwa kelele kwa mabinti walio masomoni na kuwaacha njia panda, walio nje ya masomo, hawana mwelekeo kamili, upande upi atapaza sauti yake.

Anasema watoto wengi wanapotea kimaisha, kupitia changamoto zinazoanzia majumbani. Ni aina ya mtazamo inaoibua haja ya utetezi kutoka kwa watoto, unaoweza kufanywa, ingawa najua katika baadhi ya maeneo umeanza, watembelewe mitaa,wasikilize na kutatuliwa kero zao, hiyo ndio sehemu ya utekelezaji sahihi wa haki ya mwanamke.

TANGAZO


SAMSUNG
24 MONTH WARRANTY FOR AFRICA
Kuwa wa kwanza!
Nunua Galaxy S20 Series
SPACE ZOOM 100X
SAMSUNG
SAMSUNG
Pata GB78
BURE!
Mwaka mzima
Galaxy S20
Tsh2,235,000
Galaxy S20+
Tsh2,480,000
Galaxy S20 Ultra
Tsh3,100,000
4G+
Nunua sasa kwa www.tigo.co.tz au kwenye Duka la Tigo.
*Vigezo na Masharti kuzingatiwa.
tigo
215667402

# Mafuriko yaharibu madaraja, makazi Malinyi

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

MVUA zilizonyesha siku chache zilizopita wilayani Malinyi mkoani Morogoro, zimesababisha kukatika kwa mawasiliano ya barabara na madaraja katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo, likiwamo daraja la Mto Furua.

Daraja hilo lipo njia ya kuelekea hospitali kuu ya Wilaya ya Lugala, jambo linalosababisha wananchi kutumia mitumbwi kuvuka upande mmoja kwenda mwingine, huku mtu mmoja akijeruhiwa na mamba wanaotoka mtoni kuingia kwenye makazi.

Mkuu wa Wilaya ya Malinyi, Mathayo Masele, alisema mvua hiyo imesababisha wagonjwa na watu wengine wanaotaka kwenda hospitali ya Lugala kutumia mitumbwi baada ya kukatika kwa daraja linalounganisha vijiji vya Visegese na Lugala.

"Hivi tunavyoongea kuna mtu mmoja alikuwa akitoka Kilosa kwa Mpepo ameshambuliwa na mamba, bahati alikuwa na wenzie wakapambana akajeruhiwa kwa kunyofolewa sehemu za nyama ya mwili wake, na hivi sasa amepelekwa hospitali kwa matibabu,"Alisema Masele.

Alisema kumekuwa na athari kubwa kwani maji yamejaa kwenye makazi ya watu, kuvamia mashamba lakini kikubwa zaidi ni miundombinu ya barabara hasa zinazosimamiwa na Tarura ikiwamo barabara ya Visegese-Lugala inayounganisha wakazi waliopo upande wa wanaotokea Ifakara na waliopo mjini. Pia inahudumia wanaokwenda Hospitali ya Lugala.

Alisema katika barabara hiyo daraja limeondoka takribani mita 45 na vipande vya tuta, na kwamba jitihada wanazofanya ni kurejesha mawasiliano ya barabara angalau watu wapite, baiskeli na pikipiki katika hatua za awali.

"Machi 8 kuanzia saa mbili usiku hadi kesho yake mvua ilinyesha na athari tukaziona Machi 9, lakini Machi 10 tena kuanzia majira ya saa mbili hadi tisa usiku ilinyesha mvua ambayo imeendelea kusababisha maji kujaa maeneo mengi ya mji kutokana na mto Furua kujaa," alisema na kuendelea.

"Tunaathiriwa pia na mvua zinazonyesha maeneo mengine ikiwamo Wilaya ya Ulanga."

Kuhusu athari za moja kwa moja ya wananchi kuchelewa kupata huduma wakiwamo wagonjwa, kuna athari pia kwa wanafunzi kushindwa kuvuka upande mmoja kwenda mwingine, na kwamba wametoa maelekezo kwa walimu na wazazi wasiruhusu watoto waende shule wakati huu wanapoendelea kurejesha mawasiliano.

"Halmashauri na mimi hatuwezi kufanya kazi zetu sawa sawa, tumelazimika kuhamia ofisi mpya, hatuwezi kwenda kule (ofisi zao za kawaida) hata magari yote yapo upande wa pili,ukitaka kwenda huko ni lazima utumie pikipiki tena kwa ugumu."

Alisema baadhi ya shule zimeathirika kwa wanafunzi kushindwa kuvuka kutokana na kukatika daraja au maji kubomoa barabara ikiwemo sekondari ya Malinyi Day, Kipingo na Igawa huku shule za msingi zikiwa ni Malinyi, Lugala, Igawa.

Mkuu huyo wa wilaya aliwaonya wanaoishi karibu na mto Furua na wanaofanya shughuli za kibinadamu kando ya mto huo kuhama na wanaopitisha mifugo katika mto huo kuacha badala yake watumie maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya mifugo.


The Guardian Limited

JOB VACANCY

The Guardian Limited ,publisher of leading Tanzania newspapers, The Guardian and Nipashe, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:

CIRCULATION FIELD OFFICER – DAR ES SALAAM

Job Purpose:

To boost copy sales and develop relationships with agents and vendors in the sales channel in the assigned area to meet your set sales targets.

Main Responsibilities:

The successful candidates will be responsible for the following key results:

- Work with the agents and vendors in making sure that the business grows and The Guardian Limited publications are available and visible and sold at the set retail prices with optimal return levels.
- Develop and grow more channels of distribution.
- Monitor indicators relating to market arrivals, circulation sales and returns indicators and make appropriate reports to Circulation Supervisor.
- Identify and build rapport with existing and potential customers by communicating the benefits of Selling The Guardian and Nipashe.
- Monitor newspaper distribution and sale trends in particular areas, prepare weekly sales plans and update supervisor on a regular basis.
- Monitor daily performance of TGL brands in your particular areas of operation in comparison to our rival publications and make reports that guide growth strategies.
- Open up new markets in particular areas of operation that will in turn translate into higher sales.
- Attend customer complaints that in one's particular area of operation so as to maintain good customer relations and protect the company's interests.
- Liaise with supervisor in credit control and debt management within particular area of operation.
- Submit daily and weekly reports on progress on activities, including meeting set sales targets.
- Manage debt collection and credit control within one's respective area operation.
- Demonstrate ability to work under minimum supervision.

Minimum Qualifications and Experience:

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 2 year's relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge, and familiarity with a wide range of newspapers brands.

MODE OF APPLICATION:

Apply online via HRO email address: ;**vacancy@guardian.co.tz** by March 13, 2020

NB: Only shortlisted candidates will be contacted.

***The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

615654302


# Wagonjwa 56 wapandikizwa figo Muhimbili

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), imepandikiza figo kwa wagonjwa 56 katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia Novemba 2017, hivyo kusaidia kuokoa Sh. bilioni tano ambazo zingetumiwa na serikali kuwapeleka nje ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Museru, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, katika kuadhimisha Siku ya Figo Duniani iliyowashirikisha viongozi wa dini kwa ajili ya kuhamasisha jamii kujikinga dhidi ya ugonjwa huo.

Kaulimbiu katika siku hiyo inasema 'Afya Bora kwa Kila Mmoja na Kila Mahali, Kuzingatia Kinga, Kutambua Ugonjwa Mapema na Kuwe na Fursa Dawa kwa Wote Katika Tiba'.

Prof. Museru alisema upandikizaji wa figo kwa wagonjwa hao 56 umegharimu Sh. bilioni 1.680 sawa na Sh. milioni 30 kwa mgonjwa mmoja na kwamba kama wangeenda nje ya nchi, serikali ingetumia Sh. bilioni 6.720 sawa na Sh. milioni 120 kwa kila mgonjwa.

**"Katika hatua hii watu wasio na undugu nao watanufaika ikiwamo mke na mume kwa sababu awali tulikuwa hatufanyi kwa kundi hili," alisema Prof. Museru.**

Alisema kabla ya kuwapo kwa huduma hiyo nchini, serikali ilipeleka wagonjwa 150 nje ya nchi katika kipindi cha miaka 15 ambao ni wastani wa wagonjwa 10 kwa mwaka.

"Lakini katika miaka miwili, Muhimbili imefikia asilimia 35 ya wagonjwa waliopelekwa nje ya nchi kwa kipindi cha miaka 15," amesema Prof. Museru.

Alisema katika kipindi hicho, MNH imefanikiwa kupandikiza figo wagonjwa waliokua na vihatarishi kiwango cha chini na pia wenye undugu wa karibu kama mtoto, baba, mama, kaka na dada .

Alisema kundi hilo ni la wagonjwa ambao walikuwa na shida ya figo lakini hawana changamoto nyingine.

Kadhalika alisema kutokana na utoaji huduma hiyo kuimarika, Muhimbili itaanza kupandikiza figo kwa wagonjwa wenye vihatarishi kiwango cha juu wakiwamo wagonjwa wenye maambukizi ya HIV na Homa ya Ini, wagonjwa waliowahi kupandikizwa figo lakini imeshindwa kufanya kazi vizuri hivyo kuhitaji upandikizaji mara ya pili.

"Katika hatua hii watu wasio na undugu nao watanufaika ikiwamo mke na mume kwa sababu awali tulikuwa hatufanyi kwa kundi hili," alisema Prof. Museru.

Kuhusu watoa huduma, alisema Madaktari Bingwa wa Figo wana uwezo wa asilimia 100 wa kufanya maandalizi ya uchunguzi kwa mgonjwa ili apandikizwe figo.

Alisema Madaktari Bingwa wa Upasuaji wana uwezo wa asilimia 100 wa kufanya upasuaji kwa anayetoa figo na asilimia 100 kupandikiza figo kwa anayepokea.

# Mwanamke afungwa kifungo cha nje mauaji ya mwenzake

**Na Said Hamdani, LINDI**

MKAZI wa Kijiji cha Rondo Ntene, Wilaya na Mkoa wa Lindi, Asha Mshamu Rashid (55), amehukumiwa kutumikia kifungo cha nje miezi 12, baada ya kupatikana na hatia ya kumuua bila kukusudia Zainabu Mikumbu.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara, Paul Ngwembe, baada ya mshtakiwa kukiri kosa.

Kabla Jaji Ngwembe hajatoa hukumu katika shauri namba 34/2019, Wakili Raynery Songea, aliyekuwa akimtetea mshtakiwa aliiomba Mahakama kumpatia mteja wake adhabu nafuu, ikizingatia ni mkosaji wa mara ya kwanza, anao umri mkubwa na chanzo cha kosa ni marehemu.

Baada ya ombi hilo, Jaji aliwauliza wanasheria wa serikali, Rabia Ramadhani na Abdurahamani Mohamedi kama wana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa, na kujibu kuwa hawana, huku wakiiomba mahakama kuona adhabu itakayomfaa mshtakiwa kwa kosa alilolifanya.

Jaji Ngwembe akitoa hukumu kupitia vifungu vya 195 na 198 alimuhukumu Asha Mshamu Rashiudi kutumikia kifungo cha nje cha mwaka mmoja, asifanye kosa ndani ya kipindi hicho.

Pia, Jaji Ngwembe alisema iwapo mshtakiwa atashindwa kutekeleza hilo ndani ya kipindi hicho, akifanya kosa atalazimika kutumikia kifungo cha miaka mitano gerezani.

Awali ilidaiwa na wanasheria wa serikali kuwa Juni 29, 2019 huko Rondo Ntene, Wilaya na Mkoa wa Lindi, mshtakiwa bila ya kukusudia alimuua Zainabu Mikumbu kwa kumpiga kichwani na mpini wa jembe katika ugomvi wa kugombea panga.

Ilidaiwa kuwa Zainabu akiwa anarejea kutoka shambani bila ya kujitambua alidondosha panga, lakini alishtuka baada ya kufika nyumbani kwake.

Ilidaiwa siku iliyofuata Asha akiwa ameenda shambani kukata nyasi za kuezekea nyumba yake, alifuatwa na Zainabu na kumdai ampatie panga lake, akidai ndiye aliyeliokota.

Ugomvi huo ulisuruhishwa na viongozi wa serikali ya kijiji bila mafanikio, na siku iliyofuata ndipo Zainabu alimfuata mshtakiwa shambani na kuanza kumpiga mgongoni na mpini wa jembe.

Hata hivyo, ilidaiwa katika kujitetea, mshtakiwa aliuchukua na kumpiga nao kichwa kisha kuanguka chini na kupoteza maisha.



Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Vickness Mayao (katikati), akikata utepe kama ishara ya kuzindua Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni wadau wa kutetea haki za binadamu. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Redcross yachangia damu wajawazito

**Na Mwandishi Wetu, Pemba**

WANACHAMA wa Tanzania Redcross Society Mkoa wa Kaskazini Pemba, wamechangia jumla ya chupa 20 za damu ili kusaidia wajawazito.

Akizungumza baada ya zoezi wilayani Wete, kisiwani Pemba, katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Katibu wa Chama hicho Mkoa wa Kaskazini Pemba, Asya Mohammed Omar, alisema kuwa wameamua kufanya hivyo ili kusaidia kinamama hao wanapojifungua.

Alisema kuwa sababu nyingine ambayo imewafanya waiadhimishe siku hiyo ni kuielewesha jamii juu ya umuhimu wa kuchangia damu kwani matatizo haya yanaweza kumfika kila mwanadamu.

Naye Mratibu wa Kitengo cha Damu Salama, Abdi Kassim Hamad, aliwapongeza wanachama wa Tanzania Redcross kwa uamuzi wao huo kwa kuandaa zoezi hilo kwa kujua umuhimu wa uchangiaji damu na kutambua shida kubwa wanayopata kinamama wanapokuwa wajawazito.

## Viwanda vyaanzishwa kuwasaidia wasichana

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

VIWANDA vinne vimeanzishwa wilayani Iringa na Shirika la Camfed kwa lengo la kuwasaidia wasichana waliohitimu elimu katika ngazi mbalimbali kuyaongezea thamani ya mazao.

Miongoni mwa mazao hayo ni mpunga, mahindi na alizeti. Makamu Mwenyekiti wa Mtandao wa wanufaika wa ufadhili wa masomo kutoka Shirika la Camfed Taifa (CAMA), Latifa Kiyao, alisema kuwa viwanda hivyo vinne vitawasaidia wasichana kuondokana na utegemezi kuwaimarisha kiuchumi zaidi ya wasichana 2000.

"Miradi hii yote tunasimamia kama wasichana ili kujiinua kiuchumi na kuondokana na hali ya utegemezi kupitia miradi ya mashine za cherehani, mashine ya ukoboaji wa mpunga, ufugaji wa kuku wa kisasa, uchakataji wa mahindi na mashine ya uchakataji alizeti ya kisasa," alisema Kiyao.

# Sababu RC kuvifuta viwanja 12,000

**Na Said Hamdani, LINDI**

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, kupitia kamati aliyoiunda kufuatilia migogoro mbalimbali inayowakabili wananchi, ikiwamo ya ardhi, amevifuta viwanja 12,000 vilivyopimwa visivyo halali katika Wilaya ya Nachingwe.

Zambi aliyaeleza hayo alipokuwa akizungumza na watumishi wa idara mbalimbali katika Manispaa ya Lindi wakati wa kikao kazi.

Alisema amefanya uamuzi wa kuvifuta baada ya kubaini kasoro mbalimbali, zikiwamo kutotambuliwa waliohusika na kazi ya upimaji wa viwanja hivyo kutokuwa na elimu pamoja na kutofahamika na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, hali iliyosababisha migogoro lwa wananchi.

Mkuu huyo wa Mkoa wa Lindi alivitaja vijiji au maeneo yaliyohusika na ufutaji wa viwanja hivyo ni Boma, Nachingwea, Ugawaji, Namatura na Nangoe.

Alisema kutokana na kuwapo kwa mgogoro huo, yeye kupitia kamati aliyoituma kufuatilia, ikiongozwa na Katibu Tawala wa mkoa, Rehema Madenge, ilibaini viwanja halali vinavyotambuliwa na wizara husika vipo 1,724, huku 12,000 vikiwa nje ya utaratibu.

"Baada ya kamati niliyoiunda kubaini tatizo hilo, nimefanya uamuzi wa kuvifuta viwanja 12,000," alisema Zambi.

Zambi alisema maeneo mengi Idara ya Ardhi imegeuka kuwa ni chanzo kikubwa cha migogoro katika maeneo mbalimbali kutokana na kile alichokiita kuwa ni lengo la kujinufaisha, ikiwamo kujilimbikizia viwanja.

Aidha, Zambi ameupa miezi sita uongozi wa wilaya hiyo kuanza upya mchakato mzima wa upimaji viwanja, huku akiagiza wale waliokuwa wameshalipia wapewe viwanja vyao bila ya usumbufu wowote.

Zambi alisema Idara ya Ardhi imegeuka kuwa chaanzo cha migogoro kutokana na kugawa viwanja bila ya utaratibu, huku watumishi walio wengi wakijilimbikizia idadi kubwa ya viwanja.

"Kinachosikitisha zaidi vipo viwanja 12,000 vimepimwa bila utaratibu, lakini wizara husika haivitambui, isipokuwa ni 1,724 tu," alisema Zambi.

Kwa upande wa watumishi walimhakikishia Zambi kuwa watajitahidi kufuata maadili na maagizo yanayotolewa na viongozi wa ngazi zote.

# TGNP kutafakari maazimio ya Beijing

**Na Yasmine Protace**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP Mtandao), umesema kwa mwaka 2020 umejikita katika kutafakari safari ya miaka 25 ya maazimio ya Mkutano wa Nne wa Dunia wa wanawake uliofanyika Beijing, China mwaka 1995, kwa kuangalia mafanikio yaliyofikiwa.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, katika maadhimisho ya Siku ya Wanamke Duniani, ambapo pia yaliangazia miaka 25 ya Beijing.

Katika maadhimisho hayo ambayo yaliandaliwa na TGNP Mtandao kwa kushirikiana na vituo vya taarifa na maarifa vya Wilaya ya Ubungo, jijini Dar es Salaam.

Liundi aliwataka wazazi wasimamie malezi ya watoto wao ambayo ndio yatakuwa mkombozi katika maisha yao.

"Wazazi tuhakikishe tunasimamia malezi ya watoto, bila kufanya hivyo watoto wataharibikiwa kimaisha," alisema.

Akizungumzia kuanzishwa vituo vya Taarifa na Maarifa katika maeneo vilivyopo, alisema vituo hivyo vimesaidia kuelimisha jamii katika harakati za kiuchumi na kimaendeleo na vimekuwa vikifanya kazi kwa kushirikiana na viongozi wa serikali za mitaa.

"Wilaya ya Ubungo ina vituo 14 vya taarifa na maarifa na vituo hivyo vitaendelea kuleta hamasa katika maeneo yao," alisema.

Kuhusu Siku ya Wanawake Duniani, Liundi alisema kuwa zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania ambayo ni wanawake, wakipewa fursa, haki na wajibu sawa na wanaume, kasi ya maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii itakuwa kubwa.

Alisema wanawake wakipewa fursa sawa za kushiriki katika ngazi za maamuzi katika kutatua changamoto zinazokumba kundi hilo, changamoto ambazo zitatatuliwa zitakomboa jamii yote na kwamba kutakuwa na kasi ya maendeleo ya nchi.

Aliongeza kuwa mwaka ukiwa ni wa 25 tangu kufanyika kwa Mkutano wa Beijing, TGNP Mtandao imejikita katika kutafakari safari ya miaka 25 ya Beijing ambapo imejikita kuangalia mafanikio yaliyofikiwa.

Alisema wataangalia fursa zilizopo na mikakati ya kuendeleza harakati za kuleta usawa wa kijinsia baada ya miaka 25.

Aliongeza kuwa mijadala ya maadhimisho imejielekeza maeneo manne kati ya 12 ya vipaumbele.

Alitaja maeneo hayo ni ukatili wa kijinsia, mtoto wa kike, ushiriki wa wanawake katika uongozi na uwezeshwaji kiuchumi.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela (katikati), akizungumza na walimu wa shule ya sekondari Mwanza juzi, baada ya kukagua ujenzi wa bweni la wasichana iliyokuwa ahadi ya Rais John Magufuli aliyoitoa jijini humo, Julai 17 mwaka jana. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Wenye changamoto ya akili waomba mtaala maalumu

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya kutetea watu wenye changamoto ya akili (Pearl of People with Down Syndrome Foundation), imeomba serikali kuandaa mtaala maalum wa elimu ambao utakuwa rafiki kwa kundi hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mwanzilishi wa Taasisi hiyo, Mony Pettit, alisema mtaala wa elimu uliopo sasa bado hauwapi fursa watu wenye changamoto ya akili kupata haki ya elimu na kufikia ndoto zao kama ilivyo kwa makundi mengine.

Alisema kutokana na changamoto ya kiakili kwa kundi hilo, halipaswi kuwekwa katika kundi la elimu jumuishi kwa sababu hali yao ya uelewa haiendani na watu wa kawaida wasio na tatizo lolote au kundi la wenye ulemavu mwingine tofauti na huo.

"Kuna aina nyingi za watu wenye ulemavu, kundi hili la watu wenye changamoto ya akili, mtaala wao wa elimu unatakiwa usiwekwe kama watu wengine wasio na ulemavu au wenye ulemavu mwingine tofauti na huo kwa sababu uelewa wa kundi hili huwa ni wa taratibu sana na wakati mwingine unategemea vitendo au stadi za kazi zaidi," alisema Pettit na kuongeza:

"Kuna wakati mtu wa hali hii anakuwa hayuko tayari kufanya jambo lolote ambalo watu wengine wenye ulemavu wanafanya kwa wakati huo.

"Ni mtu ambaye anaelewa zaidi kujifunza kupitia stadi za kazi zaidi kuliko njia nyingine, kwa hiyo kunapokosekana mtaala wao maalum wa elimu, moja kwa moja kundi hili tunakuwa tumelisahau katika sekta hiyo muhimu katika maisha."

"Serikali inatakiwa iangalie ni namna gani ya kuhakikisha hawa nao wanapata elimu kwa kuweka mtaala ambao baada ya kumaliza utawasaidia angalau nao wapate hata kazi za kufanya."

## Mradi wanufaisha wajawazito, watoto

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WILAYA za Misungwi na Kwimba mkoani Mwanza zimenufaika na Mradi wa Mama na Mtoto uliolenga kupunguza vifo vya kina mama wajawazito, watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka mitano.

Zaidi ya watoa huduma 6,000 wamejengewa uwezo kupitia mradi huo ulitekelezwa katika wilaya hizo ambao washirika wake ni Chuo Kikuu cha Calgary nchini Canada, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbarara (Uganda), Chuo Kikuu cha Katoliki cha Sayansi ya Afya (CUHAS) Bugando, Shirika la Agriteam Health Tanzania, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba na Misungwi, uliofadhiliwa na Serikali ya Canada ulioanza 2016-2020.

Akizungumza wakati akifungua mkutano wa kuangalia mafanikio na changamoto zilizokuwapo kwenye mradi huo ambao upo mwishoni uliofanyika jijini Mwanza, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema mradi umefanya kazi kubwa kwenye kuimarisha na kuboresha miundombinu ya kutolea huduma ya wajawazito, lakini vilevile na watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka mitano, wametoa magari ya wagonjwa, simu za mikononi kwa halmashauri hizo mbili ili utoaji wa taarifa uwe wa haraka hasa kwa maeneo ambayo hayawezi kufikika kwa haraka.

Pia ulijenga uwezo kwa watoa huduma zaidi ya 6,000 kwa wakati na mafunzo mbalimbali yaliyopelekea umahiri katika utoaji wa huduma.

Alisema, mradi huo umesaidia kupunguza vifo vya wajawazito, watoto wachanga na walio chini ya umri wa miaka mitano, hivyo aliwataka viongozi wa halmashauri hizo yale yaliyopatikana kwenye mradi yaendelezwe, na kutaka vifaa vitunzwe vizuri.

Kwa upande wake Makamu Mkuu wa CUHAS Bugando, Prof. Paschails Rugarabamu, alisema walitoa wataalamu upande wa afya ya kinamama na watoto ambao walishirikiana na wilaya za Misungwi na Kwimba katika mafunzo hasa elekezi kwa vitendo kwa ajili ya kuokoa maisha ya mama na mtoto, hivyo wamefaidika wao pia kuona kile kinachoendelea huko, ili iwasaidie kuboresha mitaala yao katika ufundishaji.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Upasuaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando, Dk. Fabian Massaga, alisema mradi umekuja na njia mbadala ya kusaidia mkoa kwani hospitali hiyo inahudumia mikoa minane kwa kufanyika katika wilaya hizo na kuwapa mafunzo na vifaa ni maboresho makubwa ya kupunguza vifo vya watoto na kinamama.

Mratibu wa Huduma za Afya ya Jamii kutoka Wilaya ya Kwimba, Luciana Tito, alipongeza mradi huo uliofadhiliwa na serikali za Canada wa mama na mtoto kwa kutoa mafunzo kwa watoa huduma 879 kwenye wilaya hiyo kwani wizara ina utaratibu wa kuleta watoa huduma wawili kwa kila kijiji, ambao pia umeleta mafanikio kwa kupunguza watoto wenye utapiamlo na wengine wamegundulika na kupatiwa matibabu.

## Takukuru yasaka ushahidi wanawake rushwa ngono

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) imewataka wanawake wilayani Longido mkoani Arusha, kutoa taarifa za matukio ya rushwa ya ngono yanapowakabili katika majukumu ya kikazi na maeneo mengine.

Mwakilishi wa taasisi hiyo wilayani humo, Mwinamila Mpela, alisema juzi kuwa rushwa ya ngono ni tatizo katika sehemu mbalimbali na waathirika wakubwa ni wanawake.

"Wanawake wengi wanakabiliwa na tatizo hili kwenye maeneo ya ajira na sehemu za kutafutia huduma mbalimbali za kijamii," alisema.

Aliongeza kuwa ni kosa kisheria kutoa au kuomba rushwa ya ngono kwa lengo la mtu kufanikisha jambo lake na tayari kosa hilo limeingizwa kwenye Sheria ya Uhujumu Uchumi.

"Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa inatamka matumizi mabaya ya nafasi au madaraka katika kupendelea kutoa haki kwa kuomba rushwa ya ngono, tunafanya kazi chini ya usimamizi wa sheria, hivyo rushwa ya ngono ni kosa kisheria," alionya.

Alisema kuwapo kwa matukio hayo kunatokana na mmomonyoko wa maadili kwa viongozi au ofisi unayoenda kuomba msaada, tamaa ya kimwili inayopelekea kumnyima haki mlengwa hadi atakapotoa rushwa ya ngono, kutojiamini kwa wanawake kwa kukosa sifa za ajira na kuhitaji kujihakikishia huduma kwa haraka.

"Rushwa hii ya ngono ipo, lakini hakuna viongozi wanaume wanaotoa taarifa kama kuna wanawake wanaenda ofisini kwao na kuwashawishi kufanya nao mapenzi," alisema.

Alisema waathirika wakubwa wa rushwa hiyo ni wanafunzi shuleni na vyuoni, na taasisi hiyo imepokea taarifa kutoka maeneo mbalimbali ya nchi na wameanza kuyafanyia kazi.

Aliwataka wanafunzi kutoa taarifa kwa kuwa ofisi hiyo hufanya kazi kwa siri na watawashughulikia wanaotumia madaraka yao vibaya.

Alisema hata watumishi wa ngazi za chini wakati wa ajira, kupandishwa vyeo na hata zinapotokea nafasi za kuhudhuria semina, huwa wanaombwa rushwa ya ngono ili watimiziwe mahitaji yao.

"Maofisa elimu nao wamekuwa wakiwanyanyasa walimu kipindi cha kuwasainia barua zao za kikazi na hata wanapoomba uhamisho, maofisa elimu wa kiume wanawaomba rushwa ya ngono ili kuwafanikishia matakwa yao," alisema.

Mwakilishi huyo wa Takukuru alisema kutoa au kuomba rushwa ya ngono ni ukiukwaji wa haki za binadamu kwa kupindishwa na kucheleweshewa haki pamoja na ukiukwaji wa utawala wa sheria na taratibu za kazi kwa kuajiri watu wasiokuwa na sifa kutokana na rushwa ya ngono.

"Faida ya kukataa rushwa hii ni kulinda heshima yako na utu," alisema.

# Wazuia msafara wa RC kisa huduma za afya

**Na Cynthia Mwilolezi, NGORONGORO**

WANANCHI wa Kijiji cha Tinaga, Kata ya Kirangi wilayani Ngorongoro mkoani Arusha, wamelazimika kusimamisha msafara wa Mkuu wa Mkoa huo, Mrisho Gambo, kutokana na adha ya kukosa huduma za afya.

Msafara huo ulisimamishwa jana wakati ukielekea Kata ya Samunge, ikiwa ni siku ya pili ya ziara ya kiongozi huyo kusikiliza kero za wananchi na kukagua miradi ya maendeleo wilayani humo.

Mmoja wa wananchi hao, Elina Dominic, alisema wanawake wanapata adha kubwa ya kukosa mahali salama pa kujifungulia kutokana na kijiji chao kutokuwa na zahanati.

"Kutokana na kero hii ya kukosa huduma za afya, wananchi tulianza ujenzi mwaka 2016 ambao upo hatua ya kupaua, lakini mpaka sasa hakuna mchango wowote wa serikali wa kuhakikisha tunapata huduma bora za afya," alilalamika.

Neema Kazimoto, mkazi mwingine wa kijiji hicho, alisema wanawake wajawazito wanalazimika kupanda bodaboda umbali wa zaidi ya Km 30 kwenda Waso ili kupata huduma ya kujifungua, jambo ambalo si salama na baadhi yao wamekuwa wakijifungulia nyumbani, kwa wakunga wa jadi na kuwanyima watoto haki ya kupata chanjo.

Baada ya maelezo hayo, Gambo alimhoji Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ngorongoro, Mathew Siloma, mipango waliyonayo kukamilisha ujenzi wa zahanati ya kijiji.

"Sasa mwenyekiti wenu ameniahidi halmashauri italeta Sh. milioni 20 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huu, hivyo msiwe na wasiwasi," aliahidi.

Gambo alisema wananchi hao wameonyesha uzalendo wa dhati wa kuunga mkono Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika sekta ya afya na kwamba kuna kila sababu kwa serikali kuhakikisha jengo hilo linakamilika mara moja, ili wananchi wapate huduma bora za afya.

Kuhusu umeme wa REA ambao mkandarasi ameshaanza kuchimba mashimo kwa ajili ya nguzo, Gambo alimtaka Meneja wa Shirika la Umeme (Tanesco) Wilaya ya Ngorongoro, Dominic Said, kuhakikisha wananchi wanapata umeme kabla ya Agosti mwaka huu, ikiwa ni pamoja na zahanati hiyo.

Alisema Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi ya Teknolojia ambaye ni Mbunge wa Jimbo hilo, William Ole Nasha, aliahidi kutoa Sh. milioni nane, kwa ajili ya kupaua jengo hilo na wiki iliyopita alitoa Sh. milioni nne.

Wengine walioahidi kusaidia ujenzi wa zahanati hiyo ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Arusha, Catherine Magige, aliyeahidi kutoa mabati 20 ili kumuunga mkono Ole Nasha na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi, Ally Karanjai aliyeahidi kutoa mifuko 20 ya saruji.



Mchungaji wa kanisa la Pentekoste Arusha, Mwalimu Onesmo Nnko (kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, mashine ya kusafishia njia ya hewa kwa watoto wachanga (sunction machine), ikiwa ni sehemu ya msaada wa vifaa tiba mbalimbali alivyovitoa kwa Kituo cha Afya USA River, katika Halmashauri ya Meru, wilayani Arumeru mkoani, Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Nyama ya pofu yamweka matatani

**Na Mwandishi Wetu, KITETO**

KIKOSI cha Kupambana na Ujangili (KDU) Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara kwa kushirikiana na askari wa Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori (WMA) ya Makame wilayani humo, kimemkamata Masudi Mussa (33) akidaiwa kukutwa na nyama ya pofu wanne.

Akizungumza na Nipashe juzi, Ofisa Wanyamapori Wilaya ya Kiteto, Doris Gama, alisema mtuhumiwa huyo alikuwa akisakwa kwa muda mrefu kutokana na kudaiwa kuhusika na matukio kadhaa ya ujangili.

Gama alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa kwa ushirikiano wa KDU, askari wa Makame WMA na askari wa kupambana na ujangili wa Taasisi ya Honeyguide.

"Kikosi cha doria wamemkamata na gobore moja, pikipiki mbili, risasi sita na visu vinne," alisema.

Meneja wa Makame WMA, Supuk ole Makao, alisema kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo wa ujangili, ni matokeo ya ushirikiano baina ya KDU, WMA na Honeyguide.

"Sisi kama WMA tumekuwa tukipata msaada mkubwa kutoka taasisi za uhifadhi kama Honeyguide, wametupa magari, wanalipia askari wetu wa ulinzi 27, wametupa pikipiki za doria," alisema.

# Wananchi waamua kufungua barabara isiyopitika

Na Godfrey Mushi, SAME

WANANCHI zaidi ya 500 wa Kata za Vumari na Mgagao katika Wilaya ya Same na wananchi wa kijiji jirani cha Pangaro kilichopo Wilaya ya Mwanga mkoani Kilimanjaro, jana waliamua kuingia kazini kwa saa 48 kwa ajili ya kufungua wenyewe barabara iliyokuwa imezuia shughuli za usafirishaji kuendelea.

Barabara hiyo kwa muda mrefu haipitiki kirahisi na baadhi ya maeneo vifusi vya udongo na mawe vilifunga mawasiliano ya barabara inayounganisha miji hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, akizungumza na wananchi wa maeneo hayo jana, alipongeza hatua hiyo ya kutosubiri ukarabati ambao ungefanywa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura).

"Uamuzi wenu huu umenishangaza sana na nimefurahi sana kwa kweli kwamba mmeungana kwa kazi ya kufungua barabara, kati ya kata hizi tatu ili kuimarisha usafiri wa barabara, nawapongeza. Ninawahakikishia nyie wananchi wangu kwamba barabara hii itaingizwa kwenye mtandao wa barabara za Tarura ili wao waendelee kuitunza kwa pamoja."

Meneja wa Tarura, Mhandisi Felician Msangi, akiwa katika eneo hilo alilazimika kushirikiana na wananchi katika kazi hiyo, huku akiwapongeza kwa kujua umuhimu wa barabara hiyo na kuanza kuifungua.

Nao baadhi ya wananchi walioshiriki kazi hiyo, Amon Aron na Victor Mshana walisema kufunguliwa kwa barabara hiyo kutarahisisha usafirishaji wa mazao na huduma za jamii, kwa kuwa miaka ya nyuma ilikuwa ikipitika, lakini haikuwa ikifanyiwa matengenezo ya mara kwa mara.

Wilaya hiyo ina eneo la ukubwa wa asilimia 40 ya mkoa wa Kilimanjaro inapata mgao kidogo wa fedha za mfuko wa barabara kuliko wilaya zote sita.

Hali ya ubora wa barabara katika Wilaya ya Same kwa asilimia 20 ni nzuri, asilimia 30 ni ya wastani na asilimia 50 ni mbaya zaidi.

**"Uamuzi wenu huu umenishangaza sana na nimefurahi sana kwa kweli kwamba mmeungana kwa kazi ya kufungua barabara, kati ya kata hizi tatu ili kuimarisha usafiri wa barabara, nawapongeza. Ninawahakikishia nyie wananchi wangu kwamba barabara hii itaingizwa kwenye mtandao wa barabara za Tarura ili wao waendelee kuitunza kwa pamoja."**

# Baba ashtakiwa madai ya 'kumtomasa' mwanawe

Na Mwandishi Wetu, SIHA

BABA mzazi wa binti wa miaka sita, mkazi wa Kijiji cha Lawate, Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Juma Mndeme (38), amefikishwa katika mahakama ya wilaya hiyo akikabiliwa na mashtaka mawili likiwamo la 'kumtomasa' sehemu za siri mwanawe.

Hati ya mashtaka iliyosomwa mahakamani hapo jana na Mwendesha Mashtaka wa Polisi, David Chishimba, ilidai kuwa Mndeme anashtakiwa kufanya shambulio la aibu dhidi ya mwanawe wa kumzaa.

Kesi hiyo ya ukatili wa kijinsia, inasikilizwa na Hakimu Mkazi wa wilaya hiyo, Petro Elibahati.

Akisoma mashtaka hayo, Chisimba aidai kuwa katika kosa la kwanza la shambulio la aibu ambalo ni kumshika mwanawe sehemu za siri, mshtakiwa huyo anadaiwa kutenda kosa hilo Machi 4, mwaka huu huko katika Kijiji cha Lawate, kinyume na kifungu cha 135 (1) na (2) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Kosa la pili anadaiwa kumjeruhi kwa mapanga mkono wa kushoto, Zuhura Hassan, ambaye ni mke wake kinyume na kifungu cha 225 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, sura ya 16 kama iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

"Mheshimwa, mshtakiwa anashtakiwa kwa makosa mawili ambalo la kwanza ni kumshika shehemu za siri binti yake wa kumzaa wa miaka sita.

"Kosa la pili ni kumjeruhi kwa mapanga mkono wa kushoto Zuhura Hassan ambaye ni mke wake, kinyume na kifungu cha 225 cha sheria hiyo."

Akisoma maelezo ya kosa, mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Machi 4, 2020.

Mwendesha mashtaka huyo alidai katika kosa la pili, mshtakiwa alitenda kosa hilo Machi 5, mwaka huu, baada ya kuzuka ugomvi kati ya wazazi hao wawili.

Baada ya maelezo hayo ya kosa kusomwa mahakamani hapo, mshtakiwa huyo alikana mashtaka hayo na Hakimu Mkazi Elibahati aliahirisha kesi hiyo hadi Machi 24, mwaka huu na kuamuru mshtakiwa kupelekwa Gereza Kuu la Karanga Mjini Moshi, baada ya kushindwa kukidhi masharti ya dhamana.



Mkuu wa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule, akizungumza jana na wananchi wa vijiji vitatu vya Pangaro, Vumari na Mgagao kuhusu umuhimu wa kujitolea kutengeneza barabara inayounganisha maeneo hayo. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Diwani aibuka na mapya mwanafunzi kutupa mtoto

Na Mwandishi Wetu, MOSHI

SIKU mbili baada ya mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya Somsom, kujifungua mtoto na kisha kumtupa chooni, mapya yameibuka kwa Diwani wa Kata ya Kibosho Magharibi (CCM), Deo Mushi, kudai kuwa uhusiano mbovu kati ya uongozi wa kata na shule hiyo yanaweza kuongeza tatizo zaidi.

Akizungumza na Nipashe baada ya tukio hilo, alisema anaona tatizo la mimba shuleni hapo linachangiwa na uhusiano mbovu wa viongozi na kwamba kuna haja ya serikali kutafuta ufumbuzi.

"Nasisitiza kuwa kumekuwapo na uhusiano mbaya kati ya uongozi wa shule na Ofisi ya Mtendaji wa Kata na bodi ya shule, nayo haitoi ushirikiano mzuri katika kuendesha shughuli za pamoja za hapo shuleni ikiwamo kusimamia nidhamu pamoja na mahitaji ya wanafunzi.

"Jitihada za Mtendaji wa Kata (Elisha Moses) kuiweka shule kwenye msimamo wa kiserikali zimekuwa zikigonga mwamba. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selamani Jafo, alishatoa maagizo kuwa walimu wakuu waliodumu miaka mitano shule moja wahamishwe maana kuna kuishi kwa mazoea.

"Ni muhimu sasa bodi ya shule ikatafakari umuhimu wa wazazi tuanze kusaidiana kulea watoto pamoja na ombi letu la kujenga hosteli ya wasichana ndiyo inahitaji kuwekewa mkazo kwa sasa."

Mwanafunzi huyo alijifungua salama bila usaidizi wa muuguzi wala mkunga, saa 3:20 asubuhi juzi akiwa nyumbani kwao, Kitongoji cha Mandeyeni, Kijiji cha Kifuni.

Tukio hilo limeacha utata kuhusu namna alivyokaa na ujauzito akiwa shuleni bila kugundulika na walimu wala wazazi.

Juzi, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kibosho Magharibi (WEO), Elisha Moses alithibitisha mwanafunzi huyo kujifungua mtoto na kisha kumtupa chooni.

"Baada ya kupata taarifa, nilifanya follow up (ufuatiliaji) kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kifuni, Felician Ollomi na Mratibu wa Elimu wa Kata yetu (Edes Paul) na wakanihakikishia ni kweli mwanafunzi huyo aligunduliwa na mjomba wake Faustine Massawe, akiwa anatoka chooni na alipombana aligundua kuna mtoto katupwa chooni, ndipo alipotoa taarifa na wananchi wakafika na kuvunja choo hicho.

Tukio hilo limetokea zikiwa zimepita siku tisa, tangu wanaharakati wanawake wa Moshi Vijijini waliojengewa uwezo na mradi wa nguvu ya pamoja ya kupambana na ukatili wa kijinsia unaoendeshwa na Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange and Community Organization (Kwieco) kwa ufadhiliwa na Women Tanzania Fund (WFT) kuitisha mkutano wa hadhara na wananchi wa kata hiyo.

Mwanafunzi huyo na mwanawe kwa sasa wako katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, kwa ajili ya uchunguzi zaidi wa kitabibu.

Juni 23, mwaka jana, Rais Dk. John Magufuli, alisema hakuna mwanafunzi yeyote wa kike wa shule ya msingi au sekondari atakayepata ujauzito kisha kuruhusiwa kuendelea na masomo, baada ya kujifungua katika uongozi wake.



Ukurasa 15

Kibiti waapizana kila 'shilingi' yao isipotee



Ukurasa 14

Saudia 'inapowakomoa' mahasimu Iran kwa kuporomosha bei ya petroli sokoni

# BUFE

IJUMAA MACHI 13, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 18

## Wachangishana kujenga kituo polisi kukabili ujambazi sugu kila mavuno



# Mrajisi Ushirika: Kanda Ziwa yaanza kwa choroko, dengu, jamii mikunde

**Na Anthony Gervas,** Mwanza

***WIKI iliyopita kulikuwapo makala iliyohusu Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza (Nyanza Co-operative Union Limited 1984 (NCU), iliyojadili safari yake na inavyojipanga kiuchumi inakoelekea kwa matumaini mapya. Wiki hiyo, pia ushirika wa Nyanza, ulikuwa mwenyeji wa MkutanoTume ya Ushirika Tanzania***

KATIKA uzinduzi huo, wadau na watendaji muhimu kutoka Mkoa wa Mwanza walihudhuria kwa ajili ya kujifunza namna ya utumiaji wa mfumo mpya wa stakabadhi mazao ghalani, utakaowawezesha wakulima kujikwamua kiuchumi kupitia mazao ya choroko na dengu.

Mazao mengine yatakayozalishwa na wakulima na kuwanufaisha chini ya usimamizi wa ushirika

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Tuna mifugo mingi kupindukia, ila uchumi wake unachechemea Ukurasa 19

BIASHARA

# Saudia 'inapowakomoa' mahasimu Iran kwa kuporomosha bei ya petroli

• Watumiaji wanufaika mafahari 'wanapogombana'



Baadhi ya visima vya nchini Saudi Arabia. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

WAKATI uhitaji wa mafuta katika uchumi wa dunia ukilega kutokana na kupungua safari za ndege na nyinginezo baada ya wimbi la homa ya corona kuanza, kuna eneo jingine la kuporomoka bei limeibuka.

Ni jinsi mawaziri wa mafuta wa nchi wanachama wa umoja wa wauza mafuta dunianii (OPEC) walivyoshindwa kukubaliana kiwango cha kupunguza uzalishaji wa mafuta na kiwango kinacholengwa cha bei. Mawaziri wakasambaa, vita ikaanza.

Vita ya bei ya mafuta kwa jadi ilikuwa ni vita ya nchi za uchumi wa kati zilizoko katika umoja huo na nchi kubwa duniani zikiwa katika viunga vyake, iwe ni kwa kujipangia bei za mafuta na sera kuhusu uzalishaji, na siyo kuingia mkutanoni.

Kwa njia hiyo, Russia kwa jadi siyo mwanachama wa OPEC ila katika miaka ya karibunii imeona isiwe mwangalizi tu katika mikutano yake ila mshiriki. Sasa pia inaelekea Russia inachukua mstari wa mbele wa kupigania bei kupungua, kinyume cha mshirika wake wa jadi siasa za ukanda wa Kaskazini Mashariki ya Kati, Iran.

Nchi ambayo kwa jadi imekuwa ikishikilia kupungua kwa bei ya mafuta hasa ni Saudia, ina kiwango kikubwa cha mafuta na idadi ndogo kiasi ya wakazi, hivyo ina uwezo wa kupunguza bei bila kuathiri matazamo yake kiuchumi.

Nchi nyingine kama Iran zina mazingira tofauti kiuchumi, na inaelekea itapata taabu kutokana na bei ya mafuta kuvurugika kabisa, wakati hata mauzo yake tayari yamewekewa vikwazo maeneo mengi duniani.

Russia ndiyo kwa jumla ilikuwa mfaidika mkubwa Iran kushindwa kuuza mafuta yake, kwa shinikizo la Marekani.

> **Hali hii inayojitokeza katika bei za mafuta soko la dunia itaonekana katika maeneo mengine kulingana na jinsi wimbi la corona linayoendelea.**



Gari la kuchukua mafuta kutoka visima vya nchini Saudi Arabia.

Suala la msingi hapo ni kuwa, uchumi wa nchi hizo mbili, kuacha watazamaji wa pembeni kama Iran, uko katika hali mbaya na hawana njia ila kujaribu kupata kiasi kinachowezekana kutokana na mafuta.

Ina maana, kulikuwapo haja ya kutoa punguzo kubwa la bei ili nchi ziendelee kununua mafuta kwa wingi huku wimbi la homa ya corona likiendelea, na kupunguza shughuli za sekta tofauti, hasa usafiri wa anga.

Katika nchi kadhaa Ulaya, Mashariki ya Kati na Asia mikusanyiko ya watu imezuiliwa, wakati nchini Marekani ni serikali majimboni ambazo zimekuwa zikichukua hatua, na Baraza la Wawakilishi kuisukuma Ikulu kupanga upya Bajeti.

Ina maana kuwa, matumizi ya usafiri binafsi yamepungua kwa kiasi kikubwa maeneo mengi, huku shughuli za biashara zikikwamishwa kwa upungufu wa safari kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Hata ingekuwa inawezekana kuagiza bidhaa kwa mfano kutoka China kwenda kwingine, inategemea bidhaa hiyo inavyoweza kukumbwa na vizuizi vilivyopo China kwenyewe.

Si China tu, kwani viwanda vingi vinategemea mali ghafi kutoka eneo moja kwenda kwingine na bila sehemu ya kinachozalishwa kuuzwa na kulipiwa, mzunguko wa uzalishaji unaathirika pia.

Nchi tofauti zinaangalia athari za wimbi la homa ya corona kulingana na ukaribu wake na China, bidhaa zake au wasafiri kwa jumla.

Kwa mfano sekta ya afya nchini Marekani imeathirika kutokana na mikwamo ya viwanda India ambavyo ni muhimu kukamilisha mzunguko wa utengenezaji wa malighafi au bidhaa kamilii katika sekta hiyo kwa ushirikiano na




Meli mpya ya kubena mafuta, Mt. Ukombozi, ilipokuwa katika bandari ya Zanzibar, baada ya kuwasili kutoka nchini China ilkoundwa. **PICHA: MTANDAO.**

kampuni za Marekani.

Maeneo kama mahoteli ndiyo yanatitia, au meli za safari za starehe ambazo zilikwama baharini na corona.

Hali hii inayojitokeza katika bei za mafuta soko la dunia itaonekana katika maeneo mengine kulingana na jinsi wimbi la corona linayoendelea.

Hivyo nchi zilizoko katika ushindani na hasa kampuni tofauti ndani ya nchi zitajitahidi kupunguza bei kupata soko la wale ambao bado wana mazingira ya kuhitaji bidhaa au huduma zao.

Bado hali hiyo haijafika Afrika, lakini kwingineko tayari ununuzi wa bidhaa nyingi umedumaa, kwani hata wale wanaoweza kufika kwa miguu wanaogopa kupata corona dukani.

Kupungua bei ya mafuta kunatazamiwa kusaidiai kiasi fulani uchumi wa nchi zinazotegemea mafuta kutoka nje, lakini tabu kubwa zaidi hasa katika nchi za Afrika ni kuporomoka kwa utalii, ambao kwa mfano hapa nchini nitegemeo kubwa la kuingia fedha za kigeni.

Hali hiyo inainua sintofahamu ya kina hasa katika kipindi cha kuandaa Bajeti ya mwaka ujao wa fedha, ambayo bado inaweza kufikishwa bungeni katika hali iliyopo.

Ni mazingira ambayo homa ya corona bado haijaingia Afrika kwa nguvu, na baadhi wameanza kuamini kuwa labda Waafrika wana kinga fulani dhidi ya homa hiyo, kwani maambukizi ya mgeni huyu yule - na katika tukio moja au mawili inasemekana huambukizwa au muathirika alikufa, lakini hapakuwa na maabukizi yoyote mapana yaliyofuata.

> **Hata ingekuwa inawezekana kuagiza bidhaa kwa mfano kutoka China kwenda kwingine, inategemea bidhaa hiyo inavyoweza kukumbwa na vizuizi vilivyopo China kwenyewe.**

Ikibaki hivyo, itakuwa ni muujiza wa dunia, lakini athari za kiuchumi bado zitaendelea kuwapo kwani bidhaa nyingi zinazouzwa nje zitakuwa hazihitajiki kwani shughuli za kufanya nje ya maskani zinapungua katika nchi tofauti.

Licha ya kuwa Russia na Saudia ndiyo ziko vitani, athari ya kujaza soko mafuta inaumiza wengi, hata wauzaji Marekani.

Saudia inaelekea ndiyo iliyoingia katika vita hiyo kwa nguvu zaidi, ikatangaza mipango ya kuleta Bajeti mpya kwa Baraza la Uwakilishi nchini humo kwa msingi kuwa bei ya mafuta itakuwa dola 12 kwa pipa badala ya dola 20 ambao ndiyo ulikuwa msingi wa makisio ya awali.

Halafu itaongeza uzalishaji wa mafuta hadi mapipa milioni 12.3 kwa siku, kiwango ambacho wachunguzi wa habari wanasema hakikuwahi kufikiwa awali. Ni kiasi cha mapipa 300,000 ya ziada ukilinganisha na kiwango cha juu kuzalisha mafuta kilichokuwa kinaonekana kama endelevu awali.

Vita hii ya mafuta ndani ya wimbi la corona na hitaji la ziada la kupata fedha za kigeni, ni sehemu ya siasa tatanishi za mataifa makubwa ya Mashariki ya Kati.

Tayari Russia kwa jumla inaonekana kuwa na nafasi zaidi katika ukanda huo na siyo kuamua masuala makubwa mengine duniani, nje ya ukanda wake wa Ulaya 'inakozikoromea' nchi kama Ukraine.

Saudia sasa imepania kulipa kisasi cha kuharibiwa medani yake ya uzalishaji na usafishaji mafuta kwa makombora ya Iran yaliyopigwa kutoka Irak; njia bora zaidi ni kujaza soko mafuta hadi Iran ifilisike.

# Marekani, Zimbabwe katika Vita siasa kupitia uchumi



Waandamanaji ,mjini Harare, Zimbabwe, wakipinga vikwazo vya kiuchumi vya Marekani dhidi ya nchi yao. **PICHA:DW**

WAZIRI wa Usalama, Owen Ncube na Balozi wa Zimbabwe nchini Tanzania, wawekewa vikwazo na Marekani, wakidaiwa kuwashambulia wapinzani wao

Waandamanaji mjini Harare, walipinga vikwazo vya kiuchumi vya Marekani dhidi ya Zimbabwe.

Marekani imewawekea vikwazo viongozi wawili wa Zimbabwe, kwa ukiukaji dai la kukiuka haki za binadamu.

Wizara ya Fedha ya Marekani, inaelezea kwamba viongozi hao walihusika na mashambulizi dhidi ya waandamanaji nchini humo.

Hatua hiyo imekuja wiki moja tu baada ya Marekani kuongeza vikwazo vya kiuchumi dhidi ya Zimbabwe kwa kipindi cha mwaka mmoja zaidi.

Taarifa ya wizara ya fedha ya Marekani imeeleza kuwa Waziri wa Usalama wa Zimbabwe, Owen Ncube, amewekwa katika orodha ya watu waliowekewa vikwazo na Marekani, akidai tuhuma za kuaamuru maofisa wa usalama wa nchi hiyo kuwavamia na kuwatesa wanachama wa upinzani.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, pia imemuwekea vikwazo Balozi wa Zimbabwe nchini Tanzania, ikimtuhumu kuongoza mashambulizi ya maofisa wa usalama dhidi ya wapinzani baada ya uchaguzi wa mwaka 2018.

Wakati huo wa tukio, Sanyantwe alikuwa akifanya kazi nchini Zimbabwe.

Kwenye taarifa yake, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, aliiambia serikali ya Zimbabwe 'ikomeshe haraka matumizi ya nguvu dhidi ya waandamanaji kwa njia ya amani, asasi za kiraia.

"Viongozi wa vyama vya wafanyakazi na wanachama wa upinzani nchini humo, na kuendesha uchunguzi na kuwafikisha mbele ya vyombo vya kisheria wale wanaokiuka haki za binadamu".

Watu sita wanatajwa kufariki katika tukio hilo na wengine kadhaa walijeruhiwa mwaka 2018, baada ya kuahirishwa kutangazwa matokeo ya uchaguzi, yaliyompa ushindi Rais Emmerson Mnangagwa.

Naibu waziri wa Fedha wa Marekani, Justin Muzinich, anasema viongozi wa kisiasa na wa kijeshi nchini Zimbabwe walitumia nguvu mara nyingi kuwanyamazisha wakosoaji na maandamano ya amani.

Vikwazo hivyo ni pamoja na kuzuia mali za viongozi hao wawili zilizoko nchini Marekani na vilevile kuzuia Wamarekani kutofanya nao shughuli zozote za kibiashara.

Mwaka 2019, Ncube na Sanyatwe, waliwekewa vikwazo vya kutozuru Marekani. Wiki iliyopita, Marekani iliongeza vikwazo dhidi ya Zimbabwe kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa kile ilichoeleza kuwa ni "mauaji na ubakaji unaofanywa na maofisa wa usalama."

Ni hatua iliyopokewa na serikali ya Zimbabwe, ikieleza tuhuma za Marekani hazina msingi.

Kwa takriban miaka 20 sasa, Marekani imeiwekea vikwazo Zimbabwe, wakiwamo maofisa wake wa kisiasa na kijeshi.

Rais wa sasa Emmerson Mnangagwa ni miongoni mwa viongozi waliowekewa vikwazo hivyo kwa tuhuma za kuwabana wapinzani.

Uhusiano baina ya Zimbabwe na Marekani umekuwa wa pandashuka toka utawala wa Robert Mugabe. Mwaka uliopita Zimbabwe ilimtuhumu Balozi wa Marekani nchini humo kuwa na tabia kama "mwanachama wa upinzani". **DW**

BIASHARA

# Mrajisi Ushirika: Kanda Ziwa yaanza kwa choroko, dengu, jamii mikunde



Naibu Mrajisi wa Vyama Vya Ushirika Tanzania, Charles Malunde, alipozungumza kwenye uzinduzi wa mnada wa zao la choroko, kwa Mfumo wa Mtandao ulioanzishwa, mkoani Shinyanga siku ya Jumatano, iliyopita. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

na Serikali ni soya, ufuta pamoja na mbaazi, ambayo serikali imeyapa kipaumbele kama yalivyo mazao mengine ya kimkakati.

Serikali ya sasa baada ya kuingia madarakani imehakikisha ushirika unafufuliwa kila kona ya nchi,na kuwashughulikia wale wote waliokuwa wamejimilikisha mali zake, ikizirejesha na kuwajali wakulima.

Wengi waliamini 'ushirika sasa ni kwa heri, bali kurejea tena ni majaliwa.' Lakini, hatua ya serikali 'imetenda miujiza' yake na kuwaondoa watendaji walioweka pabaya ushirika.

Naibu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini, Charles Malunde, ana darasa la kina hasa nini kilifanyika kuhusu vyama vya ushirika, wakulima, watendaji na wadau muhimu kuujua mfumo huo ulioenda sambamba na maendeleo ya kidigitali.

"Mfumo wa Stakabaadhi za Mazao Ghalani, utawawezesha wakulima wa choroko na dengu kuwaweka pamoja, kupitia vyama vya msingi vya ushirika vya mazao (Amcos) vitakavyokuwa vikikusanya mazao yao katika maghala na baadaye kuyapeleka kwenye ghala kuu la ushirika," anasema Naibu Mrajisi.

Anafafanua kuwa, mazao yatakusanywa kwa kuzingatia uzito na ubora, pia kukiwepo siku maalum ya kuuza kwa mnada na kila mkulima ataweka bei ya kuuza kwa kilo, kulingana na ubora uliopo.

> **"Lengo letu ni kujenga ushirika wa kuaminika na kuondoa udanganyifu wa bei ya mazao ya wakulima, hata wanunuzi watanunua katika maghala yetu kwa ushindani kulingana na bidhaa yenyewe ilivyo na ubora.**



Mfumo ulioendelea hivi sasa ni soko la bidhaa, kwamba ubora wa mazao utatanganzwa kwenye mtandao wa kijamii, wanunuzi watanunua kwa kuweka bei kwenye mtandao na kushindanishwa bei zao, mshindi ndiye atakayepata bidhaa hiyo.

"Tunatarajia kuanza kuuza mazao hayo kwa kutumia mfumo huu wa stakabaadhi ghalani kuanzia machi 10 mwaka huu, tutakuwa na mnada kwa yale yatakayokuwa tayari yamekusanywa,' anasema Malunde.



Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Soko la Bidhaa, Augustino Mbulumi, akionyesha matokeo ya mnada wa juzi. **Chini;** Sehemu ya choroko ikiwa kwenye magunia katika ghala la Kijiji cha Manigana Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

**MWENDESHA SOKO?**

Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na soko la bidhaa (tmx), ndizo itakayoendesha minada katika maghala ya choroko, dengu na mbaazi, kupitia soko la bidhaa katika maeneo husika.

Anasema kampuni zitakazonunua bidhaa, zitawajibika na ushuru wa halmashauri husika na gharama zitakazoainishwa na tume hiyo yenye dhamana ya kusimamia na kudhibiti masoko ya mazao kupitia vyama vya ushirika.

Naibu Mrajis Ushirika, anasema, serikali kupitia vyama vya ushirika, imesimama kidete kuhakikisha mazao ya wakulima yanapata thamani kubwa katika masoko, ili kuwainua kiuchumi ili waondokane na umaskini unaowakabili.

Ni hatia inayoelezwa itawasaidia wakulima kuondoa uuzaji mazao yao kiholela kwa walanguzi wakitumia "visado' badala ya mzani wa kilo, huku wengine wanauza shambani kwa kutofautiana bei, Mrajisi akitoa mfano wa bei kati ya Sh.500 hadi Sh.1000 wakati huo huo, mizani wanayotumia haijahakikiwa kwa wakala wa vipimo.

Malunde anasema, kinachotarajiwa sasa ni kuanza kuuza mazao ya wakulima kupitia mfumo huo waliouandaa wa ndani na baadaye watapata fursa za kufanya biashara kidigitali zaidi.

Anataja mikoa itakayouza choroko na dengu na kutumia mfumo huo wa sasa, ni Mwanza kupitia Wilaya zake za Magu, Misungwi na Kwimba, pia kuna Shinyanga ikiangukia wilaya zake za Kishapu na Shinyanga na mkoa Simiyu.

Inaelezwa, mfumo huo ulishaanza mkoani Ruvuma mwaka jana na kunakolimwa ufuta katika Wilaya ya Kondoa, ambako bei inaelezwa kupaa hadi Sh,1,200 kwa kilo.

**MANUFAA**

"Mfumo huo utasaidia halmashauri za wilaya zinazolima mazao yasiyokuwa ya kimkakati, kuongeza mapato yake, anasema Malunde na anaongeza:

"Hivyo, serikali itahakikisha Ushirika umesimama kuimarika, umefufuka na masoko ya wakulima yanapatikana, ili kuleta tija na mageuzi makubwa ya kiuchumi kwa wakulima wakiwemo wakulima wa pamba."

Anasema, mfumo huo wa stakabadhi za mazao ghalani ulianza kwa majaribio mwaka 1999 kwa wakulima wa pamba na wengine wa mazao ya kimkakati ambayo ni korosho, kahawa, michikichi na chai ulianza miaka mingi.

**WITO NI NINI?**

Malunde ana ufafanuzi kwamba, ili mfumo huo uwe endelevu, anahitaji watendaji wake na viongozi waliopewa dhamana kuwa waaminifu, badala ya kuwa wadanganyifu na kwamba bei ya pamba kwa ekari moja inatakiwa mkulima apate kuanzia wastani kilo moja iuzwe kati ya Sh. 800 hadi Sh.1000.

Naibu Mrajisi anasema, ni mfumo ukakaosaidia kuondoa umaskini na kuleta maendeleo, akileza kushangazwa Mkoa wa Mwanza kushika nafasi ya tano kwa umasIkini katika mikoa yote nchini, jambo linaloshangaza kutokana na Mkoa kuwa na rasilimali za kutosha, ikiwamo ardhi yenye rutuba.

**MWENYEKITI USHIRIKA**

Mwenyekiti wa Tume ya Ushirika Tanzania, Dk.Titus Kamani, anasema kuwa mfumo huo upo na umekubalika kitaifa, kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa bei bora ya wakulima wa mazao mchanganyiko, anayotaja kuwa ni choroko, dengu, soya, ufuta, mbaazi na kokoa.

Kwa mujibu wa Dk. Kamani, hii ni tofauti na mazao ya kimkakati kama vile korosho, pamba, kahawa, chai na tumbaku. Anafafanua:

"Lengo letu ni kujenga ushirika wa kuaminika na kuondoa udanganyifu wa bei ya mazao ya wakulima, hata wanunuzi watanunua katika maghala yetu kwa ushindani kulingana na bidhaa yenyewe ilivyo na ubora.

"Watashindanishwa, mnunuzi atakayetoa bei kubwa ndiye atapewa bidhaa na sasa tumeona Kanda ya Ziwa tuanze na mazao ya choroko na dengu," anaeleza Dk.Kamani.

Anasema, katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Lindi, Ruvuma, Mtwara na Pwani, tayari walishaanza kutumika na sasa takribani ni miaka mitatu mazao ya soya, mbaazi, ufuta na kokoa inayolimwa wilayani Kyela, mkoa Mbeya.

Wakulima watakaonufaika na mfumo ni pamoja na Mwanza, Simiyu, Shinyanga na anasema vyama vya msingi vya ushirika vya mazao(Amcos), vitafanya kazi ya ukusanyaji mazao na kuyaweka ghalani, chini ya usimamizi mkuu wa Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza (NCU), ili wanunuzi binafsi wanunua kupitia mfumo huo.

Inasifiwa, mfumo Stakabaadhi ya Mazao Ghalani, utasaidia kuwaunganisha wakulima moja kwa moja katika uuzaji mazao yao na kupata bei kubwa, ukidhibiti ulanguzi kutoka kwa wanunuzi binafsi wanaotumia mizani isiyokuwa na vipimo rasmi na sahihi.

Dk, Kamani anasema, kutokana na uelewa mdogo wa wakulima, wamekuwa wakiuza mazao yao kiholela kwa walanguzi, pasipo kutumia mizani, hivyo ni dhahiri wakulima wabadilike kiuchumi kupitia mifumo itakayowasaidia kimaendeleo.

***Makala hii inatokana na mkutano mkubwa wa Tume ya Ushirika Tanzania.***

# Biashara katika picha



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja, akitoa maelezo kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Dawasa, Jenerali Mstaafu Davis Mwamunyange, akiwa na wajumbe wa bodi walipokagua ujenzi wa jengo jipya la Dawasa, Ubungo, jijini Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**



Mkurugenzi wa Hazina na Masoko Benki ya NBC, Peter Nalitolela (kulia), amkabidhi cheti cha shukrani mmoja ya wastaafu wa benki hiyo, Emmanuel Mapunda, wakati wa hafla ya kuwaaga wastaafu wa benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mbunge wa Jimbo la Songwe, Phillip Mulugo (kushoto), akimshukuru Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye (kulia), kwa niaba ya wananchi wake, baada ya kuzindua mnara wa mawasiliano uliojengwa na TTCL, kwenye kijiji cha Maleza, mkoani Songwe, juzi. **PICHA: WUUM**

UCHUMI

# Wachangishana kujenga kituo polisi kukabili ujambazi sugu kila mavuno

• DC, mbunge waongoza 'kila ulicho nacho' • Mkakati Julai iwe tayari, majirani waiga • Polisi wameshaanza kwa kuishi 'gesti'



Naibu Waziri wa Ujenzi na Mbunge wa Ushetu, Elias Kwandikwa, aliyepiga na kushika kibuyu, akicheza ngoma ya asili baada ya kukabidhi bati 48 za kuezeka Kituo cha Polisi Ulowa. **PICHA: SHABAN NJIA.**

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

IMEKUWA mazoea, kero aina yake, hata kuchukua sura ya tatizo kamili katika kijiji na kata ya Ulowa, Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama. Kila inapofika kipindi cha mavuno ya kilo, basi ujue matatizo yaliyobeba sura ya ujambazi na wizi, yanachukua nafasi yake.

Ni mazingira yanayowafanya wananchi kusema 'sasa basi.' Ndicho walichoamua katika msimu wa mavuno uliopita, uvamizi wa kihalifu unaanza.

Walichoamua, wamechangishana fedha na kujenga kituo cha polisi cha kata, ili kukabiliana na wimbi la uvamizi wa uhalifu huo wa kila mara, unaojumuisha kuvunja maduka na kuibwa bidhaa zao usiku.

Ni uvamizi unaoendana na wakati wa mavuno ya mazao ya mpunga, pamba na tumbaku, wananchi wakikoseshwa amani na uhuru wa kuzalisha mali, kupitia kilimo chenye tija.

Awali uvamizi ulianza katika vijiji vya Mbika, Ubagwe cha Nonwe, katika kata ya Ulowa. Hali ilipofika pabaya, wananchi walichukua uamuzi mgumu wa kuchangishana na kujenga kituo cha afya, kwa ajili usalama wa wananchi na mali zao.

> **"Tunamshukuru sana mbunge wa jimbo letu, Elias Kwandikwa, hajatutupa kwa hili na amekuwa wakituunga mkono hasa pale tunapoanzisha jambo la maendeleo kwenye kata zetu....**

### WANANCHI WASIMULIA

Aloyce Jacob, ni mkazi wa kata ya Ulowa. Anasema walichukua hatua ya kuchangishana fedha na kujenga kituo hicho cha polisi, baada ya kukithiri matukio ya uvamizi nyakati za usiku kwenye makazi na maduka ya biashara.

Jacib anafafanua, ni matukio yanatokea wakati wa mavuno ya kilimo cha mazao ya mpunga, tumbaku na pamba. Wananchi waliingiwa na hofu, hata kusita kuendeleza kilimo cha biashara, walihofia uvamizi uliopo, baada ya mauzo ya mazao yao, ikizingatiwa kilimo ndicho ajira yao kuu.

"Uvamizi huu ulianza katika kata jirani za Mbika, Ubagwe kijiji cha Nongwe na baadae wakafika hapa kwetu Ulowa: anasimulia Jacob na kuongeza:

"Uvamizi huo, hufanyika katika nyakati za usiku na hasa wakati wa mavuno ya mpunga, tumbaku na pamba," anaeleza Jacob.

Pia, anasema mbali na uvamizi madukani nyakati za usiku, matukio mengine waliyavamia na kupora mali za wanakijiji barabarani, wanapotoka mjini Kahama kuuza bidhaa zao.

Diwani wa Viti Maalumu, Gabbriela Kimaro, anasema kujengwa kwa kituo cha polisi, kunatokana na kuandamwa na matukio mbalimbali ya wizi mbali na maduka, pia mifugo na safarini barabarani, hali kadhalika majumbani usiku

Gabbriela, anasema baada ya kuandamwa na matukio mbalimbali, waliamua kuitisha vikao na wananchi, wadau wa maendeleo na viongozi wa vyama vya msingi(Amcos) na kukakubaliana kuchangishana fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha polisi, mahali hapo. Anaeleza wananchi waliingiwa na hofu na kuchukua hatua ya kuomba askari watano kutoka Kituo cha Polisi Nyamilangano, waliofikia kwenye nyumba ya kukodi kama ua muda wakilipiwa na wananchi wa kata ya Ulowa mpaka sasa, kwa kushirikiana na mbunge wao.

Diwani huyo anaeleza, mchango ulifanyika kwa mtindo wa kila mmoja kutoa alichonacho, hadi kuanza ujenzi wa kituo hicho cha polisi, ambacho hadi sasa unaendelea.

"Tunamshukuru sana mbunge wa jimbo letu, Elias Kwandikwa, hajatutupa kwa hili na amekuwa wakituunga mkono hasa pale tunapoanzisha jambo la maendeleo kwenye kata zetu....polisi waliopo kwa sasa kwenye jengo tulilokodi wametuliza kabisa uvamizi uliokuwa ukifanyika.

"Sasa tunaendelea na ukamilishaji wa jengo letu la polisi, ili tusiendelee kuingia gharama za kulipa pango la ofisi na ifikapo mwezi wa saba mwaka huu, jengo letu litakuwa limekamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi," anaeleza Diwani Gabbriela, huku akisifu ushirkiano kutoka kwa mbunge na mkuu wa wilaya.

### MKUU WILAYA

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha anaanza kwa kuwapongeza wananchi wa Ulowa kwa kujenga kituo cha polisi, kupambana na uhalifu na anawataka wenzao wa kata jirani, kuiga mfano wa Ulowa, kujenga kituo cha polisi.

Macha anakumbusha, kwamba suala la ulinzi linaanza na wananchi na serikali inaongeza nguvu, kwa kuleta askari polisi kwenye eneo husika, hivyo anawaomba wananchi kujenga nyumba walau moja kwa ajili ya makazi ya askari hao, ili waishi jirani na kazini kwao.

Kingine, ni kwamba anawasisitiza wananchi wa kata hiyo ya Ulowa, kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa askari polisi na wa ziada watakaoongeza nguvu.

Mkuu wa Wilaya anasema, hata kata jirani ya Segese katika Halmashauri ya Msalala, awali haikuwa na kituo cha polisi, lakini sasa wamekutana kuchangishana fedha za kujenga kituo kama wenzao, lengo ni kuimarisha ulinzi wa jeshi hilo, kwa kushirikiana na walinzi wa jadi, sungusungu.

Hivyo, anawataka wakazi wa Ulowa, waendeleze wito aliyotoa kwa wenzao, kuhakikisha wanajenga nyumba walau moja au mbili kwa watumishi wa polisi, ili kurahisisha tatizo linapotokea, lishughulikiwae haraka.

### NAIBU WAZIRI

Elias Kwandikwa, ni mbunge wa Ushetu na Naibu Waziri wa Uenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, anawaondoa shaka wananchi, kwamba serikali imejipanga kuweka mazingira bora ya ulinzi katika halmashauri yote anayoiwakilisha, ili wananchi wake waendelee na uzalishaji mali kwa amani na utulivu.

"Tumepanga kuweka mazingira mazuri ya ulinzi kuanzia ngazi ya kitongoji, kijiji, kata hadi wilaya, Hakuna maendeleo yanayoweza kufanyika, kama hakuna amani," anasema na kuongeza: "Amani ni mtaji mkubwa wa maendeleo kwa nchi zilizoendelea duniani."

Katika mchango wake, Kwandikwa alikabidhi bandari nne za bati zenye bati 48 kwa ajili ya kuezeka kituo kipya cha polisi cha Ulowa, kilichojengwa kwa mchango wa vyama vya msingi na wadau wa maendeleo, kikitarajiwa kuanza kutumika Julai ijayo.

Anakumbusha, Ulowa ni kata katika Halmashauri ya Ushetu, yenye kasi kubwa ya maendeleo, hivyo inahitaji miundombinu bora na ya kutosha hasa katika ujenzi wa barabara, nishati ya umeme, pia maji safi na salama.

UCHUMI

KATIBU MKUU MIFUGO:

# Tuna mifugo mingi kupindukia, Ila uchumi wake unachechemea

**Na Moshi Lusonzo**



Baadhi ya wazalishaji wa chakula cha mifugo, wakimsikiliza Katibu Mkuu wa Wizara ya Uvuvi na Mifugo (Hayupo pichani) wakati wa mkutano wa wadau wa ufugaji wa kuku na nguruwe. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

HADI ilipofikia sasa, Tanzania inatajwa kuwa juu katika maendeleo ya ufugaji kuku na nguruwe, baada ya idadi ya mifugo hiyo kuongezeka na kufikia jumla milioni 80.

Takwimu zilizotolewa na Wizara ya Uvuvi na Mifugo, zinaonyesha idadi ya kuku wamefikia milioni 79.1 na nguruwe zaidi ya milioni 2.2, hadi mwishoni mwa wiki iliyopita.

Pamoja na kukua kwa kasi kwa sekta hiyo, wahusika wanasimamia dhamana ya eneo hilo la rasilimali, wanasema changamoto zinaongezeka kwa bei ya malisho kila kukicha inaongezeka maradufu, hata kuwakatisha tamaa wadau waliojiita katika eneo hilo la kusimamia rasilimali mifugo.

Hadi sasa, wafugaji wengi wanaelezwa kukata tamaa na wapo ambao tayari wameshindwa kuendelea na eneo hilo la rasilimali uchumi.

### SERIKALI YAGUTUKA

Serikali kwa kubaini uwepo wa tatizo hilo, imeamua kuwakutanisha wadau wa ufugaji kuku na nguruwe, kwa lengo la kuchambua na kutafuta ufumbuzi wa changamoto hiyo, pamoja na mengine yanayohusiana nayo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uvuvi na Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel, anasema tatizo la kupanda bei ya chakula cha mifugo, imekuwa moja ya vikwazo vya ukuaji wa sekta mifugo na uvuvi. Anarejea takwimu kwamba hadi kufika mwishoni mwa wiki iliyopita, bei ya mfuko mmoja wa chakula cha kuku na nguruwe, iko kati ya Sh. 64,000 hadi Sh. 70,000 kulingana na aina ya chakula na umri wa mifugo husika.

Katibu Mkuu anasema, kikao cha wadau kinachowakutanisha maofisa kutoka serikalini, watengezaji wa vyakula, wafugaji na walaji kitatoa mwanga wa njia gani ya kufuata, ili gharama ziwe za chini kwa maslahi ya pande zote.

Profesa Ole Gabriel, anasema ameshajaribu kukaa na baadhi ya wafugaji wadogo na wakubwa, kilio chao kikibaki zaidi kuwa ni kushindwa kumudu gharama ya chakula zinazopanda kila wakati.

KWANINI BEI JUU?

kuhusu wazalishaji wa chakula, Profesa Ole Gabriel, anaeleza kwamba kupanda bei, kunatokana na uhaba wa malighafi kama mahindi na maharage ya soya ambayo yanauzwa ghali na wakulima.

Anasema, hadi sasa serikali inasubiri uamuzi utakaofikiwa baada ya kutathmini mnyororo mzima wa thamani ya mifugo hiyo, kuanzia uzalishaji chakula, ufugaji hadi inapomfikia mlaji, ili kuwepo gharama zinazoleta tija kwa pande zote.

> **“Vijana wengi sasa wameamua kuingia katika ufugaji wa kuku na nguruwe, lakini unapowauliza changamoto zao watakuambia ni gharama kubwa ya chakula.**

“Serikali itaendelea kuwa pamoja na wadau wa ufugaji wa kuku na nguruwe. Kwa kupitia kikao chenu, suala la bei ya chakula litapatiwa ufumbuzi kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kunufaisha taifa kiuchumi,” anasema Profesa Ole Gabriel.

Katibu Mkuu huyo, anaeleza kwamba wajasiriamali wadogo na kati wanapaswa walindwe, kutokana na mitaji yao kuwa midogo na rahisi kupotea, kama changamoto zinazowakabili hazitatatuliwa.

“Vijana wengi sasa wameamua kuingia katika ufugaji wa kuku na nguruwe, lakini unapowauliza changamoto zao watakuambia ni gharama kubwa ya chakula. Hili ni lazima tulitazame upya kwa ajili ya kuwavutia wengine,” anasisitiza.



Ufugaji wa kuku unategemea uwepo wa chakula cha kutosha

### MWENYEKITI WAZALISHAJI

Mwenyekiti wa wazalishaji wa chakula cha kuku, Harro Bhagat, pamoja na kukiri kuwepo tatizo hilo, anasema si suala la kutupiana mpira kwani kinachotakiwa serikali na wazalishaji wa chakula kukaa pamoja kuangalia suala hilo kwa kina.

Anasema, biashara ya kuzalisha chakula cha mifugo kwa sasa inakabiliwa na ugumu wa kupata malighafi baada ya wakulima kupandisha bei ya mahindi na maharage ya soya.

Baghat anatoa mfano mwaka jana, mahindi waliyanunua kutoka kwa wakulima kwa bei ya Sh. 400 kwa kilo moja, lakini baada ya miezi michache iliongezeka kwa kasi na kufikia Sh. 900.

Anasema, sababu za wakulima kupandisha bei, inatokana na serikali kuruhusu mahindi kuuzwa katika nchi za Zimbabwe, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Sudan Kusini.

“Serikali inatakiwa kuangalia suala hili, ili tupate bei rafiki ya kununulia mahindi pamoja na kuturuhusu kuagiza nje maharage ya soya, kutokana na uzalishaji wake hapa nchini kuwa mdogo,” anasema Bhagat.

Aidha, anasema kikwazo kingine wanachokabiliana nacho ni mlolongo, mrefu wa kupata cheti cha ubora wa chakula kutoka TBS, jambo linalosababisha muda mrefu kupotea kabla ya kuanza uzalishaji.

Mwakilishi wa Wafugaji Nguruwe nchini, Doreen Maro, anasema pamoja na changamoto ya chakula, upande wao wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa machinjio ya kisasa, pia uhaba wa mbegu bora.

“Wafugaji tunapata shida kutafuta sehemu salama ya kuchinja mifugo yetu kutokana na machinjio kuwa duni na inayohatarisha usalama wa afya na kupunguza thamani ya bidhaa. Tunaomba serikali ituangalie kwa kutujengea machinjio yenye hadhi ili na sisi tupate faida,” anasema.

Hafidh Ally, aliyesimama kwa upande wa wafuga kuku, anaitaka serikali kuangalia kwa makini sekta hiyo inayoweza kuleta fedha za kigeni na kukuza uchumi wa nchi.

Wito wake, anandai wasaidiwe kutafuta masoko ya bidhaa zitokanayo na mifugo hiyo, pamoja na kusaidiwa pale inapotokea matatizo ambayo yanampa hasara mkulima.

UCHUMI

# Umeme Sola na maendelo katika kijiji kisichojua umeme miaka 45




Ofisa wa kampuni ya Ensol, akifafanua namna mtambo wa umeme unavyofanya kazi kijijini Mpale, wilayani Korogwe. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

**Na Beatrice Shayo**

KIJIJI cha Mpale kilichopo katika Wilaya Korogwe, mkoa Tanga kipo kwa takribani miaka 45, hakijawahi kuona mwanga usiku, changamoto hiyo wameeleza ni moja ya sababu iliyowafelisha watoto wao katika masomo na kuwa nyuma kiuchumi.

Wananchi wa kijiji hicho wanaeleza tangu mwaka 1972 hadi mwaka 2017 ndipo walipopatiwa ufadhili wa umeme wa jua, ikiwa ni mkombozi kwa watoto wao kusoma vizuri na kuachana na matumizi ya vibatari.

Mkazi wa kijiji hicho, Hassan Bendera, anasema wamekaa kwa muda mrefu bila ya umeme, mpaka walipokuja wafadhili wa kampuni ya Ensol na kuwapatia umeme jua mwaka 2017. Anasema umeme huo umewanufaisha kupata mwanga na watoto hao kujisomea vizuri usiku, ukilinganishwa na awali walipotumia kibatari.

"Ninashukuru kupata huu mwanga maana nilikuwa na nunua mafuta ya zaidi ya Sh 1000 kwa siku, maana nina vyumba vinne inanibidi vibatari niviweke mafuta na watoto wajisomee huyu mfadhili ametusaidia kwa sasa nimeachana na vibatari natumia huu umeme ambao naulipia kama vocha kwa mwezi Sh. 11,000," anasema.

Bendera anasema, faida nyingi waliyoipata mwanga huo umewasaidia kuongeza kipato kwani wanafanya biashara hadi saa nne usiku na kipindi cha nyuma ilikuwa mwisho ni saa 12 ya jioni.

Muhunge Mussa, ni mfanyabiashara wa duka, anasema matumizi ya nishati imewaongezea kipato kwa wafanyabiashara tofauti.

Anasema kuwa, jokofu dukani kwake imemuongezea mapato kwa siku anauza kati ya Sh. 70,000 hadi sh 80,000 ikilinganishwa na awali alikuwa anauza sh 40,000.

> **"Mazingira ya huku kutokana na hali ya hewa inatulazimu kuwasha taa hata kama ni mchana, hivyo imewasaidia wanafunzi kwa kiasi kikubwa kutokuwa katika giza**

"Huu umeme umenifanya niweke banda la kuonyesha televisheni kwa wananchi, kiingilio nimeweka Sh. 300 hadi 500 kwa baadhi ya michezo huku mpira kwa mtu ni Sh. 1000 kwa mechi moja," anasema.

### WATENDAJI KIJIJINI

Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi Mpale, Humphrey Mhina, anasema mwanga huo umewasaidia katika ufaulu wa wanafunzi, kuna walimu hujitolea kwa ajili ya kuwafundisha jioni na kutumia nishati hiyo.

"Mazingira ya huku kutokana na hali ya hewa inatulazimu kuwasha taa hata kama ni mchana, hivyo imewasaidia wanafunzi kwa kiasi kikubwa kutokuwa katika giza," alisema.

Mhina anasema, kuwepo nishati hiyo imewaboreshea mazingira walimu kubaki katika kijiji hicho ikilinganishwa na awali walikuwa wanaondoka.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mpale, Mary Kiwanga, anasema umeme huo umewasaidia kuimarisha hali ya usalama kijijini hapo, mtu atakuwa na hofu ya kwenda kuvamia nyumba ya mtu maana ataonekana.

"Hata akiwaza kwenda kumfuata binti wa mtu usiku atakuwa na hofu kuna mtu atamuona atakamatwa," anasema Kiwanga,

Anasema gharama za umeme zinalalamikiwa na wananchi hawana jinsi ni bora kutumia huo uliopo kuliko kuacha kwa sababu una gharama za juu.

"Ukiangalia suala la mafuta ya taa au matumizi mengine yanayotusababishia tupate mwanga yapo juu zaidi kuliko huu umeme wa jua. Ni kweli kwa sehemu kubwa wanalalamika tunaendelea kuwahamasisha ni bora kulipa Sh. 11,000 kwa mwezi unakuwa salama kuliko vibatari ni hatarishi zaidi,"

### KILIO CHA GHARAMA

Lisha ya wananchi hao kufurahia nishati, baadhi wanalalamika gharama za kununua ni kubwa na wengi hawana uelewa wa kutosha.

Nasibu Mhammed anasema, gharama za umeme huo wa jua, ni kubwa kwani kwa mwezi wanatakiwa kulipa Sh. 11,000 ambayo unalipia kama vocha.

"Mimi sijajiunga na huo umeme wenzangu wanasema ni gharama kubwa kutokana na kipato tulichokuwa nacho hapa kijijini bado ninaendelea kutumia kibatari lakini wenye sabufa, au majokofu wao nasikia wanalipia sh. 36,000 kwa mwezi," anasema.

Mwajuma Issa, anasema hakubaliani na umeme huo, kwa kuwa kijijini wameshaahidiwa na serikali kupatia umeme wa Wakala wa Nishati Vijijini (Rea)

### MWENYEKITI KITONGOJI

Mwenyekiti wa Kitongoji hicho, Abdallah Mdoe, anasema mkataba wa kwanza kwa mwezi walikuwa wanalipa sh 11,000 kwa sasa wamejiwekea utaratibu na kampuni ya Ensol unaweza kununua umeme hata wa sh 2,000.

"Mafuta ya taa kutumia ni gharama lakini umeme wa Sh 2,000 unaweza kutumia hata siku sita hapa ninapata unafuu," anasema

Anasema ongezeko la gharama, ni gumu kuepuka kwa kuwa nishati hiyo inawasaidia na anafafanua: "Katika maisha hakuna kitu kizuri hata ukitoa pepo unatumia gharama kumtoa...lazima kuna mwingine haoni umuhimu wa huu umeme hilo nalo ni changamoto ya namna ya maisha yake,"

### MWENYE MASHINE

Hassan Bakari anatamani kuacha kutumia mafuta ya dizeli katika mashine yake ya kusaga ili ajiunge na umeme wa jua changamoto aliyo nayo bado hajapata elimu ya kutosha katika gharama zake kwa mwezi.

"Mafuta ya dizeli ninayonunua kila siku ni Sh. 6000 huenda napata hasara kama wangenielewesha nikajua gharama za huo umeme katika hii mashine yangu kwa mwezi ningekuwa nautumia nikaachana na huu mfumo wa mafuta," alisema.

"Uelewa bado ni mdogo yaani elimu inatakiwa ifanyike watoe elimu ya kutosha ili na vijiji vingine viweze kupata umeme wanazalisha mwingi watumiaji ni wachache," anasema Bakari.

### OFISA MRADI

Ofisa Tawala wa mradi wa Ensol, Erica Jackson anasema mwaka 2014 walianza kufanya utafiti kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (Rea) kwa ajili ya kuona kijiji cha kuwapatia huduma hiyo.

"Wakati tunafanya utafiti huo kijiji cha Mpale kilijitokeza zaidi na hatimaye kikachaguliwa na mtambo huo wa nishati uliwekwa 2017 na ulizinduliwa rasmi Septemba 9, 2017 tukiwa na wateja 61," anasema

Anasema kwa sasa wana wateja 250 jambo ambalo wanajivunia na zaidi ya biashara 20 zinatumia umeme na nyumba za watumishi wamewapatia umeme huo pamoja na shule na zahanati.

Anakiri changamoto waliyo nayo, ni uelewa mdogo kuhusiana na nishati hiyo wengi huzani kuwa umeme huo hauna nguvu jambo ambalo sio la kweli.

"Umeme tunaozalisha hapa wa kilowati 48 na unaweza kutumia katika jokofu hata wale wenye mashine za kuchomelea anaweza kuutumia na yule ambaye ana shida aje tutampatia," anasema.

Jackson anasema, kwenye malipo umeme huo malipo yake ni tofauti na Tanesco umeme ni wa matumizi ya mwezi yaani wanauiti ni wa kifurushi kwani wana tarifu tofauti tofauti ya kwanza ni sh 11,000, 20,000, 36,000, 53,000, 70,000 hadi 100,000 kulingana na matumizi yako.

"Wengi wa majumbani wanatumia umeme wa mwezi ambao ni Sh 11,000 utakapokwisha atakuja kulipia na kupatiwa umeme wake," anasema.

Anasema kuna baadhi ya wananchi wanalalamikia gharama kutokana na hali ya maisha yalivyo kipato chao wanategemea msimu wa kilimo.





## Tari yatakiwa kutafiti mbegu bora alizeti

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Nchini (Tari), Kituo cha Uyole imetakiwa kufanya utafiti kutafuta mbegu bora ya alizeti itakayowasaidia wakulima kupata mazao mengi.

Wito huo ulitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, wakati akizindua jukwaa la wadau wa zao la alizeti lenye lengo la kuwasaidia wakulima kutatua tatizo la wakulima kulima mashamba makubwa na kuambulia mavuno kidogo.

Alisema kwa sasa wakulima wengi wa alizeti wanalima mashamba makubwa na kuyahudumia kwa kufuata kanuni za kilimo bora, lakini wakati wa mavuno wanaambulia mazao machache yasiyolingana na nguvu au rasilimali walizozitumia.

"Mimi naona hapa tatizo ni aina ya mbegu wanazopanda wakulima ndizo zinasababisha wapate mazao kidogo, hivyo nawataka watafiti wa kilimo kupitia kituo chetu cha Uyole, fanyieni kazi suala hili kwa kutafuta mbegu nzuri zitakazoondoa tatizo hili kwa wakulima wetu," alisema Ntinika.

Alisema zinahitajika mbegu ambazo zitamfanya mkulima afaidi jasho lake kwa kupata mavuno mengi ili aweze kurejesha gharama alizotumia na kuambulia faida inayokidhi mahitaji yake.

Awali, wakulima wadogo wa alizeti walisema kuwa wanalima alizeti kwa kufuata ushauri wa wataalamu wa kilimo na wanajitahidi kupanua mashamba yao ili wapate mavuno ya kutosha, lakini jitihada hizo haziwasaidii kujikwamua na umaskini.

Salehe Mwasole, mmoja wa wakulima wa alizeti wilayani Mbeya, alisema kulima alizeti kunahitaji moyo kwa vile mkulima anaweza kulima shamba kubwa kwa gharama za juu, lakini mavuno yanapatikana kidogo ambayo hayalingani na gharama za uzalishaji.

Alisema kitendo hicho kinawakatisha tamaa kuendelea kulima alizeti na baadhi ya wakulima wameamua kulima mahindi ambayo yanawapatia faida kidogo.

"Tunalima alizeti kwa gharama kubwa, lakini mavuno hayalingani na ukubwa wa mashamba tunayolima wala gharama tunazotumia, ukipata hasara mwaka huu hutamani tena kurudia labda uwe na moyo mgumu, ndio sababu wapo wakulima wenzetu wamekata tamaa na kuamua kulima mazao mengine," alisema Mwasole.

# CCM yatoa salamu kwa Chadema

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

UONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, umewataka viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kuwa wavumilivu katika kipindi hiki ambacho chama chao kinakimbiwa na wanachama wake wakiwamo madiwani, wabunge na viongozi wa ngazi mbalimbali.

Ushauri huo ulitolewa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, wakati alipokuwa anampokea aliyekuwa Diwani wa Kata ya Iyunga, jijini Mbeya kupitia Chadema, Mchungaji Essau Kalinga, ambaye alitangaza kuachana na chama hicho na kujiunga na CCM.

Mwakasole alisema suala la vyama vya siasa kukimbiwa na wanachama sio geni kwa siasa za Tanzania na kwamba hata CCM kiliathirika na jambo la aina hiyo kabla ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Alisema wakati huo viongozi mbalimbali wa CCM walikikimbia chama hicho wakiwamo waliokuwa wanasiasa mahiri ambao wengi walihamia Chadema na kuhatarisha ustawi wa chama hicho tawala.

"Tangu mwaka jana mpaka sasa tumeshapokea madiwani 18 waliokuwa Chadema ambao wamehamia kwenye chama chetu, sasa wenzetu wavumilie tu, haya yalituathiri hata sisi mwaka 2015 na baadhi walihamia Chadema na siku ya tatu wakagombea urais," alisema Mwakasole.

Aliwataka viongozi wa Chadema kuacha kufikiria kuwa wanachama wao wanaohamia CCM wananunuliwa na badala yake wazifanyie kazi tuhuma ambazo wanachama hao wanazitaja wanapohama ikiwamo mambo ya migogoro.

Mwakasole alisema kinachowavutia wengi kuhamia CCM ni utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 pamoja na ahadi mbalimbali ambazo chama hicho kiliwaahidi wananchi.

Akizungumzia sababu za kukihama Chadema, Kalinga alisema aliamua kuhamia CCM baada ya kuridhishwa na utendaji kazi wa chama hicho tofauti na wengi walivyokuwa wanatarajia wakati wa uchaguzi wa 2015.

Alisema kama mchungaji alikuwa anaomba kwa muda mrefu Tanzania ipate rais mchapakazi kama alivyo Rais Magufuli na hivyo hakuona sababu ya kuendelea kubaki Chadema.

"Rais Magufuli anafanya mambo ambayo yanatubariki Watanzania kwa kiwango kikubwa, anatekeleza mambo ambayo hatukuwahi kuyafikiria kuwa yangetekelezwa na serikali ambayo ipo chini ya CCM, kuna miradi mikubwa inatekelezwa ambayo inambariki kila mpenda maendeleo," alisema Kalinga.

Kwa upande wake, Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, alisema chama hicho kwa sasa kinaandaa siku maalumu kwa ajili ya kuwapokea madiwani 14 waliohamia kutoka Chadema.

Alisema baadhi ya madiwani hao akiwamo aliyekuwa Meya wa Jiji la Mbeya, Mchungaji David Mwashilindi na Naibu wake Fanuel Kyanula, walishapokelewa na Katibu Mkuu wa Chama hicho, Dk. Bashiru Ally, jijini Dodoma.

Madodi alisema chama hicho kwa sasa kinakubalika kwa kiasi kikubwa na wananchi kutokana na kutekeleza miradi ambayo inagusa moja kwa moja maisha yao ikiwamo huduma za afya, elimu na miundombinu ya barabara.




Mmoja wa wafanyabiashara wa nyama katika eneo la Soweto, jijini Mbeya, akiwa amebeba kitoweo hicho begani akihamisha kutoka kwenye gari kwenda kwenye bucha jana, kitendo ambacho serikali ilikizuia kutokana na sababu za kiafya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wenye ulemavu Tunduma waomba mtaji kujinasua

**Na Nebart Msokwa, TUNDUMA**

WATU wenye ulemavu wanaojipatia mahitaji yao kwa kuombaomba kwenye mpaka wa Tanzania na Zambia mjini Tunduma katika Wilaya ya Momba mkoani Songwe, wamewaomba wasamaria wema kuwasaidia mitaji ili waanzishe miradi itakayowafanya waachane na kuomba.

Walitoa ombi hilo juzi walipokuwa wanapokea misaada ya vitu mbalimbali kutoka kwa wafanyakazi wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco) wa Wilaya ya Momba ambao walikuwa wanasaidia watu wenye uhitaji mitaani na hospitalini.

Mmoja wa 'ombaomba' hao, Anania Mwashilindi, alisema alipata tatizo la kutoona macho akiwa na miaka mitatu na kwamba kwa muda mrefu sasa amekuwa akifanya kazi hiyo ya kuomba mitaani ili kuendesha maisha yake.

Alisema kwa sasa ameanza kuichukia kazi hiyo na anatamani kupata mtaji ili aanzishe biashara ya kudumu itakayokuwa inamwingizia fedha badala ya kuomba.

Alisema endapo watapata mtaji wana uwezo wa kukaa sehemu moja na kufanya biashara yoyote ambayo itakuwa rahisi wateja kuwakuta badala ya kuendelea kukaa mitaani na kuomba.

Alisema kazi ya kuomba inawadhalilisha kwa kuwa baadhi ya wananchi wanawadharau kutokana na kazi hiyo na wakati mwingine huwa wanachukiwa na wanaowasaidia.

"Mimi nikipata mtaji nina uwezo wa kuanza kufanya biashara ya viatu, hivyo tunawaomba wasamaria wema watusaidie tupate mitaji, hata sisi hatupendi kukaa humu barabarani na kuomba," alisema Mwashilindi.

Naye Flora Nicolous, alisema ana familia ya watoto wanne ambao baadhi wanasoma, lakini wengine ni wadogo na maisha yake anayaendesha kwa kutumia fedha na vitu anavyopewa na wasamaria wema. Alisema yeye anafikiria kuanza kufanya biashara ya viatu lakini hana mtaji, hivyo akawaomba wadau mbalimbali kujitokeza kumsaidia kupata mtaji ili aanze kufanya biashara hiyo.

Alisema mmoja wa watoto wake kwa sasa anasoma darasa la saba, lakini hana uhakika wa kumwendeleza kwenye masomo yake kutokana na kipato chake kuwa kidogo.

Baadhi ya wafanyakazi wa Tanesco Wilaya ya Momba walisema waliamua kulisaidia kundi hilo kutokana na kuwa na mahitaji makubwa na matatizo ya viungo wanashindwa kumudu maisha yao.

Mmoja wa wafanyakazi hao, Dickson Bundala, alisema katika wilaya hiyo kuna tatizo kubwa la ombaomba ambao wametapakaa maeneo mbalimbali na kwamba waliguswa kwenda kuwasaidia baada ya kubaini kuwa baadhi yao hawana msaada. Meneja wa Tanesco Mkoa wa Songwe, Mhandisi Kisika Kisika, alisema fedha zilizotumika kununua vitu ambavyo waliwapatia ombaomba hao, walichangishana wafanyakazi wote wa shirika hilo.





# Mwakyembe ataja kikwazo cha lugha ya Kiswahili

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk .Harrison Mwakyembe, amesema bado kuna baadhi ya wasomi wa vyuo vikuu wa kada ya Kiswahili wanatukuza lugha za kigeni, jambo ambalo linadidimiza lugha hiyo.

Dk. Mwakyembe alitoa kauli hiyo alipokuwa akifungua mafunzo ya stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni yaliyohusisha wadau mbalimbali wa Kiswahili chini ya uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Alisema wasomi hawapendi kuweka wazi wanasomea lugha hiyo kwa kuhisi kuwa watadharaulika na jamii.

"Unakuta mtu anasomea Kiswahili, lakini ukimuuliza unasomea nini anakwambia anasoma sayansi ya jamii kuhofia kudharaulika...nataka niwaambie kila Mtanzania ana wajibu wa kukitukuza Kiswahili," alisema.

Aliongeza: "Tusipoangalia Wachina watatuzidi Kiswahili, kwa kuwa wanafanya juhudi kubwa ya kujifunza Kiswahili kuliko hata sisi wenye lugha yetu," alihadharisha.

Alipongeza chuo hicho kwa kuanzisha kanzi data ya mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni itasaidia kwa kiasi kikubwa kujenga na kurejesha heshima ya lugha hiyo nchini na Afrika.

Dk. Mwakyembe alisema pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali kurejesha heshima na hadhi ya lugha mama ya Taifa bado kuna watu wanatumia nguvu kuikwamisha serikali katika juhudi hizo.

Kwa upande wake, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), Consolata Mushi, alisema kuwa kwa kushirikiana na UDOM waliona umuhimu wa kuienzi kwa mapana lugha hiyo ili kuchochea uchumi wa viwanda.

Mushi alisema katika kuunga mkono juhudi za serikali katika kukuza uchumi wa viwanda wananchi pamoja na wasomi wa vyuo vikuu nchini wanatakiwa kuanza kutumia Kiswahili katika mawasiliano ya umma.

"Tunaomba kuendelea kutumia lugha ya Kiswahili kwa kujidai na kujiamini kwani kwa kufanya hivyo mataifa mengine yatatuheshimu," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Makamu Mkuu wa UDOM, Prof. Justin Ntalikwa, alisema lugha ya Kiswahili ikitumiwa vyema ndiyo itakayoharakisha maendeleo nchini.

# Nacopha yaomba viongozi wa dini

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

VIONGOZI wa dini nchini wameombwa kutumia majukwaa yao kukemea suala la unyanyapaa kwa watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (VVU) na kuombea dawa za kurefusha maisha (ARVs) ili ziwafae wanaozitumia.

Ombi hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (NACOPHA), Leticia Mourice, katika uzinduzi wa kampeni ya kushirikisha viongozi wa dini kupinga unyanyapaa na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Kampeni hiyo inaratibiwa na Nacopha kupitia mradi wa 'Tuyajenge' unaofadhiliwa na Mfuko wa Rais wa Marekani wa kupambana na Ukimwi (PEPFAR) na Shirika la Misaada la Kimataifa la Marekani (Usaid).

Alisema unyanyapaa wa kimya kimya ndio unaoua watu kimya kutokana na kutojikubali na kunyanyapaliwa.

"Unyanyapaa umekuwa tishio kuliko virusi vya Ukimwi, nchi imepoteza watu wengi kutokana na unyanyapaa, wanaume wengi wanashindwa kujitokeza kupima virusi ili kutambua hali zao na kuanza dawa mapema, wanashindwa kuwa wafuasi wazuri kisa unyanyapaa," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema sasa ni wakati wa kuyajenga kwa pamoja ili kuondoa kabisa tatizo la unyanyapaa kwa viongozi kutumia fursa mbalimbali za kidini kama kanisani na msikitini.

"Sisi WAVIU utanihitaji faraja, kipindi nikiwa Bukombe nilihudumia MVIU mwenzangu alipima na kupokea majibu yake, nilipomuuliza mama una umri gani akaanza kunitajia namba za simu...hapa mtaona namna gani inavyouma, pamoja na kwamba alishafanyiwa counseling (ushauri), lakini bado akili iligoma," aliongeza.

Alisema Nacopha inatambua mchango wa viongozi wa dini na inawaheshimu, inawaamini na kuwasilikiza sana.

"Kiukweli hatuna sababu ya kunyanyapaa mtu yoyote ambaye ana maradhi ya aina yoyote, sisi leo tunaishi na virusi vya Ukimwi, lakini kuna wengine wanaishi na virusi vya corona kwa hiyo niombe huu unyanyapaa kuanzia leo tuutokomeze kabisa," alisisitiza.

Kuhusu suala la ukatili wa kijinsia kwa watoto, alisema limeendelea kuwa tatizo kubwa hapa nchini ambapo watoto wengi wanaoshi na Ukimwi wananyimwa haki zao za msingi kama elimu, afya na malezi bora.

"Hii yote ni kwa sababu ya fikra potofu dhidi ya wanaoishi na virusi vya Ukimwi, watoto wa kike wanafanyiwa vitendo vya ukatili...inauma sana, niombe kupitia kampeni hii wote tushikamane, tuwe na sauti moja tutetee haki za watoto, na kwa kufanya hivi tutayafikia malengo yetu," aliongeza.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo (CCT), Askofu Peter Konki, alisema anatamani matumizi ya ARVs yawe ya kawaida kama dawa za magonjwa mengine ili kuondoa unyanyapaa.



Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omari Mkulo (kushoto) na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Zuberi White (wa pili kushoto), wakiangalia bidhaa zinazozalishwa na kikundi cha wajasiriamali cha Chiyende cha wilayani Kongwa, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ndugai akemea wanaoficha wanaowapa mimba wanafunzi

**Na Ibrahim Joseph, KONGWA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amekemea tabia ya baadhi ya wanawake ambao bado wanakumbatia mila na desturi potofu kwa kuwaficha wanaume wanaowapa mimba wanafunzi.

Kauli hiyo aliitoa juzi katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Wilaya ya Kongwa.

Ndugai alisema bado kuna baadhi ya kinamama wanaoficha wanaume wanaoharibu malengo ya wanafunzi.

Alisema mila na desturi hizo zimekuwa zikiendelea kuchangia wanafunzi kupewa mimba kutokana na baadhi ya wazazi wa kike kuwakaribisha wanaume wenye mahusiano na watoto wao wa kike.

Alieleza idadi inaonyesha kuwa wanafunzi wanaopewa mimba inaongezeka hivyo wazazi wa pande zote wahakikishe wanaondoa mila hizo mbaya ili kuwalinda watoto wao wasikatishe masomo.


Pia Ndugai aliwapongeza wanawake kwa kuwa karibu na familia zao kwa kuhakikisha watoto wao wanapata elimu.

Alisema maadhimisho hayo yawakumbushe wanawake wote nchini kumiliki uchumi mkubwa kwa kuanzisha miradi mikubwa ya uchumi.

"Mimi nawashangaa kinamama kwenye mikusanyiko mkipewa nafasi mnazungumzia kumiliki uchumi mdogomdogo, mnatakiwa kuondokana na mawazo hayo kandamizi, anzisheni miradi mikubwa kwa sababu hakuna aliyeandikiwa kumiliki uchumi mkubwa wote tuna haki sawa kwenye hilo," alisema.

Aliitaja baadhi ya miradi hiyo wanayotakiwa kuanzisha ni viwanda vikubwa na vidogo, maduka makubwa ya biashara na kilimo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Kongwa, Faraja Kasuwi, alisema malengo ya maadhimisho hayo ni kutathmini utekelezaji wa afua za kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi, kijamii na kisiasa.



# Samia sasa ataka kasi ongezeko nishati mbadala

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

JUKWAA la nishati nchini (TEP) limetakiwa kuwa na mikakati madhubuti itakayosaidia kuwapo kwa nishati mbadala endelevu, ili kupunguza ukataji miti ambao ni chanzo cha uharibifu wa mazingira na tishio nchi kugeuka jangwa.

Hayo yalisemwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, wakati akifunga mkutano wa Jukwaa la Nishati Tanzania mjini Zanzibar na kujumuisha vyuo vikuu na taasisi zinazotoa elimu kuhusu nishati pamoja na sekta binafsi zinazozalisha nishati hiyo.

Alisema yapo matumizi mabaya ya uharibifu wa mazingira ya ukataji wa miti kwa matumizi ya kuni zaidi vijijini na kutishia nchi kugeuka jangwa.

Alisema njia pekee za kupambana na uharibifu wa mazingira na uharibifu wa misitu ni wataalamu kubuni nishati mbadala endelevu kwa maslahi ya taifa.

Kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia (WB) katika mwaka 2017, hekta 48,389 za msitu zinaharibiwa kwa matumizi ya kuni na shughuli nyingine.

''Hicho ni kiwango kikubwa cha uharibifu wa msitu ambapo nyinyi wataalamu mnatakiwa kuja na suluhisho la matumizi ya nishati mbadala endelevu ili kuiokoa nchi kugeuka jangwa,'' alisema.

Suluhu ni mlezi wa jukwaa la Nishati Tanzania linaloundwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na taasisi za elimu ya sayansi ikiwamo Taasisi ya Sayansi ya Karume iliopo Zanzibar na Taasisi ya Sayansi ya Dar-es-Salaam DIT kwa kushirikiana na Umoja wa Vyuo Vikuu vya Uholanzi.

Aidha, aliishukuru Serikali ya Uholanzi na kwamba amefurahishwa na kuona jukwaa hilo limesaidia kuwapo kwa usawa wa kijinsia kwa kuwawezesha wanafunzi wa kike kusoma masomo ya shahada ya juu ya uzamivu katika sekta ya nishati na gesi.

Naye, mwakilishi wa Ubalozi wa Uholanzi nchini, Rogier Venstreaten, alisema nchi yake ipo mstari wa mbele kuona Tanzania inapambana na uharibifu wa mazingira kwa kuwepo kwa nishati mbadala yenye maslahi kwa wananchi.

Mwakilishi wa Vyuo Vikuu vya Uholanzi vilivyomo katika mradi huo, Dk. Robeit Hack, alisema wanafunzi wa vyuo vikuu pamoja na taasisi zake waliopo nchini wanaweza kufaidika na mpango huo kama watajikita kwenye masomo ya sayansi na utafiti.

''Mpango wetu huu umelenga kuongeza wingi wa wanafunzi kuanzia katika ngazi za shule kwa kusoma vizuri masomo ya sayansi ambayo yatawawezesha kuwa watafiti wa fani mbalimbali,'' alisema.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar (Uendeshaji na Utawala), Abdallah Mzee (kulia), akizungumza na Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti wa wizara hiyo, Khalid Waziri, katika mkutano wa kutathmini maendeleo ya elimu Zanzibar juzi.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wapendekeza kujengewa uwezo zabuni

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa bodi ya zabuni kutoka wizara na taasisi mbalimbali za serikali wameiomba Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA), kuhakikisha wanawajengea uwezo wataalamu wa ndani katika kutoa huduma za zabuni.

Wakizungumza katika mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa na mamlaka hiyo kwa wajumbe hao yaliyofanyika katika ukumbi wa mtakwimu mkuu wa serikali, alisema ikiwa mamlaka hiyo itawajengea uwezo wataalamu hao kuwa na majengo yenye kiwango.

Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Kilimo, Mifungo na Uvuvi ambaye ni mwenyekiti wa bodi hiyo, Sheha Idrisa Hamdan, alisema imezoeleka kuwa wataalamu wengi wanaotoa huduma hizo wanatoka nje ya Zanzibar.

Kuhusu mafunzo hayo, alisema yana manufaa makubwa katika kuwawezesha kufanya zabuni kwa kufuata sheria na kutunza upatikanaji wa huduma hizo katika thamani inayostahiki.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Serikali kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Salma Hamad Suleiman, alisema mafunzo hayo kwa kiasi kikubwa yataamsha ari kwa watendaji katika utekelezaji wa kazi zao za kila siku na kupunguza changamoto ya manunuzi ambayo hayafahamiki katika taasisi zao.

Aliwashauri wanunuzi wenzake hasa vijana kujitahidi kufuata maadili ya taaluma yao kwa kufanya manunuzi kwa mujibu wa sheria.

Ofisa Mtathmini Majengo ZPPDA, Hafidh Rashid Zam, alisema mafunzo hayo yana lenga kujenga uwezo kwa wakurugenzi na bodi ya zabuni kwa kufuata njia sahihi za manunuzi kwa mujibu wa sheria, ili kuhakikisha thamani ya fedha halisi inapatikana katika manunuzi hayo. Aidha, alieleza kuwa mamlaka imeamua kutoa mafunzo hayo kutokana na changamoto zinazojitokeza katika manunuzi ambazo zimeonyesha wataalamu hao hawana uelewa wa kutosha.

"Lengo letu kutoa mafunzo haya ni kuwajengea uwezo watendaji hawa na kuondosha changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika njia za manunuzi," alisisitiza.

# Shein: Msanii Bibi Siti aenziwe

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wananchi kumuenzi msanii wa zamani wa Zanzibar Bibi Siti binti Saad kwa kutumia kazi kwenye shughuli mbalimbali.

Aidha, alisema nyimbo zake zilikuwa na sifa, mvuto, ghaiba na elimu kubwa kwa jamii wakati uliopita na sasa.

Rais Shein aliyasema hayo wakati akizungumza na uongozi wa taasisi ya Sinti Binti Saadi, visiwani hapa.

Alisema nyimbo za msanii huyo zimeweza kuelimisha, kuburudisha, kuadabisha na kufunza jamii na ziligusa katika mambo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Dk. Shein alieleza kuwa iwapo kazi za binti Saad zitasambazwa zikiwamo CD za nyimbo zake zitapata soko kubwa sana katika ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki, Kaskazini na Kusini mwa Afrika pamoja na nje ya Bara hilo.

Alisema hatua hiyo ni nzuri kwa kuwa mbali ya kumuenzi mwanaharakati huyo, pia itasaidia kuzitangaza kazi zake sambamba na kuongeza mtaji kwa taasisi hiyo.

Alieleza kuwa soko la nyimbo zake lilipatikana kutokana na historia ya msanii huyo ambaye alikuwa ni mwanamke jasiri na aliyekuwa na kipaji cha sanaa na sauti nzuri iliyowavutia watu wengi ambayo bado watu wanatamani kuisikia na kumfahamu vilivyo mwanaharakati huyo.

Dk. Shein alisema mengi aliyoyafanya msanii huyo wakati wa uhai wake hayaonekani hivi sasa na mengine yamebakia kwenye picha za kubuni pamoja na kuandikwa vitabuni tu, hivyo, ni jambo jema taasisi hiyo ikafanya juhudi za makusudi katika kuhakikisha mwanaharakati huyo anatambulikana ndani na nje ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa Rais Shein, taasisi hiyo imefanya vyema kuhakikisha kazi alizozifanya wakati wa uhai wake zinajulikana na jamii iliyopo pamoja na vizazi vijavyo.

Aidha, Dk. Shein aliipongeza taasisi hiyo kwa kuendelea na harakati za kuzitunza kazi za mwanaharakati huyo, huku akisisitiza haja ya kuongeza kasi ya kumtangaza msanii huyo ambaye alipata umaarufu mkubwa ndani na nje ya Zanzibar.

Awali, mwenyekiti wa taasisi ya mwanaharakati huyo, Nasra Mohamed Hilal, alimweleza Dk. Shein mafanikio yaliopatikana katika taasisi hiyo pamoja na malengo yaliyowekwa.

Alisema taasisi hiyo imeweza kufanya mambo mengi ikiwa ikiwamo kufanya utafiti mbalimbali kuhusiana na mwanaharakati huyo pamoja na makongamano ya Kiswahili, kutoa mafunzo ya uchoraji, kutoa vyeti vya uanachama na mengineyo.

Bibi Siti Binti Saad alizaliwa katika kijiji cha Fumba mwaka 1870 na kuishi miaka 80 ambayo miaka 40 ya kwanza ya uhai wake aliitwa Mtumwa Binti Saad wakati huo akiwa mfinyanzi wa vyungu vya kupikia na kazi nyingine za usanii wa mikono.

# H/shauri yatoa mil. 29/- ujenzi sekondari

**Na Neema Sawaka, USHETU**

HALMASHAURI ya Ushetu, Kahama mkoani Shinyanga imetoa Sh. milioni 29 kwa ajili ya ukamilishaji wa shule ya sekondari ya kata ya Ubagwe ili kuwaondolea adha wanafunzi ya kutembea zaidi ya kilomita 20, huku wakivuka mto kwenda shule ya jirani iliyoko kata ya Ulowa.

Kutokana na changamoto hiyo, wanafunzi 93 kati yao 52 ambao ni wasichana, wamebainika kukatisha masomo. Wanafunzi hao ni toka kata ya Ubagwe, vijiji vya Mwadui na Bugomba.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ubagwe, Lucas Magembe, aliyasema hayo juzi katika ufunguzi wa shule hiyo ambayo imekamilika majengo mawili na ofisi ya walimu huku majengo mawili yakiwa usawa wa lenta.

Magembe aliishukuru halmashauri kwa kutoa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa ujenzi wa vyumba vya madarasa vilivyokamilika kwa kuwa wanafunzi walikuwa wakitembea umbali mrefu jambo ambalo liliwafanya wachache kumaliza elimu ya sekondari wengine kuishia njiani.

"Mpaka sasa shule yetu ina vyumba viwili tu vilivyokamilika na kwa wanafunzi walioripoti kuanza kidato cha kwanza kukaa kila darasa wanafunzi 60. Lakini bado tuna changamoto ya nyumba za walimu kwani wanalazimika kupanga gesti kwa sababu nyumba za kupanga pia hakuna," alisema Magembe.

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Ushetu, Wandere Lwakatare, alisema halmashauri hiyo ina shule 18 za sekondari ambazo zimesajiliwa na kufika kidato cha nne.

"Kutokana na changamoto ya kutembelea umbali mrefu, wanafunzi 93 wamebainika kukatisha masomo na wote hao walikuwa wakisoma Shule ya Sekondari Ulowa, hivyo jamii ishirikiane na serikali kuhakikisha idadi ya wanafunzi wanaoanza shule ndio wanaomaliza," alisema.

Lwakatare alisema halmashauri, katika shule za sekondari 18, ina vyumba vya madarasa 171 wakati mahitaji ni vyumba 196, hivyo kufanya upungufu kuwa vyumba 25, sawa na asilimia 13.

Diwani wa Ubagwe, Hamis Majogolo, alisema wazo la kuanzisha shule alilipa kipaumbele kutokana na eneo hilo kukosa shule na kuhamasisha wananchi kuanza michango ya ujenzi wa shule kwa kila kaya kuchangia Sh. 15,000, huku Halmashauri ikiongeza Sh. milioni 29.

# Teknolojia ya panya buku yaokoa wagonjwa wa TB

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI isiyo ya kiserikali inayojishughulisha na kufundisha panya kutatua matatizo ya kibinadamu (Apopo), imesema teknolojia inayotumiwa na panya buku kugundua maambukizi ya kifua kikuu(TB), imesaidia kwa kiwango kikubwa kuokoa maisha ya watu.

Hayo yalielezwa kwa wanahabari na Mkuu wa Mradi wa TB kutoka Apopo, Lena Fiebig katika maonesho ya Wiki ya Ubunifu jijini Dar es Salaam ambayo yameandaliwa na Mfuko wa Ubunifu kwa Maendeleo ya Watu (HDIF) na wadau wengine.

Fiebig alisema kati ya mwaka 2007 hadi Julai mwaka jana, walifanikiwa kupima sampuli 591,878 zinazodhaniwa kuwa na kifua kikuu na kati ya hizo, sampuli zilizobainika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo zilikuwa ni 15,679 na kufanikiwa kudhibiti na kuwatibu wagonjwa wake.

"Tunasema tumeokoa maisha ya wagonjwa kwa sababu baada ya kuonekana awali kwamba hawakuwa na maambukizi na baadaye kupitia panyabuku wakabainika na kutibiwa, haya ni mafanikio na ni jambo jema kuwa maisha yao yameokolewa," alisema Fiebig.

Alisema panya buku hao wanaogundua maambukizi hayo ya TB ni wale waliopatiwa mafunzo maalum ya miezi nane hadi 12 kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kilichopo mkoani Morogoro.

Akizungumzia kazi inayofanywa na panya buku hao, daktari kutoka taasisi hiyo ya Apopo, Dk. Joseph Soka, alisema walianza kushirikiana na hospitali na vituo vya afya toka mwaka 2007, wakati huo sampuli zilikuwa zinapelekwa Morogoro.

"Awali sampuli zilikuwa zinasafirishwa kwenda Morogoro kwa ajili ya kupimwa na panya, halafu kuthibitishwa kwa teknolojia zilizopitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO), tukapata changamoto ya ucheleweshaji wa majibu ambayo yalikuwa yanachukua siku 8-10, tukapata ufadhili HDIF ambao walituwezesha ufadhili na tukajenga mahabara Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza muda wa kupata majibu kwa mgonjwa hadi siku moja, kuongeza idadi ya sampuli na kuongeza vituo vya afya zaidi.

"Novemba mwaka 2016 tulianza kazi rasmi Dar es Salaam. Tunapata wastani wa sampuli 210 kwa siku kutoka kwenye vituo 53, zikiwamo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Mloganzila, Hospitali zote za Rufani za Mkoa wa Dar es Salaam na vituo vya afya na zahanati zote za serikali na binafsi ambazo zina pima kifua kikuu. Majibu yetu yamekuwa yakitolewa ndani ya saa ishirini na nne ndani ya siku moja tokea tumepata sampuli ya mgonjwa."

"Teknolojia hii inarahisisha kazi kwa sababu panya buku ana uwezo wa kupima sampuli 100 ndani ya dakika 20 wakati ukitumia darubini itamlazimu mteknolojia wa maabara mmoja kufanya kazi hii kwa wiki moja na sampuli zinazopimwa na panya ni zile ambazo zimeonekana kwenye mashine hazina maambukizi ya ugonjwa huo hivyo huzipima tena," alisema Dk. Soka.




Mafundi wakitengeneza mashine ya kuchonga barabara 'kijiko', kilichoharibika wakati wa ujenzi unaoendelea wa barabara ya Mwenge – Morocco, eneo la Bamaga, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Matumizi mifuko karatasi yahimizwa

**Na Mwandishi Wetu, MUFINDI**

MKURUGENZI Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, amewataka Watanzania kuanza kutumia mifuko mbadala ya karatasi kwani haina athari kiafya pia ni rafiki kwa mazingira.

"Ni jambo la kushangaza kuona asilimia kubwa ya mifuko ya karatasi inayotumika nchini Rwanda na Kenya inazalishwa Tanzania huku Watanzania bado wakiendelea kutumia mifuko ya plastiki ambayo imeshazuiliwa, jambo linalokinzana na dhana ya kukuza uchumi wa viwanda," alisema Dk.Gwamaka.

Akizungumza katika ziara yake ya siku moja kutembelea Kiwanda cha karatasi cha Mufindi Maper Mills ltd (MPM wilayani Mufindi katika mkoani Iringa kujionea uwezo wa kiwanda kuzalisha malighafi kwa ajili ya bidhaa mbadala za mifuko ya kubebea pamoja na vifungashio, alipongeza kiwango cha bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho kwa sasa.

Alisema toka wapige marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki mwaka jana kumekuwa hakuna tofauti kubwa kwani matumizi ya bidhaa hiyo yameongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na takwimu za uzalishaji zilizopo viwandani.

"Awali kiwanda cha Mufindi Paper Mills Ltd (MPM), mwaka 2014/2015 kilikuwa kinauza tani 15,000 kwa soko la ndani ambapo kwa nje ilikuwa tani 26,000," alisema na kuongeza kuwa; kinachoshangaza kuwa kwa mwaka jana 2018/2019 uzalishaji umepungua mpaka kufikia tani 7,000 kwa soko la ndani wakati soko la nje ulipanda mpaka kufikia tani 40,000.

Dk. Gwamaka alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara ambao siyo waaminifu wameendelea kuingiza nchini mifuko ya plastiki kupitia njia za panya, hali inayochangia ongezeko la mifuko sokoni na kusababisha kufa kwa viwanda vya ndani na hatimaye kukosa mapato ya serikali.

Alisema kwa mujibu wa sheria mpya ya mazingira watu ambao watazalisha au kuingiza nchini mifuko hiyo batili, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ikiwamo faini kubwa.

"Wakati umefika kwa Watanzania kuachana na tabia ya kulalamika suala la ajira badala yake kuanza kuchangamkia fursa zinazojitokeza kupitia raslimali misitu, ambapo kuna fursa nyingi za kujikwamua kiuchumi hali itakayofanikisha kufikiwa kwa azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025," alisisitiza.

Kaimu Meneja Mkuu wa kiwanda hicho, Mwandisi Gregory Chogo, alisema wakati umefika Watanzania kuchangamkia fursa kupitia bidhaa mbadala za mifuko ya kubebea pamoja na vifungashio vinavyotokana na karatasi.

"Kiwanda chetu kinauwezo mkubwa wa kuzalisha na kuweza kulisha Tanzania na nchi za jirani kwani tunamalighafi za kutosha, mpaka sasa tumejihakikishia uzalishaji endelevu kwa kusaini mkataba na Wakala wa Misitu (TFS) wa miaka 30 ambapo tuna uhakika wa kukidhi uhitaji wa soko," alisema Mhandisi Chogo.

## EU yafunguka kisa uamuzi wa Rais Trump

**GENEVA,** Uswisi

UMOJA wa Ulaya (EU) umesema utautafakari uamuzi wa Rais wa Marekani, Donald Trump, wa kupiga marufuku safari kati ya Marekani na nchi za umoja huo, kama sehemu ya mkakati wa serikali yake kupambana na virusi vya corona.

Marufuku hiyo ambayo haiihusishi Uingereza isio tena mwanachama wa Umoja wa Ulaya, itadumu kwa siku thelathini na itaanza kuheshimiwa kuanzia usiku wa leo. Kupitia mtandao wa Twitter, Rais wa Baraza la Ulaya, Charles Michel, alisema chochote kinachoweza kuvuruga uchumi kinapaswa kuepukwa.

Michel amesema Umoja wa Ulaya unafanya kila juhudi kuzuia kuenea kwa homa ya virusi vya corona, ijulikanayo kama COVID-19, na unasaidia katika utafiti juu ya kirusi hicho.

Marufuku ya usafiri iliyotangazwa na Rais Trump itawahusu watu wote wasio raia wala wakazi wa nchini Marekani, lakini Ikulu ya Marekani, White House imesema haijumuishi bidhaa. **DW**

## DRC wapewa mbinu tahadhari ya corona

**KINSHASA,** DRC

WAZIRI wa Afya wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Dk. Eteni Longondo, ametoa wito kwa watu kuwa watulivu na kuzingatia usafi kwa kuosha mikono yao mara kwa mara kama tahadhari dhidi ya maambukizi ya homa ya corona..

Akizungumza na waandishi habari mjini Kinshasa siku ya Jumanne, Dk. Longondo ameuthibitishia umma kwamba mtu wa kwanza kuambukizwa na virus Corona anatibiwa mashariki mwa mji wa Kinshasa.

Mgonjwa huyo ni Mkongo wa miaka 52 anaishi Ufaransa, ambaye aliingia nchini humo siku ya Jumapili na alikuwa amewekwa karantini baada ya uchunguzi aliofanywa katika uwanja wa ndege wa Kinshasa kubaini kuwa ana ishara za mtu aliyeambukizwa na virusi hivyo.

Waziri wa Afya alisema hivi sasa serikali inawatafuta watu wote waliosafiri pamoja na mgonjwa huyo ili wapimwe na wawekwe karantini pindi watakapogunduliwa wameambukizwa na virus hivyo.

DRC ni nchi ya 11 ya Afrika kuthibitisha kwamba kuna wagonjwa walioambukizwa na virusi vya Covid-19 nchini mwao.

Dk. Longondo amesisitiza kwamba serikali inaimarisha juhudi za uchunguzi katika viwanja vyake vinne vikuu vya ndege kwa kuwakagua kwa makini wasafiri walio na viwango vya juu vya joto, hatua ambayo imekuwa ikichukuliwa kama sehemu ya kupambana na maambukizi ya virusi hatari vya ebola. **VOA**

# Corona yaathiri uchumi wa dunia

**VIENNA,** Australia

**Kwa wazalishaji wa kiasili wa mafuta wanaotegemea athari za mahitaji na ugavi haswa haswa Urusi na Saudia wanakutana na changamoto kubwa za kiushindani.**

VIRUSI vya corona vilivyoanzia katika jimbo la Wuhan nchini China na kuenea dunia nzima, vimesababisha tishio dhidi ya afya ulimwenguni, pamoja na hilo vimeanza kusababisha uchumi wa dunia uyumbe kwa kiasi kikubwa.

Baada ya virusi hivi kushambulia haswa China na mataifa mengine yaliyoendelea huku ikishuhudiwa uzalishaji ukipungua kwa kasi, matumizi kwa watu waliowekwa karantini nayo yameanza kupungua. Kutokana na hilo, kiuhalisia mahitaji ya mafuta na bidhaa nyingine nayo yameanza kupungua.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na IMF pamoja na Benki na mashirika mengine ya fedha ya kimataifa, uwezekano wa kutokea kwa anguko la kidunia ni mkubwa. Katika hali hiyo inatazamiwa kwamba kwa mwaka wote wa 2020 mahitaji ya mafuta yatapungua kwa kiasi kikubwa.

Shirika la nishati duniani linatazamia kwamba mahitaji ya mafuta yatapungua kwa mapipa milioni 3-4 kwa siku. Wakati katika soko la mafuta mahitaji yanatarajiwa kushuka kwa kiasi kikubwa, wazalishaji wa mafuta ya kwenye miamba wa Marekani wanaendelea kuongeza uzalishaji.

Marekani imeanza kuzalisha kati ya pipa milioni 12 hadi 13 kwa siku. Kutokana na maendeleo ya teknolojia inayohusiana na uzalishaji wa mafuta na gesi za kwenye miamba, gharama za uzalishaji wa mafuta hayo zinapungua kila siku. Kwa wazalishaji wa kiasili wa mafuta wanaotegemea athari za mahitaji na ugavi haswa haswa Urusi na Saudia wanakutana na changamoto kubwa za kiushindani.

Saudia inataka makubaliano ya Opec plus yaendelee ikiwezekana hata uzalishaji ushushwe kufikia mapipa milioni 1.5. Kwa upande wa Urusi wanachukulia kupunguza uzalishaji kutafaidisha mataifa washindani kama Marekani na hivyo kupelekea wao kupoteza sehemu yao ya soko kadiri siku zinavyozidi kwenda, kwa kuliona hilo Urusi haikutaka kusaini mkataba mpya.

Mkutano wa Opec uliofanyika Vienna ulimalizika bila mafanikio, na hatimaye wanachama wakaanza kutishiana misuli. Urusi na Sudia zote zimetangaza kuongeza uzalishaji wa mafuta. Katika hali hii inatazamiwa bei ya mafuta itapungua kwa asilimia 30.

Kwa mujibu wa wataalamu wa sekta husika, bei ya mafuta inaweza kushuka kufikia dola 20 kwa pipa. Bei itasababisha mtikisiko mkubwa wa uchumi katika nchi zinazozalisha mafuta. **TRT**



Mkuu Shirika la Afya Duninai (WHO), Dk. Tedros Adhanom Ghebreyes, ambaye ametangaza mlipuko wa corona kuwa janga la kimataifa. **PICHA: VOA**

## ICC yaanza hatua ya mwisho kesi ya bwana wa vita LRA

**KAMPALA,** Uganda.

MAJAJI kwenye Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu dhidi ya ubinadamu ya ICC, jana walianza kusikiliza maelezo ya mwisho kutoka kwa upande wa mashitaka na utetezi kwenye kesi inayomuhusu aliyekuwa kamanda msaidizi wa kundi la waasi wa Uganda la Lord Resistance Army (LRA), Dominic Ongwen.

Dominic Ongwen anakabiliwa na mashtaka kuhusu mauaji, mateso, ubakaji na watu kugeuzwa watumwa, mashtaka ambayo anatakiwa ajieleze mbele ya mahakama hiyo ya kimataifa.

Dominic Ongwen na kundi lake anatuhumiwa kuhusika na mauaji ya watu zaidi ya 100,000 tangu mwaka 1987 na kuwateka nyara maelfu ya watoto.

Anatakiwa ajibu mashtaka kuhusiana na uhalifu wa vita na uhalifu dhidi ya binadamu katika matukio 70 vilivyotokea kati ya mwaka 2002 na 2005 kaskazini mwa Uganda. Kesi yake ilifunguliwa kwa kuonyeshwa kanda za video na picha za miili ya watu iliyokatwa vipande vipande.

Mwendesha Mashtaka Mkuu, Fatou Bensouda, alimtaja Ongwen kuwa " katili na mbakaji" na kwamba miongoni mwa wenye kuamrisha katika kundi hilo la waasi,"yeye ndie aliyekuwa mkubwa kuliko wote." **RFI**

# Idadi kazi za usiku watoto wa kike yaongezeka

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

HALMASHAURI ya mji wa Kasulu, mkoani Kigoma ina idadi kubwa ya watoto wa kike wanafunzi wanaofanya kazi katika masoko ya usiku, jambo linalochangia tatizo la kimaadili na mimba za utotoni kufuatia takwimu kuonyesha kuanzia mwezi Januari hadi sasa tayari wanafunzi saba wameshapata ujauzito.

Akiongea wakati Shirika la Maendeleo ya Vijana Tanzania (Kivideа) likitambulisha mradi wa kuwajengea uwezo vijana katika masuala ya mimba za utotoni, ukatili na ugonjwa wa Ukimwi utakaojumuisha wilaya tatu za Uvinza, Manispaa ya Kigoma Ujiji na Kasulu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya mji wa Kasulu, Fatina Laay, alisema katika eneo hilo kuna watoto wengi wanao randaranda bila kwenda shule na wengine kufanya biashara usiku kuanzia saa moja hadi saa nne.

Laay aliyataka mashirika mbalimbali ya kijamii yaweke mpango wa kutoa elimu kwa wazazi ili watambue wajibu wao kwa kuwa wamekuwa chanzo cha kuchochea watoto wa kike kuharibikiwa tabia kwa kuwaruhusu kufanya shughuli mbalimbali kwenye maeneo ambayo si salama pamoja na kushindwa kuwatimizia mahitaji yao ya lazima.

"Hapa Kasulu ukienda masoko mengi ya usiku utawakuta watoto wa kike wakifanya biashara jambo hili hatuliungi mkono kwa kuwa lina madhara makubwa katika kushusha kiwango cha elimu na mimba za utotoni," alisema.

Mkurugenzi wa Kividea, Babu Paschal, alisema mradi huo unalenga kuwezesha kundi la vijana kujitambua na kuwa na uwezo wa kutatua changamoto za kimazingira zinazokwamisha ndoto zao za elimu na maendeleo.

Mradi huo ni wa miaka mitatu na utagharimu Dola za Marekani 240,000 (Sh. milioni 500), ukilenga zaidi kuwafikia vijana walio katika shule za msingi, sekondari na walio nje ya mfumo wa elimu wenye umri wa miaka 10 hadi 24.

Naye Paskazia Maro, mkazi mkoani humo alisema, wazazi wapewe elimu ya kutatua changamoto za uchumi ili waweze kukidhi kutoa mahitaji kwa familia zao pamoja na kuacha kuwatumia watoto kuongeza pato la familia.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC Tanzania, Theobald Sabi, akizungumza na baadhi ya wafanyakazi na wastaafu wa benki hiyo, katika hafla ya kuwaaga, iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Huduma ya Vodacom yaigusa serikali

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imeipongeza kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania kwa kubuni huduma rahisi itakayomsaidia mkulima kupata taarifa za hali ya hewa, pembejeo na masoko.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Tanzania, Kenneth Bengesi, alitoa pongezi hizo katika Wiki ya Ubunifu inayoendelea jijini Dar es Salaam.

Alisema serikali inathamini bunifu mbalimbali zinazofanywa na watu mbalimbali kwamba ipo haja ya kuendelea kuweka nguvu pia katika bunifu kwenye sekta ya kilimo.

Alisema ubunifu wa Vodacom utasaidia kuinua sekta hiyo ambayo ni uti wa mgongo kwenye uchumi wa taifa, ambayo inatoa ajira kwa vijana kwa asilimia kubwa.

"Sekta ya kilimo inachangia asilimia 27 ya pato la taifa licha ya ukuaji wake wa asilimia tatu kila mwaka. Serikali inaamini ubunifu ukiongezeka, kilimo kitakuwa bora zaidi na chenye tija," alisema Bengesi.

Alisema serikali imedhamiria kuwekeza zaidi katika miundombinu ya ubunifu na teknolojia kwenye kilimo kuanzia shambani hadi sokoni.

Mtaalamu Mshauri kwa wateja wakubwa wa Vodacom, Goodluck Moshi, alisema huduma hiyo ya ubunifu inaitwa M-Mkulima na imelenga kuondoa changamoto za ukosefu wa taarifa muhimu za kilimo.

"Hatujabadilisha utaratibu, tulichofanya ni kusogeza taarifa muhimu za kilimo kwa wakulima wetu wote, tumewalenga zaidi wakulima wadogo ambao ndio wengi hapa nchini," alisema.


SUKAH SECURITY CO. (T) LTD
AUCTION MART & COURT BROKER
(WATU WA KAZI)

HEAD OFFICE:
P.O. Box 10751, DVN Building,
Posta Road Mwanza.
Mob: 0754 860 435, 0715 860 435

Dealers in:
Day and Night Safe Guards,
Security Consultants,
Rapid Ambulance response,
Dog Unit and Mobile Patrolling,
Debt collector and General Auctioneers

KAGERA BRANCH:
P.O. Box 574,
Mobile: 0754 860 435
KARAGWE.

**NOTISI/ TANGAZO LA MNADA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA **CBA BANK SUKAH SECURITY AUCTION MART** TUNATANGAZA KUUZA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU WALIOSHINDWA KULIPA MIKOPO YAO KATIKA BENK TAJWA HAPO JUU KAMA WATASHINDWA KULIPA MADENI YAO NDANI YA SIKU (14) TANGU KUTOLEWA KWA TANGAZO HILI. MINADA ITAFANYIKA KAMA INAVYOONYESHA KWENYE JEDWALI HAPO CHINI

| NA. | JINA | DHAMANA | TAREHE | MUDA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | BARIKI CHARLES LYIMO | PLOT NO. 1892, BLOCK 'A' NYEGEZI SWEYA | JUMATATU 30/03/2020 | SAA NNE ASUBUHI |
| 2 | WILLIAM NZOHABONA | PLOT NO. 112, BLOCK 'A 111' KIRUMBA MWANZA CITY | JUMATATU 30/03/2020 | SAA SITA MCHANA |

**MASHARTI YA MNADA**

MNUNUZI ANATAKIWA KULIPA 25% PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU KUMI NA NNE (14).

***NYOTE MNAKARIBISHWA***

**KWA MAWASILIANO: 0754-860435 / 0767-372515**

215667702


## Zaidi ya wanafunzi 500 hawajaripoti sekondari

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WANAFUNZI 534 wa shule za sekondari mkoani Katavi hawajaripoti shuleni.

Akisoma taarifa ya wanafunzi walioripoti na ambao hawajaripoti jana katika kikao cha wadau wa elimu, Ofisa Elimu Mkoa wa Katavi, Newaho Mkisi, alisema wanafunzi waliochaguliwa ni 8,510 kati yao walioripoti ni 7,976 sawa na asilimia 93.7.

Alisema takwimu hizo zinafanya idadi ya wanafunzi wasioripoti kufikia 534 na kabla ya juzi waliokuwa wamefika shuleni ilikiwa asilimia 86 na jana imepanda kufikia 93.7.

"Mkuu wa mkoa, wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari ni 8,510, walioripoti ni 7,976 kwa hiyo mpaka kufikia jana (juzi) usiku, ni wanafunzi 534 ambao bado hawajaripoti," alisema Mkisi.

Alisema idadi ya wanafunzi ambao hawajaripoti katika kila halmashauri na idadi kwenye mabano ni Mlele (12), Tanganyika (143), Manispaa ya Mpanda (145), Mpimbwe (62) na Nsimbo (172).

Baada ya maofisa tarafa na watendaji wa kata kutoa sababu ya wanafunzi kutoripoti shuleni katika kata zao, ilibainika 245 wamehama makazi, 286 wanatafutwa walipo na wengine watatu wamepata ujauzito.

Walisema kuna baadhi ya wazazi wamechukuliwa hatua za kisheria mpaka watakaposema sehemu walipo watoto wao.

"Hatua tuliyochukua kuna baadhi ya wazazi tayari tumeshawakamata baada ya mahojiano walisema watoto wao wametoroka na hawajui waliko, hivyo tutaendelea kuwahoji hadi watakaposema watoto wao walipo," alisema mmoja wa maofisa hao.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, aliwataka maofisa hao kuunda kamati kwenye kila kata kwa ajili ya kufuatilia mienendo ya wanafunzi na watendaji wa kata walio mjini kuhamia kwenye katazo kuanzia leo.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BEATRICE ALOYCE GOHALIMU anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 570 BSU FUN CARGO. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DAR/KIJ/RB/226034/2020.

156664

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA
SHAURI LA MAOMBI YA ARDHI NA.55/2019
(Asilia Shauri LA Ardhi NA.5/2013 Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Mbeya)
EMMAUEL MDEKA........MWOMBAJI
DHIDI YA
1.EPHRAIM MBENJA.....MJIBU MAOMBI
2.FAIDA MBENJA.....MJIBU MAOMBI
3.SAIDI MWAIFWANI..MJIBU MAOMBI

Kwa:3.SADI MWAIFWANI
POPOTE ULIPO-TANZANIA

**KUITWA SHAURINI(MJIBU MAOMBI NA.3)**

Unaamriwa na Mahakama hii uhudhurie hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya wewe binafsi au wakili wako tarehe 15/04/2020 siku ya Jumatano saa 3:00 asubuhi,ambapo shauri limepangwa kutajwa.
ELEWA KWAMBA Ukikosa kufika siku hiyo shauri litapangwa kusikilizwa bila ya wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 24 Mwezi February,Mwaka 2020.

THE HIGH COURT OF TANZANIA

N.W. Mwakatobe
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

115666302

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo

MVOMERO-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;08/2020

Ombi la JUMANNE HABIBU MKALI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu OMARI RASHIDI MKALI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/03/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/03/20.

156676

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMAYA MWANZO CHAMWINO MJINI
USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11
(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
Katika mahakama ya Mwanzo CHAMWINO MJINI
Usimamizi wa Mirathi No. 19/2020.

Ombi la HAMISI SAID ALLY na ABDALAH SAID ALLY kuteuliwa kuwa
Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu SAID ALLY SUFIANI

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKANA MIRATHI HII.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja, kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 16/3/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo kama upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 05/03/2020

Tarehe 05/03 20 20

SAHIHI YA HAKIMU

115667102

---

NJOO

UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI

NAFUU SANA

**Uza, Chenye Thamani Kubwa**

**Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ARSENAL BADO YAKOMAA NA ZAHA




**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal bado imeonyesha nia yake ya kutaka kumsajili winga wa Crystal Palace, Wilfried Zaha.

Ofa za mwanzo za Arsenal zilikataliwa majira ya joto mwaka jana na sasa miamba hao wa dimba la Emirates wameonyesha kutokata tamaa ya kumuwania nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, tayari klabu yake ya Palace inaonekana kukubali yaishe kwa sababu imeshaanza kutafuta mrithi wa winga huyo na jina la staa wa Newcastle United, Allan Saint-Maximin ndilo linalotajwa zaidi kuja kurithi nafasi yake.

Lakini, kama Arsenal haitachangamka inaweza kuzidiwa kete na Bayern Munich inayofukuzia saini ya Zaha pia ambaye msimu huu kiwango chake kimetetereka kidogo kulinganisha na msimu uliopita ambapo alifunga mabao 10 na kupiga pasi za mwisho 10.

# Dele Alli atoa sababu kipigo Uefa kwa Spurs

**LONDON,** England

DELE Alli amebainisha kwamba, Tottenham Hotspur ilicheza chini ya kiwango na kusababisha kufungwa na RB Leipzig na kutupwa nje kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, Jumanne.

Kauli ya Dele inatokana na kipigo cha mabao 3-0 ilichopata Spurs kutoka kwa Leipzig na kutolewa katika hatua ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa kwa jumla ya mabao 4-0.

Makosa mawili ya kipa wa Spurs, Hugo Lloris yalikuwa faida kwa Leipzig iliyopata bao kupitia Marcel Sabitzer na Emil Forsberg.

Matokeo hayo yanahitimisha ndoto ya kocha wa Tottenham, Jose Mourinho pamoja na kikosi chao kurudia mafanikio yao ya msimu uliopita walipofanikiwa kucheza fainali ya mashindano hayo.

"Tulikosa wachezaji wazuri (Harry Kane na Son Heung-min ambao ni majeruhi), huo ni mpira tulitakiwa kujituma zaidi kwa ajili yao, lakini haikuwa hivyo leo (juzi)," Alli aliiambia BT Sport.

"Nadhani tunapaswa kuomba msamaha kwa mashabiki wetu. Walisafiri kuja hapa na wameondoka wakiwa na majonzi."

Alli alikataa kumnyoshea kidole kipa Lloris kwa kipigo hicho, lakini alidai Spurs hawakuwa na nguvu ya kiakili ya kupambana na kurudia yale mafanikio ya msimu uliopita walivyofanya kutoka 3-0 dhidi ya Ajax na kufanikiwa kushinda katika nusu fainali.


Tottenham sasa imebaki na michezo tisa katika Ligi Kuu England kuhakikisha inashinda ili kujihakikishia nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa kwa mara nyingine.

Vijana wa Mourinho watakuwa na kibarua kingine kizito Jumapili wakiwakaribisha Manchester United.

Mourinho alisema kukosekana kwa Kane na Son, Steven Bergwijn, Moussa Sissoko na Davinson Sanchez ni moja ya sababu ya timu yake kupoteza mchezo huo dhidi ya Leipzig.

"Watu wanaweza kusema ni sababu, lakini nina uhakika kwa timu yoyote kupoteza wachezaji wengi wa kikosi cha kwanza ni pigo."



# Drinkwater kutimuliwa Aston Villa

**LONDON,** England

KLABU ya Aston Villa imepanga kusitisha mkataba wake wa mkopo na Danny Drinkwater baada ya kiungo huyo kumpiga kichwa mwenzake, Jota mazoeni.

Villa ilimsajili kwa mkopo wa muda mrefu Drinkwater kutoka Chelsea, lakini kitendo chake cha kugombana mazoezini kimeifanya klabu hiyo kuamua kusitisha mapema mkataba huo.

Drinkwater amecheza mechi nne tangu ajiunge na Villa Januari katika mpango wa kuinusuru klabu hiyo na janga la kushuka daraja.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinadai kuwa Drinkwater alimpiga kichwa Jota katika mazoezi ya Jumanne na kuwatolea maneno makali wenzake.

Tukio la kiungo huyo mwenye umri wa miaka 30, kupigana na kutoa maneno makali kwa wenzake limesababisha viongozi hapo Villa Park kufikiria kukatisha mkataba wake haraka, lakini uamuzi wa mwisho kama arudishwe Chelsea bado haujawekwa wazi.

Pia, anaweza kukutana na adhabu kali kutoka Villa ikiwamo kupigwa faini kubwa.

# Klopp akataa kumlaumu Adrian Liver kutolewa Uefa

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amekataa kumlaumu Adrian kwa Liverpool kupoteza kwa Atletico Madrid, lakini alibainisha kwamba, makosa ya golikipa huyo yalikuwa na "athari kubwa".

Safari ya Liverpool kama bingwa mtetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya ilifikia tamati juzi, Jumatano baada ya kukubali kichapo cha 3-2 kwenye dimba la Anfield kwenye muda wa ziada na kufanya jumla ya uwiano kuwa 4-2.

Lakini miamba hao wa Ligi Kuu walionekana kama walikuwa na nafasi ya kutinga robo fainali baada ya mabao ya Georginio Wijnaldum na Roberto Firmino kuwaweka mbele, hata hivyo makosa ya Adrian yakasababisha Marcos Llorente kuifungia bao Atletico.

Llorente aliongeza la pili kabla ya Alvaro Morata kufunga la ushindi dakika za majeruhi wakati Liverpool walipofungwa nyumbani kwenye Ligi ya Mabingwa kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2014.

Licha ya kosa la Adrian, Klopp hakuwa tayari kumlaumu golikipa huyo, lakini alisema kipa huyo mwenye umri wa miaka 33, alijua makosa yake.

"Yeye ni binadamu na anajua makosa yake," kocha huyo wa Liverpool alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Hatutamlaumu kwa mara ya pili, anatakiwa kuheshimiwa kama mwanzo, katika soka makosa ni jambo la kawaida."






# SIMEONI: OBLAK NI MESSI WA MAKIPA

**LIVERPOOL,** England

DIEGO Simeone amemlinganisha Jan Oblak na nyota wa Barcelona, Lionel Messi baada ya golikipa huyo kuonyesha kiwango cha kuvutia wakati Atletico Madrid ikiwatupa nje Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Liverpool.

Oblak alitajwa kuwa nyota wa mchezo huo kutokana na hatari alizookoa wakati Atletico ikiibuka na ushindi wa mabao 3-2 kwenye muda wa ziada pale kwenye dimba la Anfield.

Liverpool walikuwa kwenye kiwango cha juu katika mchezo huo wa hatua ya 16-bora, lakini Oblak alikuwa kizingiti kwako na kuwawezesha Atletico kufuzu kwa ushindi wa uwiano wa mabao 4-2, shukrani kwa mabao ya Marcos Llorente aliyefunga mawili na Alvaro Morata.

Akiwa anachukuliwa kama mmoja wa makipa bora duniani, Oblak alisifiwa na Kocha Mkuu wa Atletico, Simeone kutokana na kiwango chake.

"Tuna golikipa ambaye ni bora duniani, bila shaka yoyote," alisema Simeone. "Nimekuwa nikisema hivyo kwa muda mwingi.

"Ni kama Barcelona ambayo ina Messi. Anaamua matokeo ya mchezo kwa staili yake ya uchezaji; Oblak yeye anaamua matokeo kwa kuokoa."

# *Tuchel aelezea furaha PSG ikitinga robo fainali*

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, ameelezea furaha yake baada ya ushindi wa timu yake dhidi ya Borussia Dortmund, wakati vinara hao wa Ligi Kuu Ufaransa wakitinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka minne sasa.

Tangu 2016 PSG haijatinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini safari hii walifuzu baada ya kuifunga Dortmund 2-0 kwenye mchezo ambao haukuhudhuriwa na mashabiki kwa hofu ya maambukizi ya virusi vya corona.

Neymar na Juan Bernat kila mmoja alifunga bao moja kipindi cha kwanza kwa kuwawezesha PSG kupindua matokeo ya 2-1 ya mchezo wa kwanza.

Baada ya mchezo huo, Tuchel aliwaambia waandishi wa habari: "Kwa uhakika lilikuwa jambo la kufurahisha na kushangaza. Timu ilikuwa imara na tulijiamini na ndio maana tumeshinda.

"Baada ya timu kuanza kuimba, tuliimba pamoja, kulikuwa na hamasa kubwa, ilikuwa hali ya hewa ya kuvutia na mchezo ulikwenda vizuri kabisa.

"Mazingira yale yalitufurahisha na tuliyahitaji kama yale, kwani presha ya timu yetu ilipungua na kuwa ya kawaida."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RUGANI AUGUA CORONA, RONALDO AJIFUNGIA URENO

## Aibuka na kufunguka, WHO watangaza sasa corona ni janga la kidunia...

**TURIN,** Italia

BEKI wa kati wa Juventus, Daniele Rugani amesema yupo "sawa" baada ya nyota huyo wa kimataifa wa Italia hofu kutanda kufuatia kubainika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona 'coronavirus'.

**Rugani alipimwa na kuonekana ana maambukizi chanya ya COVID-19, lakini havikuonyesha dalili yoyote, mabingwa wa Serie A, Juve waliweka bayana jana, Jumatano.**

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, aliambukizwa virusi hivyo kufuatia wiki iliyopita kuvaana na mahasimu wao Inter, na ikiwa ni siku sita tu kabla ya Juve kucheza na Lyon katika mechi ya mkondo wa pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.

"Utakuwa umesoma habari hizo na ndio maana nataka kuwahakikishia wale wote wenye hofu na mimi, niko sawa," Rugani aliandika kupitia mtandao wa kijamii.

"Ninawasihi kila mtu aheshimu sheria, kwa sababu virusi hivi havina tofauti yoyote! Wacha tuifanye sisi wenyewe, kwa wapendwa wetu na kwa wale wanaotuzunguka #asante."

Na wakati Rugani akiripotiwa kubainika kuwa na maambukizi hayo, mshambuliaji wa timu hiyo, Cristiano Ronaldo hakufanya mazoezi na wenzake wa Juventus jana na ameendelea kubaki Madeira, Ureno akisikilizia maendeleo juu ya mlipuko wa corona.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno, Ronaldo alirudi nyumbani kwao mapema wiki hii kwa ajili ya kuangalia afya ya mama yake ambaye alipatwa na kiharusi mapema mwezi huu.

Na kutokana na zuio la kusafiri ndani na nje ya Italia ili kuzuia kuenea kwa corona, na sasa Shirika la Afya Duniani (WHO), jana likiutangaza ugonjwa huo kama janga la dunia, mabingwa hao wa Serie A, Juve hawana uhakika ni lini mshambuliaji wao huyo atarejea Turin. Taarifa ya klabu hiyo ya Italia katika tovuti yao ilisomeka: "Cristiano Ronaldo hakufanya mazoezi [Jumatano, jana] na ameendelea kubaki Madeira akiendelea kusikilizia maendeleo ya sasa ya kiafya ya dharura."

Hakuna nchi nyingi nje ya China ambayo imeathiriwa sana na virusi hivyo, ambavyo vilianzia mjini Wuhan nchini humo Desemba mwaka jana.

Italia imechukua hatua kwa nguvu zote na serikali ya nchi hiyo imesimamisha shughuli zote za kimichezo hadi Aprili 3, mwaka huu.

Kwa mujibu wa WHO, Italia ina zaidi ya wagonjwa 12,000 walioambukizwa virusi vya corona na vifo vilivyoripotiwa kutokana na gojwa hilo ni zaidi ya 800.

## ZISIKUPITE

### AWAPOZA ARSENAL

PIERRE-Emerick Aubameyang amesema ni mwenye furaha hapo Arsenal. Kumekuwa na tetesi zikimhusisha nyota huyo wa kimataifa wa Gabon mwenye umri wa miaka 30 kwenda kujiunga na Barcelona. ***(Mirror)***

### KUZIGONGANISHA UNITED, CITY

MANCHESTER City na Manchester United zitavaana uso kwa uso katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane, 26, kwa pauni milioni 150 majira haya ya joto. ***(90min)***

### WATAKA EURO 2020 IAHIRISHWE

WAWAKILISHI wa Bundesliga, Serie A, La Liga na Ligue 1 wataiomba Uefa kuahirisha michuano ya Euro 2020 katika mkutano utakaofanyika kwa njia ya video leo, Alhamisi. ***(Football Italia)***

### JUVE KUMFUATA KANE SPURS

JUVENTUS nayo inaitaka huduma ya mshambuliaji wa kimataifa wa England na Tottenham, nahodha Harry Kane hapo Turin majira haya ya joto ili kucheza pembeni ya Cristiano Ronaldo. ***(Tuttosport - in English)***

### SANCHO AFUNGULIWA MLANGO

BORUSSIA Dortmund itamruhusu Jadon Sancho kuondoka majira haya ya joto kama ataomba kuondoka. Winga huyo wa England, 19, anatakiwa na Liverpool, Manchester United na Chelsea. ***(Standard)***

### CHELSEA, SPURS VITANI

CHELSEA na Tottenham zote zinavutiwa kumsajili kipa wa Bournemouth, Aaron Ramsdale, 21. ***(Mail)***

### BOGA AGEUKA LULU ULAYA

CHELSEA na Tottenham zinamtaka winga wa Ivory Coast, Jeremie Boga, 23. Nyota huyo wa zamani wa Chelsea anaweza kuzigharimu pauni milioni 13 kutoka kwa klabu yake ya Italia, Sassuolo, wakati huu Borussia Dortmund na Valencia pia zikivutiwa naye. ***(Sun)***

### ARSENAL, SPURS KWA MARCEL

ARSENAL na Spurs zinajiandaa kuingia vitani kuiwania saini ya Marcel Sabitzer, 25, kutoka RB Leipzig. Nyota huyo wa kimataifa wa Austria alifunga mara mbili dhidi ya Spurs katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi, Jumanne. ***(Calcio Mercato - in English)***

### WILLIAN AWINDWA BAYERN

BAYERN Munich inavutiwa na kiungo wa Chelsea, Willian. Kiungo huyo raia wa Brazil mwenye umri wa miaka 31, atamaliza mkataba wake hapo Stamford Bridge majira haya ya joto. ***(Sun)***

### ASTON VILLA YAMFUATA GRANT

ASTON Villa na West Brom zote zinataka kumsajili mshambuliaji Karlan Grant kutoka Huddersfield. Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amefunga mabao 16 kwenye Ligi Daraja la Kwanza England 'Championshi' msimu huu. ***(Sky Sports)***

### TELLES ATEGWA CHELSEA

CHELSEA itajaribu kumsajili beki wa Porto, 27, Alex Telles, kama itashindwa kumnasa Ben Chilwell. Mchezaji huyo wa Leicester mwenye umri wa miaka 23, ni chaguo lao la kwanza katika nafasi ya beki wa kushoto. ***(Star)***

# HABARI MICHEZO

## Tanzania kamili yaifuata Uganda

**Na Somoe Ng'itu**

TUNAENDA vitani! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17, Bakari Shime kuelekea mchezo wa marudiano dhidi ya wenzao wa Uganda utakaochezwa kesho, Jumamosi kwenye Uwanja wa KCCA Lugogo jijini Kampala.

Uganda inawakaribisha Tanzania katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia za U-17, zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini India.

Kikosi hicho cha Tanzania kinatarajia kuondoka nchini leo mchana kikiwa na wachezaji 20 pamoja na viongozi mbalimbali wa Shirikisho la Soka nchini (TFF).

Akizungumza na gazeti hili jana, Shime alisema kuwa wamejiandaa kwenda kucheza kwa tahadhari na kujilinda zaidi ili kujihakikishia matokeo mazuri katika mchezo huo wa marudiano.

Shime alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu wenyeji wao wataingia na "hasira" ya kulipiza kisasi baada ya kuwaondoa katika michuano mingine ya umri chini ya miaka 20.

"Kimsingi maandalizi ya timu yako vizuri na wachezaji wote wako katika hali nzuri, sina majeruhi na wamejiandaa kwenda kuulinda ushindi wao, hatutaruhusu wapate bao, hii itatusaidia kujihakikisha kusonga mbele," alisema Shime.

Naye Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Edna Lema, alisema wamejiandaa kupeperusha vema bendera ya Tanzania na watakwenda Uganda kumalizia kazi waliyoianza nyumbani baada ya mchezo wa awali kushinda 2-1, mabao yote ya kikosi cha Shime yakifungwa na mshambuliaji kinara, Aisha Masaka.

## Tshishimbi: FA yetu, Simba bingwa Bara

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuishuhudia Simba ikiendelea kupaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 71, ikiwa ni 21 zaidi yao, kiungo na nahodha wa Yanga, Papy Tshishimbi amesema kupata ubingwa wa Ligi Kuu ni ndoto, na badala yake wanaliwazia zaidi Kombe la Shirikisho, FA Cup.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Tshishimbi alisema mawazo yao kwa sasa ni Kombe la FA ili kuweza kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika na si ubingwa wa Ligi Kuu ambao bingwa hushiriki Ligi ya Mabingwa.

"Kwa sasa hivi tunaiwazia michuano ya Kombe la Shirikisho, lakini kwa ubingwa wa Ligi Kuu, si rahisi japokuwa ligi bado inaendelea," alisema Tshishimbi.

Nahodha huyo alisema kuna changamoto nyingi ambazo zilichangia kwa kiasi kikubwa timu yao kuanza vibaya msimu huu, lakini hawana budi kuziweka kando na kuelekeza akili zao kwenye Kombe la FA.

"Changamoto ya kubadilishiwa kocha ili.tuchanganya sisi wachezaji, nashukuru sasa hivi timu inaenda sawa," alisema.

Aidha, Tshishimbi aliwataka mashabiki kuendelea kuiunga mkono timu na kuacha kufuatilia mambo yanayoandikwa kwenye mitandao kwa kile alichodai kwamba kinaangusha uwezo wa mchezaji husika pamoja na kubagua wachezaji wengine.

# KAGERE KUVUNJA REKODI YA 'KIATU' MSIMU ULIOPITA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuitungua Singida United mabao manne wakati wakishinda 8-0 juzi katika Uwanja wa Uhuru, mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere amesema lengo lake ni kuvunja rekodi yake ya msimu uliopita kwa kufunga zaidi ya mabao 23 kwenye Ligi Kuu Bara.

Msimu uliopita Kagere alimaliza akiwa na mabao 23 na kuibuka mshindi wa Kiatu cha Dhahabu kwenye Ligi Kuu, na hadi sasa tayari ameshacheka na nyavu mara 19 wakati huu Simba ikiwa imebakiza mechi 10 klaba ya msimu kumalizika.

**Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Kagere alisema malengo yake yalikuwa kwanza kufikia mabao 23 ya msimu uliopita ambapo amebakiza manne aliyopania kuyatafuta katika michezo zilizobaki ili kufikia kile alichokidhamiria kabla ya kuvunja rekodi yake hiyo.**

Alisema ana imani kubwa ya kufanya vizuri katika michezo ijayo na kuhakikisha anatumia vema nafasi wanazopata kufikisha mabao hayo 23 msimu huu.

"Najipa changamoto mwenyewe, nitakapofikisha mabao ya msimu uliopita, nitapambana kuvuka idadi hiyo, nina imani hakuna atakayeweza kufikisha mabao hayo 23," alisema Kagere.

Alisema ana imani kubwa katika michezo iliyobaki ana uwezo wa kufikisha idadi hiyo kutokana na changamoto anazojipa mwenyewe.

Kagere alisema kila msimu hujiwekea malengo, na lengo la sasa ni kufikisha mabao 23 na kuyavuka.




Mshindi wa Jackpot ya SportPesa ya zaidi ya Sh. milioni 437, Yassin Ridhiwani Ally, akiwa na mwanawe na mkewe, Rehema Omary wakati akikabidhiwa mfano wa hundi ya kitita hicho na Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas (kulia). **PICHA: SPORTPESA**

# *Mke mshindi Jackpot afungukia mamilioni*

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akiendelea kufurahia ushindi wa mumewe, Yassin Ridhiwani Ally, mke wa mshindi huyo wa Jackpot ya SportPesa ya zaidi ya Sh. milioni 437, Rehema Omary amesema malengo yao ni kutumia kiasi cha fedha hizo kumiliki mjengo wa maana watakaoishi na familia yao.

Rehema ametoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni wiki chache tangu mumewe ashinde mamilioni hayo baada ya kubashiri kwa usahihi mechi zote 13 na kujishindia kitita cha zaidi ya Sh. milioni 437.

Akizungumza kwenye ofisi za SportPesa, jijini Dar es Salaam, Rehema alisema yeye na mume wake hawataki kukosea katika maisha yao na kikubwa ni kuhakikisha wanatimiza ndoto zao za kumiliki nyumba yao baada ya kupanga kwa muda mrefu.

Rehema alisema anajisikia furaha kuona hivi karibuni wakitarajia kumiliki nyumba yao wenyewe ya kuishi na familia yao baada ya mumewe kupata ushindi huo wa mamilioni.

Aliongeza kuwa hadi mume wake anapata ushindi huo alivumilia mengi ikiwamo kumuacha sebuleni peke yake kwa muda mrefu, huku akipata hofu ya kuchati na watu wake usiku wakati akicheza na SportPesa.

"Nina furaha kubwa kuona ndoto zetu mimi na mume wangu zikitimia kwa kiasi kikubwa, awali ndoto yetu kubwa ilikuwa ni kumiliki nyumba yetu wenyewe tukiwa na familia yetu.

"Hatimaye zimefanikiwa baada ya mume wangu kubashiri vema Jackpot ya SportPesa na kushinda, haikuwa rahisi kwake kupata ushindi huo, hivyo nampongeza sana mume wangu kupitia ushindi wake huo kwani utabadili maisha yetu.

"Nilikuwa namuacha muda mrefu sebuleni usiku akiwa anacheza na SportPesa, awali nilikuwa naingia hofu anafanya kitu gani sebuleni, nikawa nahisi kuwa muda huo anautumia akiwa pekee kwa ajili ya kuchati na watu wengine, kumbe haikuwa hivyo," alisema Rehema.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas alisema: "Tunajisikia furaha kuona tukiboresha maisha ya Watanzania kupitia mchezo huu wa kubashiri.

"Niwatake Watanzania waendelee kucheza na SportPesa ili wajishindie pesa na wasikate tamaa katika kucheza kwani wanavyocheza mara nyingi wanajitengenezea nafasi nzuri ya kujishindia mamilioni kama ilivyokuwa kwa Yassin ambaye ninaamini maisha yake yatabadilika baada ya ushindi huo," alisema Tarimba.

Jackpot ya wiki hii ni shilingi 241,916,240, na kila mtu ana nafasi ya kujishindia mamilioni hayo kwa kubashiri kwa usahihi kupitia SportPesa.

# Michezo

Ijumaa Machi 13, 2020

Nipashe




Rugani augua corona, Ronaldo ajifungia Ureno UKURASA 30

TUMESHIKWA...



Kiungo wa Yanga, Papy Tshishimbi, akimiliki mpira huku akizongwa na mchezaji wa KMC, Ismail Gambo, katika mchezo wa Ligi Kuu uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. KMC ilishinda 1-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Sven alia Singida kupigwa chache

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya Simba kuibuka na ushindi wa mabao 8-0 katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Singida United iliyopigwa Uwanja wa Uhuru juzi, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Sven Vandenbroeck amesikitikia baadhi ya nafasi wazizozikosa za kucheka na nyavu zaidi.

Simba ikitoka kuchezea kichapo cha bao 1-0 dhidi ya watani zao, Yanga, juzi ilishuka uwanja wa Uhuru ikiwa na njaa ya ushindi na kuiangamiza Singida United kwa mabao hayo shukrani zikiwaendea Meddie Kagere aliyefunga manne, Deo Kanda (mawili), John Bocco na Sharaf Shiboub waliofunga bao moja moja.

Akizungumza na Nipashe, Sven alisema alitamani kuona wakifunga zaidi kwa kutumia nafasi walizozipoteza ili kupata ushindi mkubwa kuliko huo.

"Ninafuraha kwa ushindi tulioupata na ninawapongeza wachezaji wangu, kwani licha ya kufanya mabadiliko makubwa katika kikosi chetu bado tuliweza kushinda, hata hivyo kuna nafasi ambazo tulishindwa kuzitumia kufunga zaidi, inatakiwa kila unapopata nafasi ya kufunga ufunge zaidi," alisema.

Sven alisema ushindi huo umezidi kuwaweka katika nafasi nzuri wakati huu wakielekea katika mapumziko ya kupisha ratiba za mechi za kimataifa na ana imani wakirejea wataendeleza mbio zao za ubingwa.

Simba ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 71 baada ya mechi 28, huku ikifuatiwa na Azam FC yenye alama 54 katika idadi hiyo ya mechi, na watani zao Yanga wakiwa nafasi ya tatu na pointi 5o kabla ya mchezo wao wa 26 jana dhidi ya KMC FC.

# *Furaha Yanga yaishia K'ndoni*

## ●●● Simba roho kwatu wadai watani zao ni maji kupwa kujaa, kelele nyingi lakini...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuwachapa watani zao wa jadi Simba bao 1-0 Jumapili iliyopita, timu ya Yanga jana ilikiona cha moto ilipokubali kipigo kama hicho dhidi ya KMC ya Kinondoni kwenye mfululizo wa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayozidi kuyoyoma.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Uhuru, lilikuwa ni bao la mshindi wa pili wa ufungaji bora msimu uliopita, Salim Aiyee alipozamisha mpira kimyani kwa ustadi dakika ya 62, baada ya mabeki wa Yanga kudhani ameotea.**

Bao hilo lilitokana na mabeki wa Yanga kujichanganya na kumwachia Aiyee aliyekuwa amejiweka pembeni ya msitu wa wachezaji wa timu zote mbili, kabla kupewa pasi safi na kumchambua kipa Metacha Mnata.

Katika mechi hiyo ya jana, KMC ingeweza kuondoka na ushindi mnono kama mastraika wake wangekuwa makini. Kwani ilikuwa ni dakika ya pili tu, Kelvin Kijili alipoambaa na mpira wingi wa kulia na kuachia kombora kali lililopita nje kidogo ya lango la Yanga.

Kama vile haitoshi dakika ya 20, Hassan Kabunda alikosa utulivu kwenye mechi hiyo, alipopewa pasi safi na Kijili akiwa anatazamana na kipa Metacha, lakini alipiga mpira hafifu.

Dakika tano baadaye Kabunda tena aliikosesha timu yake bao la wazi, baada ya kumiminiwa krosi safi iliyokuwa inahitaji kuguswa tu, lakini alipiga fyongo na mpira ukaambaa pembani ya uwanja.

Yanga ilizinduka dakika ya 29, wakati Papy Tshishimbi alipopiga 'tik-tak' baada ya mpira wa kona, lakini uliishia kwa kipa mahiri wa KMC, Jonathan Nahimana.

Kipindi cha pili Yanga ilitawala kwa dakika 30, lakini KMC ilizinduka dakika 15 za mwisho na kama wachezaji wake wangekuwa makini, huenda kipigo kama kile cha mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar kingetokea.

Charles Ilamfya aliyeingia badala ya Aiyee alikosa mabao mawili ya wazi dakika ya 86 akiwa ana kwa ana na Metacha, lakini alipiga shuti kubwa, huku nafasi nyingine akimlamba chenga kipa huyo, na ilionekana kama aliangushwa, lakini mwamuzi Elly Sasi alitafsiri kuwa alijiangusha.

Nafasi nzuri zaidi ya Yanga kusawazisha ilikuwa dakika ya 78 wakati Mapinduzi Balama alipovunja mtego wa kuotea wa walinzi wa KMC na kubaki na kipa Nahimana ambaye alifanya kazi kubwa ya kuupoza mpira uliodokolewa na mchezaji huyo ili utinge wavuni.

Kwa matokeo hayo, Yanga inabaki na pointi zake 50 huku ikiwa imecheza mechi 26, ikisalia kwenye nafasi ya tatu, lakini KMC ikichupa mpaka kwenye nafasi ya 16, kwa kufikisha pointi 30, ikicheza mechi 28, wakati huu ikiwa katika harakati ya kujiepusha kwenye janga la kushuka daraja.

Ushindi huo wa KMC pia umepokelewa kwa mikono miwili na mashabiki wa Simba, ambao juzi walikuwa wakitaniwa vibaya na watani zao hao kuwa kushinda kwao mabao 8-0 dhidi ya Singida United ni sawa na kutupa bomu mochwari ujigambe umeua wakati zilizopo eneo hilo ni maiti.

"Walitamba sana na waliahidi leo [jana], watashinda dhidi ya KMC, hawa jamaa ni maji kupwa kujaa, mbona wameishindwa KMC iliyokuwa nafasi ya tatu kutoka mkiani?" Alihoji shabiki wa Simba aliyejitambulisha kwa jina la Salum Bakari.

Naye Ally Masalu, alisema: "Hawa jamaa walituotea tu, sasa kelele zao mwisho Kinondoni, wakati sisi tunatamba kila kona nchini."

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042